كنز الفؤائد والمجربات في قضاء الحوائج

تجميع وانتاج

المستكشف أبومنال دانا

KANZ AL FAWAID WA AL MUJARRABAT FII QADHAI AL HAWAIJ

Hazina ya Faida Na Mujarabati Katika Kufanikisha Mambo Mbali Mbali

المستكشف أبو منال دانا

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

KIMETAYARISHWA NA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

1445 A.H - 2023 CE

كنز الفوائد والمجربات

في قضاء الحوائج

تجميع وانتاج
المستكشف أبومنال دانا

KANZ AL FAWAID WA AL MUJARRABAT FII QADHAI AL HAWAIJ.

HAZINA YA FAIDA NA MUJARABATI KATIKA KUFANIKISHA MAMBO MBALI MBALI.

المستكشف أبو منال دانا
AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

KIMETAYARISHWA NA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH
KIMECHAPISHWA NEW DELHI, INDIA.
MWAKA *1445 AL HIJRA – 2023 C.E*

المستكشف أبو منال دانا
AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

§——————————————§§——————————————§

إنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ نَحْمَدُهُ ونَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُضْلِلْ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Inna Al-hamda Lillaahi nahmaduhu wanasta'eenahu wa nastaghfiruhu, wa na'oodhu billaahi min shuroori anfusinaa wa min sayi'aati a'maalinaa. Man yahdih - Illaahu falaa mudhilla laahu wa man yudhlil falaa haadiya lahu. Wa ashhadu an laa ilaaha ill-Allaahu wahdahu laa shareekallahu, wa ashhadu anna Muhammadan 'Abduhu wa Rasooluhu.

Tafsir: ***Kwa jina la Allah, ambae kwa hakika ndie anastahiki shukrani zote, tunaemuomba msaada na msamaha wake. Tunajilinda kwa ulinzi wa Allah na kila maovu ya Nafsi zetu na mambo mabaya yetu. Kwani kwa hakika mtu yeyote yule alieongozwa na Allah basi hakuna atakaempotoa, na aliepotoshwa na Allah basi hakuna atakaemuongoa. Nnashuhudia kua hakuna anaepaswa kuabudiwa isipokua Allah pekee asiekua na mshirika, na nnashuhudia kua Muhammad (Salallahu A'layhi wa Salam) ni Mja wake na ni Mtume wake.***

يَقُولُ اللهُ عَزَّ وَجَلَّ

﴿يأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha haqqa tuqatihi wala tamootunna illa waantum muslimoona *(Surat Al Imran 3:102)*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Muogopeni Allah (kwa kutekeleza maamrisho yake na kuachana na makatazo yake) kama anavyotahiki kuogopewa. (Mtiini, mshukuruni na daima mkumbukeni), na msife isipokua mkiwa katika hali ya kua ni Waislam.***

﴿يَأَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُواْ رَبَّكُمُ الَّذِى خَلَقَكُمْ مِنْ نَّفْسٍ وَحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالاً كَثِيراً وَنِسَآءً وَاتَّقُواْ اللَّهَ الَّذِى تَسَآءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيباً﴾

Ya ayyuha alnnasu ittaqoo rabbakumu alladhi khalaqakum min Nafsin wahidatin wakhalaqa minha zawjaha wabaththa minhuma rijalan kathiran wanisaan waittaqoo Allaha alladhii tasaaloona bihi waal-arhama inna Allaha kana AAalaykum raqeeban *(Surat An Nisaa 4:1)*

Tafsiri: ***Enyi Watu! Mcheni Mola wenu aliekuumbeni kutokana na Nafsi moja (Adam), na kutokana nae (Adam) akamuumba mke wake (Hawa), na kutokana nao (Adam na Hawa) akawaumba Wanaume na Wanawake wengi na muogopeni Allah ambae ana haki juu yenu, na msivunje udugu, kwani kwa Hakika Allah ni mwenye uangalifu mkubwa juu yenu.***

﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ وَقُولُواْ قَوْلاً سَدِيداً ❁ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَلَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَن
يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزاً عَظِيماً﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha waqooloo qawlan sadeedan, Yuslih lakum aAAmalakum wayaghfir lakum dhunoobakum waman yutiAAi Allaha warasoolahu faqad faza fawzan AAadhiman *(Al Ahzab 33:70-71)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini! mcheni na muogopeni Allah, na (daima) semeni kauli za ukweli ulionyooka, atakuongozeni kufanya mema na kukusameheni dhambi zenu. Na kwa hakika yeyote yule ambae anaemtii Allah na Mtume wake (Salallahu A'layhi wa Salam) basi atakua ni miongoni mwa waliofuzu.***

Allahuma Ij'Aalna minna al faizin fawzan A'adhimah…Aamin

قَالَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ:فَإِنَّ أَصْدَقَ الْحَدِيثِ كِتَابُ اللَّهِ، وَأَوْثَقَ الْعُرْيِ كَلِمَةُ التَّقْوَى، وَخَيْرَ الْمِلَلِ
مِلَّةُ إِبْرَاهِيمَ، وَخَيْرَ السُّنَنِ سُنَنُ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، وَأَشْرَفَ الْحَدِيثِ ذِكْرُ اللَّهِ تَعَالَى،
وَأَحْسَنَ الْقَصَصِ هَذَا الْقُرْآنُ

Qala Rasul Allahi Salallahu A'alayhi wa Salam: fa'inn 'asdaqa alhadith kitab allahi, wa'awthaq al'aAuryi kalimat alttaqwaa, wakhayr almilal millat 'Ibrahima, wakhayr alssunan sunan Muhammad Sala Allahu Alyhi wa Salam, wa'ashraf alhadith dhikr allah taalaa, wa'ahsan alqasas hadha al Quran.

Amesema Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam kua:* Kwa hakika hadith za kweli kabisa ni za Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na kauli zenye uzito ni kauli zenye Taqwa, na Mila bora ni *Milat Ibrahima,* Na Sunna bora ni Sunna za Muhammad (*Sala Allahu Alayhi wa Salam) na Maneno Matukufu ni Dhikr Allah Ta'ala na* Visa bora ni hii *Qur'an.

وَيَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ

﴿وَبِٱلْحَقِّ أَنْزَلْنَاهُ وَبِٱلْحَقِّ نَزَلَ وَمَآ أَرْسَلْنَاكَ إِلاَّ مُبَشِّراً وَنَذِيراً❁وَقُرْآناً فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ عَلَى ٱلنَّاسِ عَلَىٰ
مُكْثٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنْزِيلاً❁قُلْ آمِنُواْ بِهِ أَوْ لاَ تُؤْمِنُوۤاْ إِنَّ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْعِلْمَ مِن قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ
لِلأَذْقَانِ سُجَّداً❁وَيَقُولُونَ سُبْحَانَ رَبِّنَآ إِن كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولاً❁وَيَخِرُّونَ لِلأَذْقَانِ يَبْكُونَ وَيَزِيدُهُمْ
خُشُوعاً❁قُلِ ٱدْعُواْ ٱللَّهَ أَوِ ٱدْعُواْ ٱلرَّحْمَـٰنَ أَيّاً مَّا تَدْعُواْ فَلَهُ ٱلأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ وَلاَ تَجْهَرْ بِصَلاَتِكَ وَلاَ

تُخَافِتْ بِهَا وَٱبْتَغِ بَيْنَ ذَٰلِكَ سَبِيلاً۝وَقُلِ ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى لَمْ يَتَّخِذْ وَلَداً وَلَم يَكُنْ لَّهُ شَرِيكٌ فِى ٱلْمُلْكِ
وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ وَلِيٌّ مِّنَ ٱلذُّلِّ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيراً۝

Wabialhaqqi anzalnahu wabialhaqqi nazala wama arsalnaka illa mubashshiran wanadheeran, Waqur-anan faraqnahu litaqraahu AAala alnnasi AAala mukthin wanazzalnahu tanzeelan, Qul aminoo bihi aw la tu/minoo inna alladheena ootoo alAAilma min qablihi idha yutla AAalayhim yakhirroona lil-adhqani sujjadan; Wayaqooloona subhana rabbina in kana waAAdu rabbina lamafAAoolan; Wayakhirroona lil-athqani yabkoona wayazeeduhum khushooAAan; Quli odAAoo Allaha awi odAAoo alrrahmana ayyan ma tadAAoo falahu al-asmao alhusna wala tajhar bisalatika wala tukhafit biha waibtaghi bayna dhalika sabeelan, Waquli alhamdu lillahi alladhee lam yattakhidh waladan walam yakun lahu shareekun fee almulki walam yakun lahu waliyyun mina aldhdhulli wakabbirhu takbeeran *(Surat Al Isra 17:105-111)*

Tafsir: ***Na kwa haki tumeiteremsha chini (Hii Qur'an) na kwa haki imeshuka, na tumekutuma wewe (Muhammad) si kwa chochote isipokua kwa ajili ya kuweka wazi na kuonya. Na hii Qur'an ambayo tumeigawa (katika aya na sura tofauti) ili upate kuisoma kwa watu kwa makusudio. Na tumeishusha hii (Qur'an) kwa vituo (tofauti). Sema (Ewe Muhammad): 'Iaminini au msiiamini. Kwani kwa hakika wale waliopewa Ilm kabla yake (Ilm ya Ahl Al Kitab kina Abd Allah Ibn Salam Radhi Allahu Anhu, Salman Al Farsi Radhi Allahu Anhu n.k)' waliposomewa, walianguka chini kwa nyuso zao kwa Unyenyekevu wa Kusjudu. Na wakasema: 'Utukufu ni Wa Allah Pekee. Ahadi ya Mola wetu ni lazime iwe ni yenye kutekelezwa'. Na wakaanguka kwa nyuso zao wakilia machozi na hii ilizidisha Unyenyekevu wao. Sema (Ewe Muhammad) Muombeni Allah, au muombeni Ar Rahmani, au kwa jina lolote (Katika Majina yake Matukufu), kwani kwake yeye ndio kwenye umiliki wa Majina Matukufu, na Salini bila ya kufanya kelele au kwa sauti ya chini, bali fuateni njia ya baina yake (hali hizo mbili). Na semeni shukrani zote anastahiki Allah ambae hana mtoto, na wala hana mshirika katika Ufalme wake, na ni asiekua (na uhitaji wa) Msaidizi wala Mlinzi. Na Mkuzeni kwa Takbir***



ALLAHU AKBAR!

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

VITABU VILIVYOTANGULIA VYA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH:

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

1-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA KWANZA - MWAKA - *1435 AL HIJRA* (2014).

2-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA PILI - MWAKA - *1437 AL HIJRA* (2016).

3-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA TATU - MWAKA *1439 AL HIJRA* (2018).

4-TAFSIR SURAT YUSUF – AHSAN AL QASAS - MWAKA *1441 AL HIJRA* (2020).

5-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL AWWAL – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA KWANZA – MWAKA 1442 AL HIJRA (2021).

6-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL THANI – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA PILI – MWAKA 1443 AL HIJRA (2022).

7-TABAQAT WARATHAT AL ANBIYAI - AL JUZUU Al AWWAL - MATABAKA YA WARITHI WA MITUME-JUZUU YA KWANZA - MWAKA 1443 AL HIJRA (2022).

8- TAFSIR YA SURAT AL KAHF MWAKA 1444 AL HIJRA (2023).

YALIYOMO

MASHARTI YA KUA NA SIFA STAHIKI YA KILA MWENYE KUTAKA ILM YA MUJARRABATI.

Bismi Allahi AlRahmani Al Rahim, Alhamd Lilladh Rabbi Al Alamin, wa Salatu wa Salamu AaLA Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, wa aAla alihi wa As-habihi wa Salam wa al Muslimina wa Al Muslimati ajmaAin.

Hiki ni kitabu chenye malengo ya kufunza kuhusiana na Ilm ya Utabibu wa Mujarrabati yaani Majaribio yaliojaribiwa na kutoa Matokeo stahiki katika na Utatuzi wa Matatizo mbali mbali yakuondoa Madhara katika Jamii kwa kutumia njia zilikua zikitumiwa na Wanazuoni maarufu katika Fani ya Ilm hii wakiwemo *Hujjat Ul Islami* Imam Abu Hamid Muhamamd IbnMuhamamd Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii, Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din Ibn Al Arabi, Sultan Al Mutakkalimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi, Imam Abd Al Qadir Al Jaylani, Imam Ahmad Al Bunni na wengineo.

Ambapo tunapoangalia ndani yake njia zao Maimamu hawa wakubwa sana katika fani ya *Mujarrabati* basi tunaona kua walikua ni wenye kutulia mkazo kua malengo ya Ilm hii ya *Mujarrabati* ni Kuondoa Madhara na Kurahisisha kwa kusababisha matokeo mazuri bila kudhuru ambapo miongoni mwa muongozo wao ili kufanikisha na kupata matokeo stahiki juu ya jambo husika basi tunaona kua Wanashauri kua Ili mtu kua ni mwenye sifa nzuri ya Utabibu na hivyo kua ni mwenye mafanikio zaidi katika Utabibu wake basi kuna mambo muhimu ya kuyafuatilia ambayo kila mmoja mwenye kutaka kua na sifa hio anatakiwa awe ni mwenye kushikamana nayo na mambo hayo ni yafuatayo:

1- Kua na Msimamo na Ikhlasi katika kufanya Amali husika na kua na Imani kua Majibu ya Tatizo husika yatapatikana kupitia katika njia husika kwa Idhini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

2- Kua na Msisitizo katika kufanya jambo husika na kutokua na papara, kiasi ya kua kama ikiwa Majibu hayatapatikana katika Amali husika basi inabidi Amali hio irudiwe tena upya.

3- Kua na siri katika ufanyaji wa Amali husika hivyo isiwe ni yenye kufanywa mbele ya watu, bali ifanywe katika sehemu ya faragha.

4-Kua na Usafi wa Moyo, Mwili na Mavazi ya Mfanyaji Amali husika na pia kuwe na Usafi wa mahali inapofanyiwa Amali husika.

5- Kua na Ucha Mungu katika utafutaji riziki ya mfanyaji Amali husika na isiwe kuna hadaa, utapeli, mambo ya haramu yasiyofaa au kusababisha Madhara ndani yake.

6- Kutokua ni mwenye hali ya kua ni mwenye kushiba sana katika wakati wa kufanya amali husika, kwani shibe husababisha Uvivu na kumkaribisha Shaytan katika ufahamu na mawazo ya mtu husika.

7-Kutopenda kutumia chakula kinachotokana na Wanyama kama Nyama na Maziwa au Mayai kwani nako pia hupelekea Mtu kua na Uvivu na kutaka kula zaidi vyakula hivyo kutokana na maumbile yake.

8-Kutopenda kula Vyakula vyenye kutoa harufu mbaya mdomoni kabla ya kufanya Amali husika au katika wakati wa kufanya Amali husika kama Vitunguu Maji, Vitunguu Thaumu, Figili n.k.

9-Kua ni mwenye kupenda kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kila Amali kabla ya kufanywa kwake, katika kufanywa kwake na baada ya kufanywa kwake, kwani Amesema *Umar Ibn Al Khattab Radhi Allahu Anhu* kua: 'Maombi yote hua ni yenye kuningi'inia baina ya Mbingu na Ardhi hadi pale atakaposaliwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.'(*Imam At Tirmidhii*)

10 – Kua na Utulivu katika wakati wa Ufanyaji Amali husika yaani akili na ufahamu usiwe ni wenye kufikiria mambo mengine ya kifamilia, kimaisha, kiuchumi n.k bali uwe ni wenye kufikiria juu ya jambo husika tu, na hivyo kutotakiwa kua ni mwenye kusikiliza mambo mengine.

11- Kuelekea katika Upande wa Kibla katika ufanywaji wa Amali husika, isipokua katika baadhi ya Amali ambazo hua ni zenye masharti ya kukutaka kuelekea katika upande fulani kwa mfano kukielekea kitu husika au kukipa mgongo katika kuomba kwako.

12- Kua na ufahamu wa Nyakati za siku na saa katika Ufanyaji wa baadhi ya Amali ambazo hua zinahitaji mda husika na saa husika ambazo hua ni zenye kusimamiwa na wawakilishi maalum wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambazo kupitia kwao basi hua ni wenye kusaidia kuzipa nguvu zaidi Amali husika kimafanikio kulingana na jambo husika.

13-Kua na Ufahamu wa aina ya Bukhuri (Vifukizo) Udi, Ubani n.k katika kuongeza nguvu ya Ufanikishaji wa Amali husika yaani ambazo hutofautiana kulingana na Amali husika, Mda na Siku husika.

14- Kutumia *Qawlan Sadida* yaani maneno machache, yaliyowazi na yaliyonyooka katika Uombaji wa Maombi ya Amali husika.

15-Kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kua na unyenyekevu katika Ufanyaji amali husika na kukubaliana na matokeo yake juu ya Amali husika.

KINGA YA ANAETAKA KUANZA KUFANYA AMALI ZA MUJARRABATI.

Kwa kila mtu ambae ni mwenye kutaka kufanya Mujarrabati basi wajibu kwake kuanza na ngao au kinga ambayo itamsaidia kutokana na madhara ya viumbe wasioonekana na athari za nguvu zisizoonekana kwa kufanya yafuatayo:

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

حصنت نفسي بالحصن الذي اساسه لا اله الا الله وبابه محمد رسول الله

وحيطانه سلام قول من رب رحيم ودائرته له معقبات من بين يديه ومن خلفه

يحفظونه من امر الله همتا لمتا انا الاسد همي شرد سهمي نفذ بفظل بسم الله الرحمان الرحيم

﴿ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ لَا تَأْخُذُهُۥ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ لَّهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ مَن ذَا ٱلَّذِى يَشْفَعُ عِندَهُۥٓ إِلَّا بِإِذْنِهِۦ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَىْءٍ مِّنْ عِلْمِهِۦٓ إِلَّا بِمَا شَآءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلْأَرْضَ وَلَا يَـُٔودُهُۥ حِفْظُهُمَا وَهُوَ ٱلْعَلِىُّ ٱلْعَظِيمُ﴾

﴿قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ❁ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ❁ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ❁ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ﴾

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلْفَلَقِ ❁ مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ❁ وَمِن شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ❁ وَمِن شَرِّ ٱلنَّفَّاثَاتِ فِى ٱلْعُقَدِ ❁ وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ﴾

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ❁ مَلِكِ ٱلنَّاسِ ❁ إِلَٰهِ ٱلنَّاسِ ❁ مِن شَرِّ ٱلْوَسْوَاسِ ٱلْخَنَّاسِ ❁ ٱلَّذِى يُوَسْوِسُ فِى صُدُورِ ٱلنَّاسِ ❁ مِنَ ٱلْجِنَّةِ وَٱلنَّاسِ﴾

حصنت نفسي بالحي القيوم الذي لا يموت ابدا ودفعت عني السوء والاذى بالف الف

لا حول ولا قوة الا بالله العلي العظيم وصلى الله على سيدنا محمد وعلى آله وصحبه وس

Hivyo baada ya kuzitafuta sifa hizo tulizozitaja hapo juu basi basi tunaingia katika hatua ya pili ambayo ni yenye kutufafanulia kua ili kufahamu kwa kina maarifa ya Ilm hii ya Mujarrabati basi kuna mambo ambayo inabidi kuyajua kabla ya kuendelea kuzama zaidi, na hivyo kwa kuanzia basi na tuanze na Sifa kuu za Siku za wiki kama zilivyofafanuliwa na Shaykh Al Akbar Imam Ibn Arabi.

SIFA KUU ZA SIKU ZA WIKI KATIKA ILM AL MUJARABBATI.

Anasema Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din Ibn Al Arabi kua: '**Kila siku ya wiki hua ni yenye kua na Mtume wake miongoni mwa Mitume wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae hua ni mwenye kuwasilisha Siri fulani ndani ya Kifua cha Muumini mwenye kumthibitisha kwa ushahidi, siri ambayo hua ni yenye kufurahiwa na mtu katika siku yake husika ambayo humpelekea mtu huyo husika kua ni wenye kujua juu ya kitu anachohitaji kujua, ambapo tukio hili hua ni lenye kutokea kwa wale wenye Nyoyo zenye Nuru ndani yake.**

Ambapo kama mtu utakua ni miongoni mwa watu wanaotaka kuwasiliana nae katika siku hio na hivyo siku yako ya kuwasilishiwa siri yako kua ni katika Siku ya Jumapili ambayo ni siku ya kwanza. Basi usijishughulishe na yeyote ndani ya siku hio kwani siku hio hua ni siku ya Nabii Idrisa *Alayhi Salam*, ambayo ndani yake hua ni mwenye kukufunulia Siri yenye kukudhihirishia ubainisho wa mambo kabla ya kutokea kwake na ukubwa wa athari yake. Hivyo:

Siku ya Jumapili:
Sifa yake Tukufu ni *Al Samiu*
Ni *Yawm Al Ahad.*
Mtume wake ni Nabii Idrisa Alayhi Salam,
Sayari yake ni Shams (Jua).

Sifa ya Kimaumbile ni *Nur*.
Nafasi yake katika Sala ni Imam.
Nyota zake ni *Simak.*
Mbingu yake ni ya Nne
Ardhi yake ni ya Nne.
Herufi yake ni *Nun*.

Tafakkar! Kwani kila Siku ya Wiki hua ni yenye Kutawaliwa na Jina Maalum Tukufu, na Jua na Mfumo wa Mzunguko wa Sayari zake limeumbwa katika siku ya Jumapili, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amelijaalia Jua kua ndio Mhimili mkuu wa Roho za Ibn Adam.

Ambapo Nabii Idrisa ndio Mhimili wa katikati wa Nyoyo na hivyo Nabii Idrisa amewekwa katikati hii ni kwa sababu kimaumbile basi Jua ndio Kitovu cha Uhai Ulimwenguni na Mbingu yake ni ya nne kwa sababu Mbingu ya nne ndio Mbingu ya katikati baina ya Mbingu saba, na Mbingu ya nne imeumbwa kwa ajili ya kulidhihirisha Jina Tukufu la *Al Nur* na ndio sehemu ambayo ya juu kidarja kama ilivyosema Qur'an kua:

﴿وَرَفَعْنَاهُ مَكَاناً عَلِيّاً﴾

WarafaAAnahu makanan AAaliyyan *(Surat Maryam 19:57)*

*Tafisr**: Na tukamnyanyua katika sehemu iliyokua Juu kidarja.***

Hivyo imeitwa *Makanan Aaliyyan* kwa sababu ndio Moyo mbali ya kua Mbingu zilizojuu yake zi za juu zaidi, lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemaanisha kua ni Sehemu ya Juu Kidarja na ameiumba katika Simak ambayo si sehemu ya kituo cha 14 cha mzunguko wa vituo 28 vya Mwezi na kisha kuiumbia Sayari yake ambayo ni Jua na mfumo wake na akaiumbia herufi yake ambayo ni Nun.

Ambapo kimaumbile hua kuna Viumbe saba tofauti ambao ni wasimamizi wa maeneo ya Mbingu saba tofauti na hivyo kila mmoja hua na siku yake ambapo Msimamizi wa Ilm ya siku ya kwanza ni Nabii Idrisa *Alayhi Salam* na kila kitu kinachouathiri Ulimwengu kwa siku hio hua ni chenye maumbile ya Hewa na Moto vyenye kutokana na Jua na Usimamizi wake kama ilivyokabidhiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Ambapo kuhusiana na athari ya maumbile ya Udongo na Maji ndaniya siku hii basi hua ni kulingana na mzunguko wa Jua katika Mbingu ya nne

Na katika sehemu hio amewekwa Nabii Idrisa kwa sababu ya kua ni kulingana na Safari ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam ya Isra na Miraj* ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* alikutana na Nabii Adam ambae ni mwenye sifa ya Qamar , Nabii Isa ambae ni mwenye sifa ya Attarid, Nabii Idrisa ambae ni mwenye sifa ya Shams, Nabii Harun ambae ni mwenye sifa ya Mirikh Nabii Musa ambae ni mwenye sifa ya Mushtara na Nabii Ibrahim ambae ni mwenye sifa ya Zohal.

Hivyo Kama siku yako ni ya Jumatatu basi mshirika wako hua ni Nabii Adam *Alayhi Salam* ambae ndie mwenye kuwasiliana nawe kwa siri yenye kudhihirisha sababu ya kuongeza na kupungua kwa ustawi wa kitu.

Siku ya Jumatatu:
Sifa yake Tukufu ni *Al Hayy.*
Ni *Yawm Al Ithnayn.*
Mtume wake ni Nabii Adam Alayhi Salam,

Sayari yake ni Qamar (Mwezi).
Sifa ya Kimaumbile ni *Mubin.*
Nafasi yake katika Sala ni Mamuma.
Nyota zake ni *Iklil.*
Mbingu yake ni ya Kwanza
Ardhi yake ni ya Saba.
Herufi yake ni *Dal.*

Tafakkar! Kwani maumbile ya Mzunguko wa Siku ya Jumatatu yameumbwa kwa sifa Tukufu ya *Al Hayy* ambayo kutokana nayo basi ndio imekua kuna uhai Ulimwenguni, hivyo kila kitu hua kinaanza kua hai katika siku ya Jumatatu, Kwani Mwezi ndio wenye mfumo wa Sayari ya Mwanzo kabisa kutoka Duniani kuelekea juu Mbinguni ambapo Jina lake Tukufu hua ni Al Mubin yaani Mwenye Kudhihirisha ambalo ndio kusudio la Kuumba Mbingu, Sayari zake ikiwemo na Mwezi na Kitu chake ni cha Iklil yaani Kofia ya Kifalme ambayo ni Kituo cha 17 kati ya Vituo 28 vya Mwezi na herufi yake ni Dal ambayo ndio yenye mzunguko wa Mwezi.

Mwezi ndio Sayari pekee yenye mzunguko wa kasi miongoni mwa Sayari zinazozunguka kwenye Mfumo wa Jua ambapo mzunguko wake hua uanachukua siku 27 za kidunia na kutokana na siku hizi 28 za mzunguko wa Mwezi basi ndio ndani yake mmepatikana herufi 28 za Alfabeti zinazotumika katika Lugha tofauti za Ulimwenguni. Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemuumba Nabii Adam *Alayhi Salam* na kumuweka katika Mbingu ya Kwanza kwa sababu Nabii Adam *Alayhi Salam* ni mwenye kudhihirisha Ukamilifu wa kiumbe Ibn Adam.

Hivyo Kama siku yako ni ya Jumanne basi mshirika wako hua ni Nabii Harun *Alayhi Salam* ambae ndie mwenye kuwasiliana nawe kwa siri yenye kudhihirisha ni kipi chenye manufaa nawe na ni kipi chenye madhara nawe kutokana na athari za Ulimwengu wa Al Ghayb.

Siku ya Jumanne:
Sifa yake Tukufu ni *Al Basiru.*
Ni *Yawm Al Thulathaa.*
Mtume wake ni Nabii Harun *Alayhi Salam,*
Sayari yake ni Mirikh.
Sifa ya Kimaumbile ni *Al Qahir*
Nafasi yake katika Sala ni Al Isha.
Nyota zake ni *Awwa.*
Mbingu yake ni ya Tano
Ardhi yake ni ya Tatu.
Herufi yake ni *Lam.*

Tafakkar! Kwani Maumbile ya mzunguko wa Siku ya Jumanne umeumbwa kutokana na sifa ya *Al Basiru* yaani Mwenye uwezo wa kuona Juu ya Kila Kitu. Hivyo hakuna sehemu hata moja ya Ulimwengu isipokua sehemu hio ni yenye kuonekana na kushuhudiwa na Muumba wake ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae hata hivyo yenye hua si wenye kuonekana bali hua ni mwenye kuonekana kwa kupitia katika udhihirisho wa Sifa zake Tukufu.

Ambapo Jina tukufu la sifa ya Al Qahir yaani mwenye uwezo wa Kudhibiti na kuzidi nguvu kila kitu ni lenye kudhihirisha Mbingu ya Tatu ambayo ndio sehemu ya Tano kutoka Ardhini na hua ndio inayotofautisha uhalisi wa maumbile ya Kiroho kutokea Pamoja na Sayari yake ya Mirikh ambayo mzunguko wake ndani yake ndio anaishi Nabii Harun *Alayhi Salam.* Na katika mzunguko wa vituo vya

Mwezi basi ipo katika kituo cha 13 kati ya vituo 28 vya Mwezi katika siku ya Jumanne na Mzunguko wake hua uko katika herufi ya Lam.

Na Kama siku yako ni ya Jumatano basi mshirika wako hua ni Nabii Isa Ibn Maryam *Alayhi Salam* ambae ndie mwenye kuwasiliana nawe kwa siri yenye kudhihirisha ukamilifu wa mizunguko ya vituo na Wasimamizi wake.

Siku ya Jumatano:
Sifa yake Tukufu ni *Al Irada.*
Ni *Yawm Al Arbaa.*
Mtume wake ni Nabii Isa Ibn Maryam *Alayhi Salam,*
Sayari yake ni Attarid.
Sifa ya Kimaumbile ni *Al Muhsi*
Nafasi yake katika Sala ni Al Asr.
Nyota zake ni *Zabbana*
Mbingu yake ni ya Pili
Ardhi yake ni ya Sita.
Herufi yake ni *Ta.*

Tafakkar! Kwani Maumbile ya mzunguko wa Siku ya Jumatano hua ni wenye kutokana na sifa tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni *Al Arada*, na hivyo kumaanisha kua hakuna hata sehemu moja ya Ulimwengu ambayo haimtukuzi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie alieiumba.

Attarid ipo kwenye Mzunguko wa sita kutoka Ardhini na imeumbwa kutokana na kujidhihirisha kwa Jina *Tukufu la Al Muhsi* yaani mwenye kusimamia Hisabu, ambapo *Allah Subhana wa Ta'ala* ameiumba Sayari ya Attarid katika siku ya nne yaani siku ya Jumatano na herufi yake ni Ta ambayo sayari yake ni Zabana na iko kwenye kituo cha 16 mzunguko wa mwezi kati ya vituo 28 vya Mzunguko wa Mwezi na kisha akamjaalia Nabii Isa Ibn Maryam Alayhi Salm kua ni mwenye kukaa ndani yake Mbingu hio.

Siku ya Jumatano ni siku ya nne na ndio siku ya katikati ya Wiki kama vile ambavyo Jua lilivyokua ndio katikati ya Mbingu ya nne, na hivyo Jumatano ni Siku ya Nuru na kama ilivyokua kwa darja ya Nabii Isa basi ndivyo ilivyokUa siku ya Jumatano yaani ni siku inayowakilisha katikati ya wiki na ndio siku inayowakilisha muhuri wa Ulimwengu wa Ilm.

Na Kama siku yako ni ya Alkhamis basi mshirika wako hua ni Nabii Musa *Alayhi Salam* ambae ndie mwenye kuwasiliana nawe kwa siri yenye kukufunulia kila kitu kwa kupitia njia ya Malaika mwenye kufurahia yale anayokufunulia. Na Nabii Musa ndie anaekufungulia Ilm ya Imani ya Dini na Mawasialiano ya Vitu visivyozungumza.

Siku ya Alkhamis:
Sifa yake Tukufu ni *Al Qadr*
Ni *Yawm Al Khamis*
Mtume wake ni Nabii Musa Alayhi Salam,
Sayari yake ni Mushtara.
Sifa ya Kimaumbile ni *Al Alim*
Nafasi yake katika Sala ni *Al Dhuhr.*
Nyota zake ni *Mushtara*
Mbingu yake ni ya Sita
Ardhi yake ni ya Pili
Herufi yake ni *Dhad.*

Tafakkar! Kwani Maumbile ya mzunguko wa Siku ya Alkhamis basi ni siku ambayo imeumbwa kupitia katika Sifa Tukufu ya Al Qudra yaani ya Uwezo na hivyokudhihirisha kua hakuna sehemu ya Ulimwengu isipokua ni yenye kua n uwezo wa kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Mushtara ipo kwenye Mbingu ya Sita kutoka kwenye Dunia na Imeumbwa kwa ajili ya kudhihirisha Sifa Tukufu ya Al Alim yaani Mwenye kujua juu ya Kila kitu. Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameumba Mbingu hii na Sayari zake katika siku ya Tano na herufi yake ni Dhad ambayo iko katika kituo cha 12 cha Mizunguko 28 ya Mwezi na kuijaalia kua ni sehemu anayoishi Nabii Musa *Alayhi Salam.*

Na Kama siku yako ni ya Ijumaa basi mshirika wako hua ni Nabii Yusuf *Alayhi Salam* ambae ndie mwenye umilikia wa sifa za kupendwa sana kihisia na hivyo hua ni mwenye kuwasiliana nawe kwa siri yenye kudhihirisha upandaji Darja wa kudumu na kuendela kutokana na Majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Siku ya Ijumaa :
Sifa yake Tukufu ni *Al Alim*
Ni *Yawm Al Arbaa.*
Mtume wake ni Nabii Yusuf Alayhi Salam,
Sayari yake ni Zuhra.
Sifa ya Kimaumbile ni *Al Musawwir*
Nafasi yake katika Sala ni Al Maghrib
Nyota zake ni *Ghafir*
Mbingu yake ni ya Tatu
Ardhi yake ni ya Tano.
Herufi yake ni *Ra.*

Tafakkar! Kwani Maumbile ya mzunguko wa Siku ya Ijumaa hua ni siku maalumu ambayo Nafsi zetu hua zinapokea Siri kutoka kwa Allah Subhanah wa Ta'ala, kwani Mzunguko wa siku ya Ijumaa unatokana na maumbile ya Sifa Tukufu ya Al Alim ambapo hamna sehemu katika Ulimwengu isiyojua kua Imeumbwa na A*llah Subhanah wa Ta'ala.*

Al Zuhra ko katka mzunguko wa Pili wa Mbingu kutoka Ardhini na imeumbwa kutokana na kudhihirishwa kwa sifa Tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ya Al Musawwiru, yaani mwenye kudizaini na kukikamilisha kitu kwa umbo lililobora, ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliumba Mbingu ya Sayari ya Zuhra katika siku ya Mkusanyiko yaani Al Jumaa na kisha akaiweka herufi Ra katika Nyota ya Ghafir katika kituo cha 15 miongoni mwa vituo 28 vya Mwezi na kisha akaifanya ndio makazi ya Nabii Yusuf *Alayhi Salam.*

Na Kama siku yako ni ya Jumamosi basi mshirika wako hua ni Nabii Ibrahim *Alayhi Salam* ambae ndie mwenye kuwasiliana nawe kwa siri yenye kudhihirisha kuhusiana na namna ya kukabiliana na maadui zako na wakati gani hua ni sahih katika kukabiliana nao.

Siku ya Jumamosi:
Sifa yake Tukufu ni *Al Kalam*.
Ni *Yawm Al Sabt.*
Mtume wake ni Nabii Ibrahim *Alayhi Salam*.
Sayari yake ni Zohal.
Sifa ya Kimaumbile ni *Al Rabb.*

Nafasi yake katika Sala ni *Al Maghrib.*
Nyota zake ni *Khirtan.*
Mbingu yake ni ya Saba.
Ardhi yake ni ya Kwanza.
Herufi yake ni *Ya.*

Tafakkar! Kwani Maumbile ya mzunguko wa Siku ya Jumamosi umeumbwa katika Sifa ya Kauli na hivyo kila kitu katika Ulimwengu hua ni chenye kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kumshukuru Muumbaji wake, ila sisi hua si wenye kufaham utukufu wake.

Zohal ipo katika Mbingu ya Saba kutoka Duniani na Mbingu yake imeumbwa kwa ajili ya Kudhihirisha Jina tukufu la Al Rabb yaani Mola ambae ndie alieumba kila kitu na ameiumba Mbingu yake katika siku ya Al Sabt yaani siku ya mapumziko, Nyota yake iko kwenye Nyumba ya Khirtan au Zabran ambayo ni kwenye kituo cha 11 kati ya vituo 28 vya Mwezi na kisha ndani yake yakafanywa kua makazi ya Nabii Ibrahim *Alayhi Salam.*

Naam hio ni kuhusiana na Sifa kuu za Siku kulingana na Mtizamo wa Imam Ibn Al Arabi, na kama tunavyojua kua katika Ilm ya Mujarrabati basi hua kuna baadhi ya Maombi ya Visomo hua ni yenye kuhitaji kurudiwa rudiwa mara kadhaa kwa idadi kulingana na Idadi husika na hitajio lake katika kutekeleza haja au jambo husika. Hivyo tunapoangalia kuhusiana na tunapozungumzia kuhusiana na kurudia kukariri Maneno husika au aya husika au Majina husika basi hua ni jambo lililowazi kua hua inafanywa kwa ajili ya kusisitiza na kutuilia nguvu athari ya utekelezwaji wa jambo husika.

Ambapo hata hivyo mbali ya kua kunahitajika kukariri maneno lakini pia baadhi ya wakati hua tunaona kua kuna uhitaji wa kurudia herufi za Lugha ya Kiarabu, na hivyo kwa baadhi wanaweza wakajiuliza, hivi kwa nini Hizi Herufi peke yake tu hua inabidi kurudiwa, hivi jee hua inamaanisha nini? Au hua zina athari gani. Hivyo ili kujua juu ya haya hilo basi na tuangalie kuhusiana na Sifa za Herufi 28 za Lugha ya Kiarabu.

SIRI ZA KIMAUMBILE ZA HERUFI.

Amesema Imam Abu Qasim Al Qushayr kua: **'Wakati Allah Subhanah wa Ta'ala alipoziumba herufi alizijaalia kua na na Siri tukufu sana herufi hizo, halafu akamuumba Adam na kisha akampa siri hio ya Herufi hizo.'**

Hivyo Kimaumbie Kila herufi inayotumika katika Maneno Majina na kadhalika hua ni yenye kua na nguvu yake kiathari ambayo hua ni yenye kuweza kutuathiri sisi Ibn Adam Kiroho na Kimwili na kiufahamu kulinga na nguvu ya uwezo wa herufi husika hususan katika Majina yetu, maombi yetu na kulingana na mahusiano ya baina yetu na Viumbe wenzetu. Hivyo Wanazuoni wamezifanyia uchunguzi herufu na kugundua mambo mengi sana juu yake kulingana na namna zinavyotuathiri kimaumbile ambapo miongoni mwa athari hizo ni Pamoja na zifuatazo:

Herufi ALIF…(ا)

Herufi Alif katika Lugha Kiarabu hua inawakilisha nambari 1 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Moto.

Ambapo kutokana na muonekano wake basi herufi Alif hua ni yenye kufanana na nambari Moja na kuwakilisha Umoja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na hivyo herufi Alif hua ni yenye uzito wa thamani ya herufi zote za Kiarabu kwa ujumla na hua zinanasibishwa na Nabii Adam kama Baba wa Ibn Adam.

Ambapo tunapoiangalia Ibada ya Sala ya Kiislam basi hua tunaona kua mna hatua kuu tatu ndani yake ambazo ni Kusimama Kama herufi Alif, Kurukuu Kama herufi Dal na Kusujudu kama herufi Mim ambapo hatua tatu hizi ukizichanganya kulingana na mithali zake basi tuaona kua ndani yake tunapata Jina la Adam.

Aanasema Imam Ibn Ataa Allah Al Iskandari kua: **'Herufi Alif inatokana na Ulfa yaani kua na Rafiki wa Karibu ambae ni Mtu mzuri, na hii ni kwa sababu Alif hua ni yenye kuunganisha na kukubaliana na herufi nyengine zote za Lugha ya Kiarabu.'**

Ambapo kwa mtizamo mwengine basi *Herufi Alif* hua inamuwakilisha kiumbe Ibilisi na hii ni kwa sababu Herufi Alif ndio herufi pekee ambayo haijainama tofauti na herufi nyenginezo za Lugha ya Kiarabu.

Matumizi: Mtu atakaeiandika Herufi Alif mara 1111 katika Usiku wa Siku ya Ijumaa na akawa ni mwenye kua nayo basi atakua na athari ya kupendwa na Viongozi na pia na watu mbali mbali kutokana na kua na usafi wa Moyo, mwenye kuondoa shaka na kufanisikisha kila kitu chake na anatakiwa asome dhikr ya (يا سبحان يا اله) katika wakati wa kuandika.

Tatizo: Mtu mwenye Jina linaloanzia na Herufi Alif hua ni mwenye kua na athari ya kupendwa kudhibitiwa na Kiumbe Jini, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kunywa Maji yaliyosomewa Surat Falaq, Surat An Nas kwa mda wa siku 7 mfululizo na awe na Nakshi yenye Sura mbili hizo..na *Biidhni Allah* Atapona

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Alif pia huwemo Maradhi ya Goita, Figo, Tumbo, Ngozi na Upungufu wa Nywele na hivyo awe anapenda sana kutumia Samaki, Vitunguu maji, Mafuta ya Mzaituni, Zaituni na Tini na Zafarani mara moja moja na asipende sana kutumia vyakula kama Ndizi, Machungwa na Embe.

HERUFI BA…(ب)

Herufi Ba katika Lugha Kiarabu hua inawakilisha nambari 2 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Hewa.

Ambapo kama ilivyokua kwa *Alif* kua ni yenye kusimama basi herufi *Ba* ni yenye kulala na hivyo ni yenye kuana uwezo wa kufunganisha na kukubaliana na Herufi nyenginezo zinazoendana nayo kama *Ta, Tha, Nun.* Ambapo Herufi *Ba* ni herufi bora zaidi katika Lugh aya Kiarabu kwa sababu ni Heruf ambayo ni yenye Ufunguzi wa Neno *Bismi Allah Rahmani Al Rahiim* ambalo ndio ufunguzi wa Sura Zote za Qur'an isipokua *Surat At Tawba* na pia ndio ufunguzi wa Kila Jambo.

Ambapo kidoto kilichopo chini yake herufi *Ba* hua kinawakilisha Mwanzo wa kila kitu na hivyo hii hua hua ni hali yenye kumaanisha kua herufi *Ba* imebeba Maneno yote vitabu vilivyoshushwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na ujumbe wa Qur'an nzima imebebwa na *Surat Al Fatiha* na ujumbe mzima wa *Surat Al Faitha* umebebwa na *Bismi Allah Al Rahmani Al Rahiim* na Ujumbe mzima wa *Bismi Allah Al Rahmani Al Rahiim basi umo ndani ya herufu Ba.*

Matumizi: Mtu atakaeiandika Herufi Ba kulingana na uzito wa idadi ya jina lake kwa herufi za Kiarabu katika Usiku wa miongoni mwa masiku meupe, na kisha akwa nayo basi atakua ni mwenye kuepukana na kila shari za maneno ya watu na akawa ni mwenye kua na hata kama alikua ni mwenye kumpenda mtu ambae hata hivyo yeye hapendwi nae basi akifanya hivyo ataona athari ya kupendwa zaidi na mtu huyo, na kama akiwa anaumwa basi akiandika kwenye chombo cha kauri kwa zafarani na kisha akazikosha kwa kwa maji safi huku akisema Ya Rahmani ya Rahim katika kuandika kwake na kukosha kwake na kisha akanywa Maji hayo basi atapona,na pia ataondokewa na kiza cha Moyo na kuana uwezo wa kuhifadhikila kitu. (يا رحمن يا رحيم)

Tatizo: Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ba hua ni mwenye kua na athari ya kupendwa kudhibitiwa na Kiumbe Jini anaeruka, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kufukizwa kwa mda wa siku tatu kwa mafusho ya aina tatu tofuati na hivyo atapona In-shaa Allah.

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Ba pia huwemo Maradhi ya Kichwa, Moyo an kuganda kwa damu na hivyo awe anapenda sana kutumia Samaki, Tungule (Nyanya) Makomamanga, Mafuta ya Mzaituni, na Tini na vyakula vinavyotokana na unga wa Ata na asipende sana kutumia vyakula vyenye mafuta mengi.

HERUFI TA…(ت)

Herufi Ta katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 400 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Hewa.

Herufi *Ta* ina uzito wa thamani kubwa pale tunapozungumzia kuhusiana na Ilm ya Kiroho kwani hii ndio herufi ya kwanza ya neno *Tawhid* ambayo ni fani ya Ilm ya Tawhid yaani Ilm yenye kuhusiana na kumpwekesha *Allah Subhaanh wa Ta'ala katika* hali ya umoja wake. Herufi Ta pia hua inawakilisha hali ya kurudi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika hali ya kuomba msamaha yaani hali ya Toba.

Matumizi: Mtu atakaeiandika Herufi Ta mara 401 katika wakati wa Magharibi ya Siku ya Jumatano na kisha akaikosha kwa Maji Safi na kunywa maji hayo basi atakua ni mwenye Nuru ndani ya Moyo wake na atakua na uwezo mkubwa wa kuhifadhikila kwenye ufahamu wake, na kama akipoteza kitu chake au kuchukuliwa basi aandike herufi hio na kuiweka kwenye Msahafu na kitu hicho kitapatikana, na akiwa nayo basi atakua salama kutokana na Maadui zake ambapo katika wakati wakuandika basi atumie dhikr ifuatayo (يا قيوم يا واجد)

Tatizo: Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ta hua ni mwenye kua na athari ya kuingiwa na khofu ya mshtuko katika Usiku wa siku ya Jumapili na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kunywa Maji yaliyosomewa Surat Falaq, Surat An Nas na Ayatt Al Kursiy kwa mda wa siku 7 mfululizo na awe na Nakshi yenye Sura 3 hizo..na *Biidhni Allah* Atapona.

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Ta pia huwemo Maradhi ya ndani ya mwili kama upungufu wa Damu, na udhaifu wa misuli na mifupa na hivyo awe anapenda sana kutumia Ufuta, Nyama, na mboga mboga na asipende sana kutumia vyakula vyenye Sukari nyingi na Uwanga na machungwa pia.

HERUFI THA…(ث)

Herufi Tha katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 510 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Maji.

Herufi Tha hua ni yenye kuwakilisha Uthubutu na pia huwakilisha hali ya Haki na Uadilifu.

Matumizi: Mtu atakaeiandika Herufi Tha mara 510 katika wakati wa Jioni ya Siku ya Jumanne na kisha akaitundika kwenye ukuta wa Nyumba yake uliokuwepo kwenye upade wa Qibla, basi atakua ni mtu mwenye kufanya mema na kuacha na maovu. (يا دائم يا صمد) na kama ataziandika kwa Zafarani kwenye chombo cha kauri na kisha akakikosha chombo hicho kwa maji safi na kisha akayatumia maji hayo kuwapa wanandoa waliofarikiana wanywe basi watakua ni wenye kupatana na kupenda sana.

Tatizo: Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Tha hua ni mwenye kua na athari ya kupendwa kudhibitiwa na Kiumbe Jini, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kunywa Maji yaliyosomewa Surat Falaq, Surat An Nas kwa mda wa siku 7 mfululizo na awe na Nakshi yenye Sura mbili hizo..na *Biidhni Allah* Atapona

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Tha pia huwemo Maradhi ya ndani ya mwili kama Mishipa ya Damu, Moyo na Mbavu na hivyo awe anapenda sana kutumia Mvuke wa Mafuta ya Karafuu na kujichua kwa Mafuta ya Karafuu pia miguuni na mikononi, Vyakula vya nafaka na mboga mboga karoti, matango, mchicha n.k na asipende sana Ndizi, Mananasi wala Jibini.

HERUFI JIM…(ج)

Herufi Jim katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 3 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Maji.

Herufi Jim hua inawakilisha Subra na Ustahmilivu ambayo ni sifa ya Wenye Taqwa.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Jim mara 53 katika wakati wa Asubuhi na akawa ni mwenye kua nayo basi atakua na ulinzi wa kutoathriwa na uchafu wa maneno ya watu wovu dhidhi yake na atakua ni mwenye kuweza kuona yasiyoonekana na watu na atakua ni mwenye kuneemeka katika Maisha yake. Ambapo anatakiwa awe ni mwenye kutumia dhikr ifutayo katika kuandika kwake* (يا بارئ يا كبير)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Jim hua ni mwenye kua na athari ya kuingiwa na khofu katika siku ya Jumanne wakati akiwa Makaburini, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Ayat ul Kursiyu,Surat Falaq, Surat An Nas..na Biidhni Allah Atapona*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Jim pia huwemo Maradhi ya Mafua, Kikohozi, Kichwa, Koo, Miguu na Kiuno na hivyo awe anapenda sana kutumia Maini, Wali,Vitunguu Thomu, Ufuta, Ndizi, Makomamanga, Zaituni na Tini na asipende sana kutumia Nyama nyeupe kama Kuku, Samaki, Vitunguu Maji

HERUFI HA…(ح)

Herufi Ha katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 8 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Udongo.

Herufi Ha hua inawakilisha hisia za Kimumbile za Ibn Adam, Muanzilisho au Uasisi wa Kitu unaotokana na Uwezo wa Ibn Adam aliojaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Herufi Ha ndio iliyotoa neno *Hubb* yaani hisia za Mapenzi na hivyo pia hua inamaanisha hali ya Muonekano wa kuwepo kwa kitu.

Matumizi: Mtu atakaeiandika Herufi Ha mara 18 katika Usiku wa Siku ya Alkhamis wakati wa Mwezi mpevu na akawa ni mwenye kudumu nayo basi atakua si mwenye kuathirika na madhara ua Uchawi na kama akiiandika kwa Misk na Zafarani na kisha akaifunga kwa Kitambaa cha Hariri Na kisha akachukua Kipande cha Sega na kuweka ndani yake kisha akaweka ndani baina ya Mdomo wake na Meno yake kwa nje basi atakua ni mwenye kuona Viumbe wasioonekana na anatakiwa adumu na dhikr ya (يا بارئ يا زكي)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ha hua ni mwenye kua na athari ya kushtuka kutokana na viumbe wanaotisha anaowaona wanaofanana na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Ayat ul Kursiyu,Surat Falaq, Surat An Nas..na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Ha pia huwemo Maradhi ya Msukumo wa Damu na Mapigo ya Moyo, Kifua, Kichwa na hivyo awe anapenda sana kutumia Nazi, Samaki, Kuku, Maziwa, Mayai, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Kahawa, Nyama Nyekundu, na Karanga.

HERUFI KHA…(خ)

Herufi Kha katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 600 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Udongo.

Herufi Kha hua inawakilisha hali ya *Khayr Daaima* yaani Kheri ya Milele na hivyo hua inamaanisha Hali ya kuhisi mwangaza wa Nuru ambayo ni sehemu ya Roho.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Kha mara 610 katika Usiku wa Siku za mwishoni za mwezi wa Kiarabu Na kisha ikawekwa ndani ya Nyuma yake basi hua ni mwenye kupata kila anachokitaka katka haja yake. Ambapo anatakiwa awe ni mwenye kutumia dhikr ifuatayo katika kuandika kwake* *(يا كافي يا راجي)*

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Kha hua ni mwenye kua na athari ya kupendwa kudhibitiwa na Kiumbe Jini katika siku ya Jumatano, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kunywa Maji yaliyosomewa Surat Falaq, Surat An Nas kwa mda wa siku 7 mfululizo na awe na Nakshi yenye Sura mbili hizo..na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Kha pia huwemo Maradhi ya Msukumo wa Damu na Mapigo ya Moyo, Kifua, Kichwa na hivyo awe anapenda sana kutumia Nazi, Samaki, Kuku, Maziwa, Mayai, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Kahawa, Nyama Nyekundu, na Vyakula vyenye mafuta mengi.

HERUFI DAL…(د)

Herufi Dal katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 4 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Udongo.

Herufi Dal hua inawakilisha muendelezo wa kila kitu kilichoumbwa na hii ni kwa sababu herufi Dal ndio mwanzo wa maneno yasemayo *Daaba Fi Aww aAlaa yaani* kujitolea kwa kufanya kitu kwa ajili ya wengine, kuendelea kufanya kitu kwa mda mrefu bila ya kusita na hivyo kumaanisha Maumbile ya Ibn Adam katika uhai wake hapa Duniani katika kujitahidi kujitafutia Maisha kuendelea kuishi kwa ajili ya Maisha ya kidunia na kiakhera. Na hivyo pia kumaanisha Usafi wa Kiroho.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Dal mara 35 katika Usiku wa Siku ya Jumatano kw akutumia Misk na Zafarani na akawa ni mwenye kua nayo mfukoni basi atakua na athari ya kupendwa na Watu na Moyo wake na Mikono yake itakua mikunjufu, na hua ni yenye kusaidia katika kulipa madeni kwa haraka na anatakiwa adumu na dhikr ya (يا حنا يا منان)na katika wakati anapoandika.*

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Dal hua ni mwenye kua na athari ya kufanyiwa Uchawi na hiyvo awe na Nakshi yenye Sura An Nas,Surat Al Falaq na Ayat Al Kursiyyu..na Biidhni Allah Atapona*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Dal pia huwemo Maradhi ya Macho, Mafua na Mabega na hivyo awe anapenda sana kutumia Zabibu, Samaki, Kuku, Maziwa, Mayai, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Ndizi na Maboga.

HERUFI DHAL…(ذ)

Herufi *Dhal* katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 700 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Moto.

Herufi *Dhal* hua inawakilisha Kiini cha Mtizamo au Fikra au Moyo wa Mtizamo wa Kitu. Na pia humaanisha Ilm ya Lugha.

Matumizi: Mtu atakaeiandika Herufi Dhal mara 731 katika Asubuhi ya Siku ya Jumamosi na kisha kaizika katika sehemu inayosaliwa sala ya Ijumaa kwa nia ya kuhifadhika kwa mali yake basi atakua na athari ya kua na usalama wa Mali zake na anatakiwa adumu na dhikr ya (يا ديان يا خالق)

Tatizo: Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Dhal hua ni mwenye kufanyiwa Uchawi, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Dhal pia huwemo Maradhi ya Mifupa, Shingo na Msukumo wa Damu na hivyo awe anapenda sana kutumia Wali, Vitunguu Maji, Ndizi, Mbatata, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Nyama nyekundu wala Maini.

HERUFI RA (ر)

Herufi Ra katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 200 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Udongo.

Herufi Ra hua inawakilisha Risala yaani Ujumbe na pia humaanisha Sura na Uwezo wa Kuiteka nyara Nafsi na Utanuzi wa ndani ya Kifua.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Ra mara 210 katika Usiku wa Siku ya Jumatatu yenye kua na mwezi unaoonekana hadi asubuhi yake atakua na athari ya kufanikiwa kupata kile akitakachona kama akiwa nayo basi atapendwa nakufukia malengo yake ayatakayo na anatakiwa adumu na dhikr ya*
(يا رحمن يا دائم)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ra hua ni mwenye kufanyiwa Uchawi na maadui zake au na Mwanamke, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismi Allahi,Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Ra pia huwemo Maradhi ya Msukumo wa Damu, Kichwa,Mafua,Macho na Uti wa mgongo na hivyo awe anapenda sana kutumia Zabibu, Samaki, Makomamanga, Tende, Matikiti, Ufuta, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Kahawa, Pilipili Nyama nyekundu au Maharage mekundu.

HERUFI ZA (ز)

Herufi Za katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 7 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Maji.

Herufi Za hua inawakilisha Zaybaq yaani Zebaki na hivyo humaanisha uwezo wa kubadilika kimaumbile kutoka katika hali moja kuingia kwenye hali nyengine kirahisi na humaanisha Kufanya Kitu kwa Moyo uliokua Safi bila kinyongo.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Za mara 700 katika Siku ya Jumamosi na akaizika makaburini basi atakua na athari ya kujua matatizo ya watu na wanaosababisha matatatizo hayo na pia atakua na mamlaka na anatakiwa adumu na dhikr ya* (يا مبدع يا علام)*)*

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Za hua ni mwenye kuchanganywa akili na Mwanamke na atakua na wasi wasi na mashaka mengi sana, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Zal pia huwemo Maradhi ya Moyo, Viunguo vya Mifupa,Kichwa, Kifua na hivyo awe anapenda sana kutumia Tangawizi, Brokoli, Samaki, Kuku, Maziwa, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Nyama Nyekundu na Kahawa.

HERUFI SIN (س)

Herufi Sin katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 60 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Moto.

Herufi Sin hua inawakilisha Nguvu ya Ushindi wa Kitukufu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na pia hua inamaanisha uwezo wa kuwaonea Huruma wale waliokua chini kidarja.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Sin mara 120 katika Siku ya Ijumaa na akawa ni mwenye kua nayo mfukoni basi atakua na athari ya kutopingwa na na kama atakua safarini basi atakua ni mwenye kurudi salama katika safari hio na anatakiwa adumu na dhikr ya* (يا حليم يا معيد)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Sin hua ni mwenye kua na athari kuchanganyikiwa akili na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kujifukiza kwa kutumia manyoya ya Simba na Mtu huyu hutakiwa kua na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona..na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Sin pia huwemo Maradhi ya Figo, Kichwa, Kifua na hivyo awe anapenda sana kutumia Nyama Nyekundu, Mboga mboga Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vitunguu thoum, Mabilingani na Maini..

HERUFI SHIN (ش)

Herufi Shin katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 300 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Moto.

Herufi Sin hua inawakilisha Sharia yaani Njia ya kupitia katika kukifikia Kitu, na hivyo pia humaanisha Majaaliwa ya mwisho wa Kiumbe Ibn Adam.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Shin amara 360 katika Siku ya Jumatano na akawa ni mwenye kukogea maji yake herufi Shin basi atakua na athari ya kufunguiwa milango katika kila sehemu anayoenda na anatakiwa adumu katika hali ya unadhifu na anatakiwa adumu na dhikr ya*
(يا حميد يا عزيز)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Shin hua ni mwenye kudhibitiwa na Jini wa chini ya Ardhi, na hivyo mtu huyo atakua na matatizo ya Moyo pia na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kutibiwa kwa kutumia majani ya Harmala awe na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Shin pia huwemo Maradhi ya Moyo, Mifupa, Kisukari, na hivyo awe anapenda sana kutumia Brokoli, Samaki, Kuku, Maziwa, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Sukari, Wali na Kahawa

HERUFI SAAD (ص)

Herufi Ssaad katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 90 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Maji.

Herufi Ssad hua inawakilisha Usafi wa Moyo na Ukweli, hivyo huwakilisha ukamilifu wa Ufahamu wa Ibn Adam kama ulivyoumbwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Sad mara 95 katika Bakuli la Kauri kwa kutumia Misk na Zafarani Na kisha akampa mtu alieathirika na athari za Uchawi na ajimwagie kichwani mwake basi mtu huyo atapona, au kama kuna mifarakano baina yake na watu basi kutakua na salama na kama akiitia kartasi hio ndani ya Mas-haf basi kama ana uadui basi uadui utaisha na maadui zake wataangamia na anatakiwa adumu na dhikr ya* (يا قاهر يا غريب)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Sad hua ni mwenye kua na athari ya kua na maradhi ya muambukizo wa ndani kwa ndani na hivyo hutakiwa kupewa dawa za kuzia muambukizo.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Sad pia huwemo Maradhi ya Moyo, Mafua, Kichwa, Kisukari, na hivyo awe anapenda sana kutumia Brokoli, Samaki, Kuku, Maziwa, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Nyama nyekundu, Vyakula vyenye Viungo vya Pilau, Ndimu, Limau, Mbirimbi, Embe Mbichi n.k

HERUFI DHAAD (ض)

Herufi Dhaad katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 800 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Hewa.

Herufi Dhaad hua inawakilisha Ufunuo au kuweka wazi na pia humaanisha Uwazi wa Maiti kua wanakua katika hali ya kutosema uongo.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Dhad mara 705 katika Usiku wa Siku ya Jumatano na kisha kaifunga na mjiti wa Mkomamanga na kisha akairembea kwenye Nyumba basi watu wa nyumba hio watakua ni wenye kumpenda sana na pia watapendana miongoni mwao na anatakiwa adumu na dhikr ya*
(يامذل يانور)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Dhad hua ni mwenye athari ya kuzidiwa kuumwa katika siku ya Jumanne, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kutibiwa kwa majani ya Harmala kua na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Dhad pia huwemo Maradhi ya Mafua, Kichwa na Kisukari, na hivyo awe anapenda sana kutumia Brokoli, Samaki, Kuku, Maziwa, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Nyama nyekundu, Vyakula vyenye Viungo vya Pilau, Matunda yenye Ladha ya Ukali.

HERUFI TTAA (ط)

Herufi Ttaa katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 9 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Moto.

Herufi Sin hua inawakilisha Utukufu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Taa mara 19 kwa Miski na Zafarani katika Usiku wa Siku ya Ijumaa na akawa ni mwenye kuiwekwa chini ya Mto wake katika wakati wa kulala basi atakua ni mwenye kumuona Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kwenye usingizi wake, na kama akinywa maji yake basi basi atakua na nuru ndani ya Moyo wake nak ama akiiandika kwenye silaha yake basi hatoshindwa kwenye mapigano yake na kama atadumu nayo basi atapendwa na viongozi anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياعالي ياقدوس)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Taa hua ni mwenye Matatizo ya Moyo na Pumzi, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismillah na Surat Al Inshirah na Biidhni Allah Atapona*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Ttaa pia huwemo Maradhi ya Mkojo, Mifupa, Figo, na Moyo na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Machungwa, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Nafaka.

HERUFI DHAA (ظ)

Herufi Dhaa katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 900 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Maji.

Herufi Dhaa hua inawakilisha Dhahir au Udhihirisho wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na pia humaanisha udhibiti wa Vishawishi na minong'oneza ya Kishaytan.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Dhaa mara 910 katika Siku ya Ijumaa Usiku na akawa ni mwenye kua nayo basi kama alikua na maradhi atapona, na kama alikua na matatizo yatarahisika katika kufanikisha kwake na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياوالي يا متعالي)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Dhaa hua ni mwenye homa inayopanda ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismi Allah, Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat Al Kursiy na Biidhni Allah Atapona*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Dhaa pia huwemo Maradhi ya Mkojo, Mifupa, Figo, na Moyo na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Machungwa, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Nafaka.

HERUFI AYN (ع)

Herufi Ayn katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 70 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Udongo

Herufi Sin hua inawakilisha Akili na Ufahamu, na pia humaanisha Usamehevu.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Ayn mara 130 katika Sikau ya Alkhamis na akawa ni mwenye kua nayo mfukoni basi atakua na athari ya kupendwa watuna atakua ni mtu mwenye Imani sana ya Dini yake na anatakiwa adumu na dhikr ya* (يامحمود ياكريم)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ayn hua ni mwenye kukumbwa na Jini au Uchawi, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Ayn pia huwemo Maradhi ya Kuzidiwa na Uzito wa Mwili au kupukiwa na Uzito wa Mwili na Kichwa na hivyo awe anapenda sana kutumia Matufaa, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Uwanga wala Sukari.

HERUFI GHAYN (غ)

Herufi Ghayn katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 1000 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Udongo

Herufi Ghayn hua inawakilisha Ghayb yaani Mambo ya Siri yasiyoonekana wala kujulikana.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Ghayn mara 1060 katika Siku ya Ijumaana akawa ni mwenye kua nayo basi atakua nimweny ekukinai na hatohitaji ktu chochote kutoka kwa watu kwani atakua na neema kubwa sana na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياعظيم يامجيب)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ghayn hua ni mwenye kufanyiwa Husda, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kula Tende 7 kila siku asubuhi kabla ya kula kitu chochote kua na Nakshi yenye Bismi Allah Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Ghayn pia huwemo Matatizo ya Wivu mkubwa sana na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Machungwa, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Nyama Nyekundu.

HERUFI FAA (ف)

Herufi FAA katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 80 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Moto

Herufi Faa hua inawakilisha Mlango wa Ilm.
Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Faa mara 90 katika Usiku wa Siku ya Jumatano na akawa ni mwenye kudumu nayo basi Allah Subhaanh wa Ta'ala atamjaalia kua nakila nachokihitajia katika Maisha yake, na pia atakua ni mwenyekupendwa kutokana n akua ni mwenye kuwasaidia sana wasiokua na uwezo na wenye matatizo na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياغياثي يامغيث)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Fa hua ni mwenye tatizo la kuona jinamizi na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismi Allahi na Al Kawthari na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Faa pia huwemo Maradhi ya Mifupa, Macho, na Kifua na hivyo awe anapenda sana kutumia Zabibu, Nyama Nyeupe, Karoti, Makomamanga, Machungwa, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Kahawa.

HERUFI QAAF (ق)

Herufi Qaaf katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 90 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Maji.

Herufi Qaaf hua ni jina la Mlima unaosifika sana, na ni herufi ambayo ndio Jina la Sura ya 50 ya Quran n ani moja katiya Herufi ambazo zinajulikana kua kama Herufi Muqataaat ambazo tutazizungumzia hapo baadae.

Herufi Qaaf hua inamaanisha Hali ya Muonekano wa kujiona kutokea ndaniya Nafsi.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Qaf mara 180 na akawa ni mwenye kudumu nayo basi atakua na athari ya kutokua na matatizo yeyote kwani atakua na mali nyingi na kama yuko kifungoni basi atatoka kwani atafunguliwa milango ya kila kheri na pia na watu mbali mbali na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياملك يامهيمن)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Qaf hua ni mwenye matatizo ya akili, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismi Allahi, Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Qaf pia huwemo Maradhi ya Tumboni ikiwemo Kidole Tumbo nk na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Machungwa, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Chumvi nyingi.

HERUFI KAAF (ك)

Herufi Kaaf katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 20 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Maji

Herufi Kaaf hua inawakilisha *Kun* yaani Kua ambalo ni amrisho la *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale anapotaka kitu kiwe basi hukiambia Kua na kinakua kitu hicho tangu mwanzo wake hadi mwisho wake na mahitaji yake yote yanakua Pamoja nacho kitu hicho na hivyo herufi Kaaf hua pia inamaanisha Ilm ya Allah Subhanah wa Ta'la katika kujua na kufanya kwake ayatakayo.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Kaaf mara 101 na akawa ni mwenye kudumu nayo basi atakua na athari ya kufungiwa milango yote ya shari na huzuni na atafunguliwa milango ya kheri na mamlaka na pia na watu mbali mbali na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياكليم ياكريم)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Kaaf hua ni mwenye kudhibitiwa na Jini na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismi Allah, Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat Al Kursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Kaaf pia huwemo Maradhi ya msihipa ya Damu, Msukumo wa Damu na hivyo awe anapenda sana kutumia Nyama Nyeupe Machungwa, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Chumvi nyingi.

HERUFI LAM (ل)

Herufi Lam katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 30 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Udongo.

Herufi Lam hua inawakilisha Ufahamu kamilifu, kwani hii ndio Herufi iliyoanza kuuzugumzia Laytlat Al Qadr yaani Usiku wa Makadirio ambao ni bora kuliko Miezi 1000 na hivyo humkaribisa Mja karibu ya Mola wake, na hivyo herufi Lam inawakilisha pia Ilm kamilifu.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Lam mara 71 katika Siku ya Jumatan usiku na akawa ni mwenye kudumu nayo basiatakuana Ulinzi na hifadhi dhidi ya shari za viumbe mbali mbali na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياشكور ياغفور)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Lam hua ni mwenye matatizo ya Moyo, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismi Allah, Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Lam pia huwemo Maradhi ya Kifua, Mfumo wa Hewa na Mfumo wa Hisia nk na hivyo awe anapenda sana kutumia Matikiti, Makomamanga, Viazi vitamu, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Viungo viungo.

HERUFI MIM (م)

Herufi Mim katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 40 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Moto

Herufi Mim hua inawakilisha Marudio ya kiumbe kuelekea katika sehemu ambayo haina kurudi tena ukiingia umeingia hutoki tena yani kwa Mola wake.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Mim mara 90 katika Alfajir ya Siku ya Ijumaa na akawa ni mwenye kudumu nayo basi atakua na atakua na afya nzuri sana na kuondokewa na maradhi kama akiandika na*

kisha akaiweka kwenye shamba basi shamba hilo halitokua na wadudu waharibifu na anatakiwa adumu na dhikr ya (ياخالق يامحيط)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Mim hua ni mwenye kudhibitiwa na Jini, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye maumivu ya kifuai na mbavuni kwa upande wa kulia na anatakiwa kua na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Mim pia huwemo Maradhi ya Mgongo na Kichwa na hivyo awe anapenda sana kutumia Nayma Nyeupe Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Uwanga.

HERUFI NUN (ن)

Herufi Nun katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 50 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Hewa

Herufi Nun hua inawakilisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan na hivyo kumaanisha sehemu ya Maumbile ambapo nusu yake iko wazi na nusu yake imefichikana.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Nun mara 106 katika Usiku wa Siku ya Jumanne na akawa ni mwenye kudumu nayobasi atakua na ufahamu mkubwa sana na atakua na afya nzuri sana nakuondokewa na maradhi na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياالحبا ياأعلى)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Nun hua ni mwenye maumivu ndani ya mwili mzima, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Bismi Allahi, Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Nun pia huwemo Maradhi ya Kichwa, Alaji, Mafigo na Mfunguko wa Damu na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Nyama Nyeupe, Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, Nyama nyekundu na Vyakula vyenye kemikali.

HERUFI HAA (ه)

Herufi Haa katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 5 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Moto.

Herufi Haa hua inawakilisha Hali ya hisia ya Muonekano wa kuwepo kwa kitu

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Ha mara 15 na akawa ni mwenye kudumu nayo basi atakua na athari ya Habari za Ulimwengu wa Ghayb na anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياوافي ياخفي)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ha hua ni mwenye kua na athari ya kupendwa kudhibitiwa na Kiumbe Jini, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kunywa Maji yaliyosomewa Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat Al Kurisy na awe na Nakshi yenye Sura hizo..na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Haa pia huwemo Maradhi ya Macho, Moyo na Meno na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Machungwa,

Ndimu, Malimau, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, Mabiringanyi au Chumvi nyingi.

HERUFI WAAW (و)

Herufi Waaw katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 6 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Hewa.

Herufi Mim hua inawakilisha Kurudi kwa yule asiekua na Mwanzo wala Mwisho na kutokana na uzito wa nambari yake basi hua inamanisha ukamilifu wa Nambari ambao ni ukamilifu wa Ibn Adam.

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Waw mara 13 katika Siku ya Jumamosi na akaiweka ndaniya Msahafu basi atapata kila alichokua na shida nacho anatakiwa adumu na dhikr ya* (ياحكيم ياشكور)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Waw hua ni mwenye kua na athari ya kupendwa kua na khofu kutokana na mkusanyiko wa Majini, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kunywa Maji yaliyosomewa Surat Falaq, Surat An Nas kwa mda wa siku 7 mfululizo na awe na Nakshi yenye Sura mbili hizo..na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Waw pia huwemo Maradhi ya Kichwa na Kifua na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Machungwa, Ndimu, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Nyama nyekundu

HERUFI YAA (ي)

Herufi Yaa katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 10 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Hewa.

Herufi Yaa hua inawakilisha Msaada wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Matumizi: *Mtu atakaeiandika Herufi Ya mara 20 na kadumu nayo basi atakua ni mwenye kufunguliwa milango yote iliyojifunga hapo kabla kwa ajili na anatakiwa adumu na dhikr ya* (يايقيني يامجيب)

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na Herufi Ya hua ni mwenye kudhibitiwa na Jini Mahaba, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kula Asali Asubuhi kabla ya kula kitu chochote kwa mda wa siku tatu na kua na Nakshi yenye Bismi Allah Surat Falaq, Surat An Nas na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

Miongoni mwa Maradhi ya Watu wenye majina yenye kuanzia na herufi Dhaa pia huwemo Maradhi ya Kichwa, Moyo na Msukumo wa Damu nk na hivyo awe anapenda sana kutumia Karoti, Makomamanga, Ndimu, Mafuta ya Mtini na Mzaituni na asipende sana kutumia Vyakula vyenye Mafuta, Pilipili, wala Chumvi nyingi au Sukari nyingi.

HERUFI LAM ALIF (ء)

Herufi Lam Alif katika Lugha ya Kiarabu hua inawakilisha nambari 10 na hua ni herufi yenye sifa ya kua na maumbile ya Nguvu ya Hewa.

Herufi Lam Alif hua inawakilisha kutokosekana kwa Nia.

Tatizo: *Mtu mwenye Jina linaloanza na HerufiLam Alif hua ni mwenye maumivu ya kifua na kichwa, na hivyo Mtu huyo hua ni mwenye kutakiwa kua na Nakshi yenye Surat Falaq, Surat An Nas, Surat Nur na Ayat AlKursiy na Biidhni Allah Atapona.*

HARFU MUQATAA'AT.

Tunapozungumzia Harfu MuqattaA'at hua basi hua Tunazungumzia herufi za Lugha ya Kiarabu ambazo zinapoandikwa na zinaposomwa hua zinasomwa kwa kutengenishwa, kwa mfano neno *Alif Lam Ra* ambalo ndio lililoanzia na aya ya mwanzo ya *Sura Yusuf* ambayo ni sura ya 12 katika Qur'an, ama tunapozichunguza harfu *MuqattaA'at* zilizozomo ndani ya *Qur'an* basi tunaona kua kwa baadhi pia hua wanaziita kua ni *Huruf al Mutafarriqa* yaani Harfu zilizotenganika.

Baadhi ya wenye kujua wamesema kua *Harfu hizo MuqaattaAt* zinamaanisha*:*

Alif (ا): Inayowakilisha neno *Anā* (أنا, Mimi) au neno (*Allah* ﷲ)
Hā (ه): Inayowakilisha neno *Al-Hādī* (الهادي, Muongozi) Inayowakilisha neno *Huwa* (هوYeye).
Ḥā (ح): Inayowakilisha neno *Al-Ḥamīd* (الحميد, Kushukuriwa).
Ṭā (ط): Inayowakilisha neno (Ewe).
Yā (ي): Inayowakilisha neno (Ewe) au (*Yaqin* يقين)
Kāf (ك): Inayowakilisha neno *Al-Kāfī* (كافي, Anaetosheleza).
Lām (ل): Inayowakilisha neno *Allāh* (ﷲ, Harfu ya pili katika Neno Allah) au (*Latif* التف)
Mīm (م): Inayowakilisha neno *Al-ʿAlīm* (العليم, Harfu ya mwisho ya neno *Alim*) au inayowakilisha neno *Al-Majīd* (المجيد, Mwenye Kushinda).
Nūn (ن): Inayowakilisha neno *Al-Qalam* (Inayowakilisha neno Kalamu au Peni) au (*Nur*نر)
Sīn (س): Inayowakilisha neno *As-Samī'* (السميع, Mwenye Kusikia).
A' in (ع): Inayowakilisha neno *Al-ʿAlīm* (العليم, Mwenye Kujua).
Ṣād (ص): Inayowakilisha neno *As-Ṣādiq* (الصادق, Mkweli).
Qāf (ق): Inayowakilisha neno *Al-Qādir* (القادر, Mwenye Kukadiria).
Rā (ر): Inayowakilisha neno *Al Raa* (Kuonaبصير / يرى / رؤيا / رأى / رائي).

Qurán ina Surah 29 zilizoanzia na Huruf MuqattaA'at ambapo 3 kati yao zina harfu 1, 9 kati yao zina harfu 2, 13 kati yao ina harfu 3, 2 kati yao zina harfu 4 na 2 zina harfu 5, Sura hizo ni:

Nambari	Namba ya Surah	Jina la Sura	*Huruf-a-MuqattaA'at*
1	38	*Surat Saad*	صٓ *Saad*
2	50	*Surat Qaaf*	قٓ *Qaaf*
3	68	*Surat Al Qalam*	نٓ *Nun*
4	40	*Surat Al Ghafir*	حمٓ *Ha Mim*
5	41	*Surat Al Fusilaat*	حمٓ *Ha Mim*
6	43	*Surat Az Zukhruf*	حمٓ *Ha Mim*
7	44	*Surat Ad Dukhan*	حمٓ *Ha Mim*
8	45	*Surat Al Jathiyyah*	حمٓ *Ha Mim*
9	46	*Surat Al Ahqaaf*	حمٓ *Ha Mim*
10	20	*Surat Ta-Ha*	طه *Ta-Ha*
11	27	*Surat An Naml*	طسٓ *Ta Sin*
12	36	*Sura Yasin*	يسٓ *Ya-Sin*
13	10	*Surat Yunus*	الر *Alif Lam Ra*

14	11	*Surat Hud*	الر *Alif Lam Ra*
15	12	*Surat Yusuf*	الر *Alif Lam Ra*
16	14	*Surat Ibrahim*	الر *Alif Lam Ra*
17	15	*Surat Al Hijr*	الر *Alif Lam Ra*
19	29	*Surat Al Anqabut*	الٓمٓ *Alif Lam Mim*
20	30	*Surat Ar Rum*	الٓمٓ *Alif Lam Mim*
21	31	*Surat Luqman*	الٓمٓ *Alif Lam Mim*
22	32	*Surat As Sajda*	الٓمٓ *Alif Lam Mim*
23	2	*Surat Al Baqara*	الم *Alif Lam Mim*
24	3	*Surat Al Imran*	الم *Alif Lam Mim*
18	26	*Surat Ash Shuara*	طسٓمٓ *Taa Sin Mim*
25	28	*Surat Al Qasas*	طسٓمٓ *Taa Sin Mim*
26	7	*Surat Al Araf*	الٓمٓصٓ *Alif Lam Mim Sad*
27	13	*Surat Rad*	الٓمٓر *Alif Lam Mim Ra*
28	19	*Surat Maryam*	كٓهيعٓصٓ *Kaf Ha Ya Aain Saad*
29	42	*Surat Ash Shuraa*	حمٓ عٓسٓقٓ *Ha Mim Aain Sin Kaf*

Tunapoangalia *Harfu MuqattaAat* kulingana na mitizamo ya Wanazuoni wenye *Ilm ya Tasawwuf* katika Fani ya *Ruhaniyya* basi wao wanasema kua *Harfu* hizo ambazo zipo mwanzo mwa sura 19 tulizoziangalia hapo juu kua zimezigawa harfu za lugha ya Kiarabu nusu kwa nusu, kwani hizo zinaitwa *Al Huruf Al Nuranniyah* (Yaani Harfu zenye sifa ya kua na Nuru) ambazo ziko 14.

Na Harfu zilizobakia hua zinaitwa *Al Huruf Al Dhalamiyyah* ambazo nazo zimegawika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni yenye harfu 7 zenye sifa ya darja ya juu na sehemu ya pili ni zenye darja ya chini. Harfu hizi hua zina athari yake kinguvu, ambapo katika *Surat Al Fatiha* tunaona ina harfu zote hizo 7 zenye darja ya chini ambazo hujulikana kama *Sawaqit al Fatihah.*

Harfu hizo ni zenye kunasibishwa na Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Taála* na hivyo kua ni zenye kufanyiwa *Dhikr* kila moja katika siku yake kwa mpango ufuatao:

ف *Fa'- Al Fardan* lenye kumaanisha Mwenye Upekee. Ambalo ni jina la *Dhikr* ya siku ya Jumapili.
ج *Jim – Al Jabbar* lenye kumaanisha Mwenye Nguvu na Ujabari wa kipekee ambalo ni jina la *Dhikr* ya siku ya Jumatatu.
ش *Shin – Al Shahid* lenye kumaanisha Mwenye Kushuhudia kila kitu ambalo ni jina la *Dhik*r ya siku ya Jumanne.
ث *Tha'- Al Thabit* lenye kumaanisha Mwenye Uthabiti wa Kipekee ambalo ni jina la *Dhikr* ya siku ya Jumatano.
ظ *Dha – Al Dhahir* lenye kumaanisha Mwenye Kuonekana dhahir kwa dalili zake ambalo ni jina la *Dhikr* ya siku ya Alkhamis.
خ *Kha' – Al Khabbir* lenye kumaanisha Mwenye Habari juu ya Kila kitu ambalo ni jina la *Dhikr* ya siku ya Ijumaa.
ز *Zay – Al Zakiy* lenye kumaanisha Mwenye Utukufu wa Juu kabisa ambalo ni jina la *Dhikr* ya siku ya Jumamosi.

Ama kwa upande wa Dhu Nun Al Misri basi yeye anasema kua: '**Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ni mharakisho wa dua ambayo ikiombwa kupitia katika Majina hayo basi Dua hio hua ni yenye Kujibiwa Haraka. Na ndani yake mna Harfu 7 na katika *Ummu ul Kitaab* yaani *Surah Al Fatiha* ambayo ni Sura yenye Aya 7 basi harfu zote za Kiarabu zimo katika aya isipokua ث*Tha' (500),* ج *Jim (3),* خ *Kha' (600),* ز*Zal (7),*ش *Shin (300),* ظ*Dha' (900),*ف*Fa' (80)* '**

Ama katika vitabu vingi sana vya *Ilm Ruhaniyat* basi Wataalamu wa fani ya *Ilm* hio akiwemo *Hujjat ul Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali, *Shaykh Al Akbar*

Muhyi Ad Din Imam Abu Bakr Ibn Arabi Al Maliki Al Qurtubi, Imam Abu Hasan Ali Al Shadhili, Imam Shihab Al Din Ahmad Ibn Ali Ibn Yusuf Al Buni Al Maliki Al Ifriqi, Imam Muhammad Ibn Ali Al Sanusi Al Muhajiri Al Hasan Al Idris, Imam Mohammed Ibn Mohammed Ibn Mohammed Abu Abdallah Ibn Al Hajj Al Abdari Al Maliki Al Fassi n.k basi mara kadhaa wamekua wakitumia harfu hizo *katika Dua na baadhi ya Nyiradi zao mbali mbali kwa kuanzia na neno* ***Wa Bi Haqqi - yaani kwa Haki ya*** - kisha humalizia na harfu husika kwa mfano ***ثTha' (500), ج Jim (3), خ Kha' (600), ز Zal (7),ش Shin (300), ظDha' (900),فFa' (80) .***

Kwa upande wa *Shaykh Al Akbar Muhyi* Ad Din Imam Abu Bakr Ibn Arabi Al Maliki Al Qurtubi basi yeye anasema kua**: 'Inabidi Mjue kua *Harfu MuqataA'at* zote, zilizoanza mwanzoni mwa Sura za *Qur'an* ni majina ya Malaika na nimezitaja katika baadhi ya matukio, ambapo kamwe haijawahi kutokea kwangu kuzitumia bila ya kutokea Malaika ambae alinielezea mie juu ya Jambo nisilolijua. Kwa kifupi hawa ni Walimu wangu. Hivyo nikiita moja kati ya *Harfu* hizo basi hua ni sawa na kumuita mmoja kati ya Malaika ambae nae hutokea na kunisaidia kama ninavyohitaji'**

Ambapo:

Harfu	Siku yake	Malaika wake	Jina Maalum
ف (80) Fe	Jumapili	*Rawfa'il*	فرد *Fardan*
ش (300) Shin	Jumatatu	*Jibril*	شاكر *Shakur*
ز (7) Zal	Jumanne	*Samsama'il*	زكي *Zakiy*
ظ (900) Dhal	Jumatano	*Mika'il*	ظاهر *Dhahir*
ث (500) Tha	Alkhamis	*Sirfaya'il*	ثابت *Thabit*
ج (3) Jim	Ijumaa	*'Anya'il*	جبار *Jabbar*
ف (80) Fa	Jumamosi	*'Azra'il*	فاطر *Fatir*

Shaykh Al Akbar Muhyi Ad Din Imam Abu Bakr Ibn Arabi Al Maliki Al Qurtubi anaendelea kutuambia katika *Al-Durr al-Maknūn fī 'Ilm al-Ḥurūf*, kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* alimfundisha Nabii wake Adam Jina tukufu kuliko yote. Kisha baada ya hapo Nabii Adam akamfundisha mtoto wake Seth ambae nae akamfundisha Nabii Idrisa *Alayhi Salaam*. Nabii Idrisa *Alayhi Salaam* alikua ni mwenye kupokea vitabu 30 kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na akapewa *I'lm* ya harfu, na siri za Hikma, Nambari na mambo mengineyo, na yeye ndie aliyekua ni wa mwanzo kuandika kwa kutumia Kalamu.**

Nabii Idrisa aliandika kitabu kiitwacho *Kanz Al Asrar* (Hazina za Siri), ambacho Thabit Ibn Qurta Al Harani ameandika kukielezea juu yake. Na mimi nilipokutana nae Nabii Idrisa baada ya kupata ufunuo, basi nikamuuliza, ufunuo zaidi juu yake ambapo nae akasema: 'Ufunuo huu ni ule ambao uliohifadhiwa nje ya Kitabu kwani myengine yote iliyobakia imefichika na imefungwa ndani yake. Kisha akanifunulia baadhi ya Siri zisizojulikana ambazo hakuna mtu mwenye kuzijua juu yake. *Ilm* hii ya Harfu baadae ikarithiwa na watu 40 tu wa jamii ya watu wa *Haramisa* wa Misri''

Kwani baadhi wanaweza kujiuliza kwa nini kila nikiandika harfu basi hua ninaandika nambari mbele yake kwa mfano ث *Tha*' (500), ج *Jim* (3), خ *Kha'* (600), ز *Zal* (7), ش *Shin* (300), ظ *Dha*' (900), ف *Fa*' (80) n.k.

Hivyo hua nnandika hivi kwa sababu hii ni kulingana na mtizamo wa *Ilm Ruhaniyyah* ambapo harfu hizi zimepewa thamani ya uzito wa kiidadi kama ifuatavyo.

الف 1 ب 2 ج 3 د 4 هـ 5 و 6 ز 7 ح 8 ط 9 ى 10 ک 20 ل 30 م 40 ن 50 س 60 ع 70 ف 80 ص 90 ق 100 ر 200 ش 300 ت 400 ث 500 خ 600 ف 700 ض 800 ظ 900 غ 1000.

Na wenye *Ilm Ruhaniyyah* hua wanatumia uthibitisho wa kua kila kitu kina idadi yake kinambari kutokana na ile aya ambayo inasema:

﴿لِّيَعْلَمَ أَن قَدْ أَبْلَغُواْ رِسَالاَتِ رَبِّهِمْ وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَداً﴾

LiyaAAlama an qad ablaghoo risalati rabbihim waahata bima ladayhim waahsa kulla shay-in AAadadan *(Surat Al Jinn 72:28)*

Tafsir: ***Na huwalinda (Mitume) hadi ahakikishe kua wamefikisha ujumbe wa Mola wao. Na yeye (Allah) amekizunguka na amekilinda kila kitu katika idadi.***

‘**Ambapo aya imetumia neno *Ahata* lenye kutokana na neno *Ha-Ta* linalomaanisha Kuangalia, Kulinda, Kuzunguka, Kugubika, au Kujua kitu kwa Undani, na pia ikatumia neno *Ahsa* ambalo linalotokana na neno *Ha-Ssa* ambalo hua ni lenye kumaanisha Kupiga Changarawe au Kurusha Kijiwe kimoja kimoja, Kuhesabu kwa Umakini, Kutia Nambari, Kuhesabu Kiidadi, Kujua au Kufahamu Idadi ya Kitu’**.

Ama kwa upande mwengine basi Imam Muhammad Ibn Is-haq amesema kua amesema Imam Hisham Ibn Muhammad Al Kalbi kua amesema Abu Salih, kua amesema Jabir Ibn Abd Allah Ibn Riyab kua: **Abu Yasir Ibn Akhtab, pamoja na baadhi ya Mayahudi walipita mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae nae alikua akisoma *Surat Al Fatiha,* kisha akasoma *Alif Lam Miim, Dhalika Al Kitab La Rayba Fihi Hudda lil Mutaqqin.***

Hivyo (Abu Yasir Ibn Akhtab) akamfuata ndugu yake Huyayy Ibn Akhtab ambae alikua amekaa na Mayahudi wenzake na kuwaambia: ‘*Wallahi*! Nimemsikia Muhammad akisoma kile alichoteremshiwa, *Alif Lam Miim, Dhalika Al Kitab La Rayba Fihi Hudda lil Mutaqqin.*’ Huyayy akamuuliza: ‘Umemsikia akisoma maneno hayo?’

Abu Yasir akajibu; ‘Naam!’

Hivyo Mayahudi hao wakaondoka wote kwa pamoja hadi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuuliza: ‘Jee Jibril amekuteremshia maneno yasemayo *Alif Lam Miim, Dhalika Al Kitab La Rayba Fihi Hudda lil Mutaqqin*?’

***Rasul Allah Salallahu A’layhi wa Salam* akajibu: ‘Naam.’**

Mayahudi wakasema: ‘Allah ameleta Mitume kabla yako, lakini sisi kamwe hatujawahi kusikia miongoni mwao dambae ameataarifiwa juu ya mda wa Mamlaka isipokua wewe. Na mda wa uhai watakaoishi watu wa Ummah wako kwani, *Alif* ni 1, *Lam* ni 30, *Mim* ni 40, na hio jumla yake ni 71. Hivyo hio ni miaka 71, sasa jee tunataka kumfuata Mtume ambae Mamlaka yake mwisho wake ni Miaka 71 na uhai wa Watu wake mwisho wao ni miaka 71?’

Kisha wakamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam:* ‘Ya Muhammad Jee kuna jambo jengine ulilshushiwa zaidi linalofanana na hili?’

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Naam.’**

Mayahudi wakauliza: 'Jee ni lipi?' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: '*Alif Lam Mim Sad.*'

Mayahudi wakasema: 'Hio ni zaidi, kwani Alif ni 1, Lam ni 30, Mim ni 40, Sad ni 90 hivyo hapa inamaanisha miaka 161.'

Mayahudi wakauliza: 'Ya Muhammad jee kuna jengine zaid?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Naam. *Alif Lam Ra.*'**

Mayahudi wakasema: '*Alif* ni 1, *Lam* ni 30 na *Ra* ni 200. Hio hua ni miaka 231'.

Wakauliza tena: 'Ya Muhammad jee kuna jengine zaid?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: '*Alif, Lam, Mim, Ra*'.**

Mayahudi wakasema: '*Alif* ni 1, *Lam* ni 30, *Mim* ni 40 na *Ra* ni 200. Hio ni miaka 271.'

Kisha Mayahudi hao wakaondoka na kusema: 'Ya Muhammad hakika sisi tumechanganyikiwa juu ya mambo yako haya, kwani hatujui juu ya mda wa Mamlaka yaliopewa Ummah wako kama utakua ni mrefu ama la.'

Mayahudi hao wakaambiana: 'Twende zetuni' kisha wakaondoka kwa pamoja huku Huyay akimwambia Abu Yasir pamoja na Rabbi wao kua: 'Na ni nani atakaeweza kujua kwani huenda miaka hio yote 71, 61, 100, 231, na 271 hua ni 734 ni kwa ajili ya Ummah wa Muhammad, na bado kuna mengine ambayo hayakuhesabiwa.'*(Tarikh Imam Bukhari, Durr al Manthur na Al Itiqan Fi Ulumu Ul Qur'an Imam Al Suyuti, Tafsir Imam Ibn Kathir ya Maktabah Qurtubah Al Qahira.)*

Kwa upande wa Suhayl basi yeye anasema: '**Inaonekana kua jumla ya idadi ya harfu *MuqataaAt* zote zilizorudiwa ndio Urefu wa Mamlaka ya Ummah huu.**'

Ama kwa upande wa Imam Abu Al Khayr Shams Al Din Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Yusuf Al Jazari Al Shafii basi yeye anasema katika ushairi wake wa *Al I'lm Hukm Al Qiraat* kua:

والبيت هو أبياتها قاف وزاي في العدد....من يحسن التجويد يظفر بالرشد

وقاف في العدد = 100 و زاي = 7

آي عدد الآبيات 107 بيت والله أعلم

'**Na Nyumba yake ni Nyumba za *Qaf* na *Zay* katika Idadi. Na anaekiboresha kisomo chake cha *Tajwid* kwa kutumia muongozo wa Jaffar.**

Na *Qaf* kiidadi ni 100 na *Zay* 7 hivyo idadi ya nyumba yake ni 107.

Na Allah ni mwenye kujua zaid.*(Mandhumat Al Muqaddimat, Imam Ibn Al Jazari)*

Vile vile tunapoangalia miongoni mwa Wanazuoni katika kuitafsiri *Surat Ar Rum* basi anasema Imam Abu Shamah Shihab Ad Din Abd Rahman Ibn Ismail Ibn Ibrahim Ibn Uthman Ibn Abi Baqr Ibn Ibrahim Ibn Muhammad Al Maqdisi kua: **Alisema Imam Abu Al Hakam Abd Salam Ibn Abd Al Rahman Ibn Mohammad Ibn Barrajan katika kuitafsiri *Surat Ar Rum*:**

﴿الٓمٓ ۞ غُلِبَتِ ٱلرُّومُ﴾

Alif, Laam, Miim, Ghulibati Alrum *(Surat 30:1-2)*

Tafsir: ***Alif Laam Miim; Warumi wameshindwa.***

Kua: '**Jerusalem itakua chini ya Mamlaka ya Utawala wa Roman Empire hadi katika mwaka 583 Al Hijr kwani katika mwaka huo ndio watakaposhindwa na kupinduliwa. Na Jerusalem itakua chini ya Mikono ya Uislam hadi mwisho wa Dunia. Na hii ni kulingana na idadi iliyomo ndani aya hii'.** Na hivyo ndivyo ilivyotokea. *(Tarikh al-Khulafa, Imam Al Suyuti, Al Itiqan Fi Ulumu Ul Qur'an Imam Al Suyuti)*

Tafakkar!

Kwani *Allamah* Ibn Barrajani alichukua idadi ya neno *Ghulibat* yaani *Watashindwa* ambalo kiidadi ni 1432 na kwa kua wenye kushindwa hua ni wenye kula hasara hivyo na hivyo hua ni wenye kupungukiwa na walichokua nacho basi nae akapunguza neno *Al Rum* kutoka katika Idadi kamili ya neno *Ghulibat*, ambapo *Al Rum* kiidadi ni 277, hivyo alipotoa 277 kutoka katika 1432 basi akapata jawabu ya 1155 kisha akajumlisha na nambari ya Sura ambayo ni 3 na kisha akajumlisha na nambari ya aya ambayo ni 2 akapata jawabu ya mwaka 1187 Christian Era.

Na ukweli ni ilikua ni katika mwaka huo wa 1187 ambao Sultan Salah Ad Din Yusuf Ibn Ayub alipoukomboa Mji wa Jeruslaem kutoka mikononi mwa Crusaders.

Ingawa hio ni mitizamo mbali mbali pale tunapozungumzia Harfu *Al MuqattaAat* kupitia katika *Ilm ya Ruhaniyya* lakini pia kuna mtizamo wa pili ambao nao una ufafanuzi tofauti juu yake, ufafanuzi huo unawekwa wazi na mfano ufuatao:

Katika kipindi cha Utawala wa Khalifa Al Mutawakkil ambae alikua ni mtawala wa Mamlaka ya Al Abbas, basi aliandikwa barua na Mtawala wa Rumi ambayo ilikua inseam: '**Hakika mimi nimesikia kua katika kitabu cha Dini yenu mna Sura ambayo ina harfu zote isipokua harfu 7 (*Sawaqit al-Fatiha*: *ث Tha' (500), ج Jim (3), خ Kha' (600), ز Zal (7),ش Shin (300), ظ Dha' (900),ف Fa' (80))* ndani yake. Na kama Surah hii ikisomwa basi basi humpatia Pepo yule aisomae. Hivyo mimi nilikua nataka kujua ni Sura gani hio na kwa nini harfu hizi hazimo ndani yake'**

Suali la barua hii lilimchanganya sana Khalifa Abu Al Faḍhl Jaʿfar Ibn Muḥammad Al *Muʾtaṣim Billāh* maarufu kama Khalifa Al Mutawakkil, hivyo ikambidi kumtafuta Imam Ali An Naqi ambae alikua akiishi katika ardhi ya mjini Samara. Imam Ali An Naqi alipoulizwa juu ya suali hilo basi akajibu: '**Sura hio ni *Surat Al Fatiha,* na harfu hizo hazimo ndani yake kwa sababu kila moja kati ya *Sawaqit* hizo zinawakilisha maneno yenye maana maangamizo katika kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.**'

Khalifa al Mutawakkil akamuuliza Imam Ali An Naqi juu ya harfu 7 za *Sawaqit,* ambapo Imam Ali An Naqi nae akajibu: '**Harfu ya kwanza ni harfu ث *Tha* ambayo inawakilisha maangamizo yaani *Thubur*, harfu ya pili ni ج *Jim* ambayo inawakilisha Moto wa Jahannam yaani *Jahim*. Harfu ya**

tatu ni خ *Kha* ambayo inawakilisha Ubaya yaani *Khubth* au Hasara yaani *Khusr*. Harfu ya nne ni ز*Zal* ambayo inawakilisha *Zaqqum* ambao ni mti wa Motoni ambao Matunda yake ni yenye sumu na machungu yasiyokua na mfano wake. Harfu ya tano ni ش *Shin* ambayo inawakilisha *Shaqawa. Harfu ya sita ni* ظ *Dhal* ambayo inawakilisha *Dhulma* na harfu ya saba *ni* ف *Fe* ambayo inawakilisha *Afat* yaani Mitihani na maangamizo kwa ujumla.'

Kwa upande wa wataalamu wa Lugha wanasema kua kila harfu ya Kiarabu hua ina maana pekee inayojitegemea kwa mfano: Harfu *Alif* inapokua peke yake inatumika kuuliza Suali, harfu *Mim* inawakilisha kuuliza juu ya kitu au Mtu na pia humaanisha wingi katika kiwakilishi, Harfu *Lam* huwakilisha Kukataa, n.k

Hivyo basi kulingana na mtizamo huo hua tunaona kua Neno *Alif Lam Mim* hua linamaanisha hali ya Mahojiano, Kupinga au Kuuliza masuali, yaani kupinga baadhi ya mambo na kuafikiana baina ya mambo yanayopingana. *Sultan Al Mutakallimi Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi anasema pia kua: '**Waarabu walikua wakitumia harfu 'ع' kumaanisha Pesa, harfu 'غ' kumaanisha Mawingu, harfu 'ن' kumaanisha Samaki, n.k**'

Katika kuunga mkono maana hizo basi tuangalie mifano ifuatayo ambapo tunapoangalia moja kati ya mashairi ya Walid Ibn Uqba Ibn Abu Mua'yit basi tunaona kua anasema:

قلت لها قفي فقالت قاف

Qultu Laha Qifiy faqalat Qaf.

Tafsir: '**Nilimwambia yeye (Mwanamke)**: '**Kaa Kidogo'**, **nae akajibu**: '***Qaf***.

Ambapo harfu ya mwisho ambayo ni *Qaf* imetumika kuwakilisha neno: *Waqafa* وقف ambalo maana yake hua ni **Kusimama** Mfano mwengine ni ule wa Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abu Bakr al Ansari Al Qurtubi ambae anatoa mfano kwa kusema kua Waarabu hua wanasema:

كف لنا السيف شا

Kafa Lana al Sayf Shin yaani: **'Unatutosha sisi Upanga kua *Sha*'** ambapo *Harfu Shin* imetumika kumaanisha neno ***Shafii.*** Na wengine hua wanasema kua inamaanisha neno ***Shahidan'***

Kwa upande wa Imam Abu Talib Al Makki basi yeye anasema kua: '**Sayyidna Ali Ibn Abi Talib *Karamah Allahu Wajh* alikua akiomba dua kwa maneno yasemayo: '*Ya Kaf, Ha, Ayn, Sad*, hakika mimi nakuomba kupitia kwako uninusuru na Dhambi zenye kuangamiza, Kuondokewa na Baraka, Kuondokewa na mvua, au Kuzidiwa na Maadui zangu. Ya Allah! Tulinde dhidi ya Nafsi zetu.**'' Ambapo harfu *Kaf* inawakilisha Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* la *Al Kafi*, *Ha* ni *Al Hadi*, *Ya* ni *Al Yaqin*, *A'ayn* ni *Al A'lim* na *Sad* ni *Al Sadiq*.

Ama tunapomuangalia Imam Tahir Ibn Ashur katika kuitafsiri *Surat Yasin* basi amesema kua neno *Ya Sin* ambazo ni Harfu mbili za *Ye na Sin* hua linamaanisha *Ya Sayyid* yaani Ewe Bwana (wa Mitume).

Ambapo Imam Hamid Al Din Abu Hasan Ahmad Ibn Abd Allah Al Kirmani basi yeye anasema kuhusiana na *Surat Ta-Ha* kua: '***Ta-Ha* maana yake ni Mwezi Mweupe kwani *Harfu Ta* ina uzito wa idadi ya 9 na harfu *Ha* ina thamani ina uzito wa idadi ya 5 na ukizijumlisha kwa pamoja unapata 14 kumaanisha mwezi 14 muandamo.'***(Al Gharaib)*

Imam Abu Muhammad Sahl Al Tustari ambae yeye anatuambia kua: '**Kila Kitabu ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* alikishusha basi kina mfumo wa siri ndani yake, na mfumo wa siri wa *Qur'an* umo katika harfu ambazo ndio ufunguzi wa Sura husika, kwa sababu Harfu hizo ndizo ni Majina na Sifa zake. Kama anavyosema *Alif Lam Mim* (2:1, 3:1, 29:1 na 31:1), au *Sad (38:1)* au *Alif Lam Ra (10:01, 11:1)* n.k. basi harfu hizi zinapojumuishwa pamoja, zinatoa jina Tukufu la Allah *Subhanah wa Ta'ala*. Kwa mfano *Alif, Lam, Ra, Ha, Mim na Nun* basi hua tunapata jina la *Al Rahman.* Ambapo kwa Abd Allah *Ibn Abbas(Radhi Allahu Anhu) na Dahhaq* basi wao wamesema kua *Alif Lam Mim* hua inamaanisha: 'Mimi ni Allah Mwenye Kujua.**

Ambapo kwa Upande wa Ali Ibn Abi Talib *Karama Allahi Wajh* basi yeye anasema kua: 'Haya ni Majina ambayo, yapo katika hali ya harfu zilizotawanyika. Lakini kama ikichukuliwa harfu moja kutoka katika kundi kila kwa mpangilio wa kua ni tofauti na harfu iliyokaribu yake harfu hio, na zikakusanywa pamoja kiidadi basi hua ni zenye kuunda jina la mwingi wa Rehma. Hivyo kama ikiwa jina hili litajulikana na kisha likatumiwa katika maombi ya Dua basi litakua ni jina lenye Nguvu sana kiasi ya kua Dua ya muombaji kwa kupita jina hilo itakua ni yenye kukubaliwa.''

Imam Al Tustari anaendelea kutufafanulia kwa kutuambia kua: '**Nimepokea Hadith kutoka kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae anasema kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* ameapa kua kitabu chake hiki, alichomshushia Nabii Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam*, ni kitabu ambacho kipo chini ya uangalizi wake. Hivyo akasema: '*Alif Lam Mim*. Hiki ni Kitabu..ambapo *Alif* hua inamaanisha *Allah*, *Lam* inamaanisha *Jibril* na *Mim* hua inamaanisha Muhammad, hivyo basi hapa inaonesha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala*, amekula kiapo kwa ajili yake yeye mwenyewe, na kwa ajili ya Malaika wake Jibril, na kwa ajili ya Nabii wake *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam*.'''**

Tumalizie kwa kumuangalia Imam Jafar As Sadiq kupitia kwa Sufyan Ath Thawry ambae anasema kua: '**Mimi nilimuuliza Imam Jafar As Sadiq: '*Ya Ibn Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, jee ni nini maana maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kusema kwake *Alif, Lam, Miim na Alif, Lam, Miim, Saad na Alif, Lam, Ra na Alif, Lam, Miim, Ra na Kaf, Ha, Ya, ` Ayn, Saad na Ta, Ha na Ta, Siin na Ta, Siin, Miim na Ya, Siin na Saad na Ha, Miim na Ha, Miim, `Ayn, Siin, Qaaf and Qaaf na Niin''***

Imam Jafar As Saddiq akajibu: '**Ama kuhusiana na Alif-Lam-Mim iliyo mwanzoni mwa *Surat Al Baqara* basi hua inamaanisha *Mimi ni Allah Mfalme na Alif-Lam-Miim* iliyo mwanzoni mwa *Surat Al Imran* basi hua yenye kumaanisha Mimi ni Allah Mtukufu na *Alif-Lam-Miim-Saad* humaanisha Mimi ni Allah Muamuzi wa Kila kitu na Mkweli. *Alif-Lam-Ra* hua inamaanisha Mimi ni Allah Mwenye Wingi wa Usamahevu. Maana ya *Alif-Lam-Miim-Ra* hua inamaanisha Mimi ni Allah Mwenye Kuhuisha, Mwenye Kufisha, Mwenye Kutoa Rizki. Maana *ya Kaf-Ha-Ya-Ayn-Sad* hua ni Mimi Mwenye Kutosheleza, Mwenye Kuongoza, Mwenye Kuhifadhi, Mwenye Ilm, Mwenye katika Ahadi zake.**

Ama kuhusiana na *Ta-Ha* basi hili ni jina miongoni mwa Majina ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Na hua linamaanisha Ewe Mwenye Kuutafuta ukweli na Kuongoza katika njia ya Ukweli. Hatujakuteremshia *Qur'an* ili usifanikiwe katika njia yako, bali tumekuteremshia kwa sababu ya kukurahisishia njia na kukuboreshea Hali yako. Ama juu ya maana ya *Ta-Sin* basi maana yake hua ni Mimi ndie Mwenye Madai ya Kutekelezewa na ndie Mwenye Kusikia Kila Kitu. Ama kuhusiana na *Ta-Sin-Miim* basi hua inamaanisha kua Mimi Ndie mwenye Madai, mwenye Kuona Kila Kitu, ndio wa Mwanzo na Ndie wa Mwisho.

Ama kuhusiana na *Yasin* basi nalo pia ni jina la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hua linamaanisha Ewe Mwenye Kusikiliza Uteremsho wetu na Qur'an iliyojaa Hikma, Kwa Hakika wewe ni Mjumbe Wetu Katika Njia Iliyonyooka. Ama kuhusiana na *Saad* basi ni Chemchem inayotiririka kutoka chini ya *Arshi ya Allah Subhanah wa Ta'ala* na ndio kutokana na maji ya Chemchem hii basi ndio rasul *Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitilia Udhu wake pale alipopelekwa juu Mbinguni katika Usiku wa *Miraj.*

Na ndio Chemchem ambayo Malaika Jibril huenda kujitumbukiza kila siku, kisha hutoka na kujikunuta Maji yote yaliyomo kwenye mbawa zake. Na hakuna hata tone moja linalopukutika kutokana na Maji hayo kutoka kwenye mbawa zake isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kuumba Malaika ambae hua ni mwenye kumtukuza na kumisfu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa mda wote mpaka siku ya Malipo.

Ama kuhusiana na *Ha-Mim* basi hua inamaanisha Mwenye Kustahiki Kusifiwa na Kutukuzwa. na *Ha-Miim-Ayn-Sin-Qaf* basi hua linamaanisha Mstahmilivu, Mwenye Kulipa Malipo Bora kwa Wafanyao Mema, Mwenye Kujua Kila kitu, Mwenye Kusikia Kila Kitu, Mwenye Uwezo wa Kila Kitu na mwenye Nguvu Juu ya Kila kitu. Na *Qaf* hua inamaanisha Mlima ambao ni wenye Kuizunguka na Kuifunika Dunia na kupitia katika Mlima huu ndio *Allah Subhanah wa Ta'ala* akaitandaza Dunia kwa ajili ya Ibn Adam kuishi ndani yake. Ama Kuhusiana na *Nun* basi huu ni Mto wa Peponi ambao *Allah Subhanaha wa Ta'ala* aliuambia ujikusanye na uwe mgumu na akatoa Kalamu na Wino kutokana nao, kisha akaiambia Kalamu hio: 'Andika!' nayo ikaandika kwenye *Al Lawh Al Mahfudh* kila kitu kilichotokea na kitakachotokea hadi siku ya Malipo. Na Kalamu hio ni yenye Nuru ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na *Lawh* ni yenye Nuru *ya Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Sufyan Ath Thawry akamwambia Imam Jafar As Sadiq: **'Ewe *Ibn Rasul Allah!(Salallahu Alayhi wa Salam)* Hebu Nielezee juu kikamilifu juu ya Amri ya *Lawh* na Kalamu na Wino wake na nifundishe kile ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekufundisha.' Imam Jafar As Sadiq akasema: 'Ewe Ath Thawry, kwa hakika kama wewe usingekua mtu anaestahiki kujibiwa basi mimi nisingekujibu. Hivyo fahamu kua *Nun* ni Malaika anaeielekeza Kalamu, na Kalamu ni Malaika anaeielekeza *Al Lawh,* na *Al Lawh* ni Malaika anaemuelekeza Malaika Israfil na Israfil anamuelekeza Mikail na Mikail anamuelekeza Jibril na Jibril anawaelekeza Mitume wote *Sala na Salamu* ziwe Juu yao' Sufyan Ath Thawry anasema kua, kisha Imam Jafar As Sadiq akaniambia: 'Haya nenda zako ewe Ath Thawry kwani hakuna kizingiti juu yako kutokana na Ilm niliyokuachia kwako'’**

Tunaporudi kwa *Sultan Al Mutakallimin Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii, na pia Imam Abu Jafar Muhammad Ibn Jarir at Tabari Al Shafii basi tunaona kua wanasema pia kua: '***Harfu MuqataA'at* zilikua pia ni zenye umuhimu wa kutaka kuwaonesha Makafiri wa Mji wa Makkah utofauti na maajabu ya Qur'an na hivyo iwavutie, kwani wao walikua ni wenye kuapa kua kamwe hawatoisikiliza Qur'an. Hivyo basi Maajabu ya *Harfu* hizi yaliwafanya wawe na hamu ya kutaka kujua zaidi kuhusiana na Qur'an ambayo tayari hapo kabla walikua hawako tayari kuisikiliza**.'

Na ndio maana pia akasema *Sultan Al Balagha* Imam Abu Al Qasim Mahmud Ibn Umar Ibn Ahmad Al Zamakhshari na Imam Nasir Ad Din Al Baydawi kua: **'Malengo ya *Harfu MuqataA'at* ni kuwawekea wazi Makafiri kua Qur'an ina harfu ambazo na wao pia hua ni wenye kuzitumia katika Lugha yao lakini hata hivyo wakawa ni wenye kushindwa kutoa mithili ya Sura moja tu ambayo itafanana na japo moja kati ya Sura 114 za zilizomo ndani ya Qur'an.'**

Hivyo kwa njia moja au nyengine basi hua haishangazi kwanini Wanazuoni wakawa wana mitizamo tofuati juu ya harfu hizi kwa sababu Qur'an tukufu ina aya *Mutashabihat* ambazo hua ni zenye maana

nyingi ndani yake na hi hua ni yenye kuweka wazi Ukubwa usiokua na mwisho wa I'lm ya alieteremsha Qur'an ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Hivyo basi ni jambo la kawaida kwa *Harfu Muqata'Aat* kua ni zenye siri ndani yake na pia kua na maana tofauti kulingana na mitizamo wa Wanazuoni tofauti juu yake.

TALSIM AINA 7 KWA KILA TATIZO

Zifuatazo ni Talsim za kutekelezea aina mbali mabli za haja na matatizo ambapo inayofuatia ni kwa ajili ya Kulinda uhusiano wa Kindoa:

اط١١١٩ط١١١٥٦٩٨٨١ك ح ١١١١١١٣

ســـــــــــــــــــــــ ـــــــــح

Ya pili ni kwa ajili ya kukubalika katika kila kitu:

ا ك ١١١١ان ١ ١ ١ ط ١١١ ل ك ٩ ا ن ٢١١٩ ط ص كا

فــــــــــــــــــــــــ ــــــــــــــــــ

Ya tatu ni kwa ajili ya kutekeleza haja:

٤١١ل اااا غ ححح ١١١ ااا ت ك ٨٨ أ ١١١

كـــــــــــــــــــــ ـــــــــر

Ya nne ni kwa ajili ya kufunika mtu ili asione mtu mwengine yeyote aliebora Zaidi yako:

ط ن ا ن ٨٦ ط م اا ط ع ٩٨ م ن مـ ا ك مـ

لــــــــــــــــــــــ ــــــــلح

Ya Tano kwa ajili ya kutibu maradhi mbali mbali ikiwemo wazimu, Kifafa n.k

ااا اااا٩طط جـ ٢٣٠٠ ٣ ١١١١

كــــــــمــــــــــمـــــــــ د

Ya sita kwa ajili ya Ndoa:

ح ح ح ح ح ح ح وه وه وه وه وه وه

ـــــــــــــــــــــــــ ــــ

Ya Saba kwa ajili ya Safari na Kichumo

ح ج ج ج ج اه آه آه ى آآآآ
ـــــــــــــــ ل ـــــــــــــــ
ح ح ح ح ج ج ج ج مـــــم

ATHARI ZA SAYARI KATIKA MAISHA YA DUNIANI.

Kimaumbile basi Sayari hua ni zenye kuathiri Maisha ya Ulimwengu wa Viumbe Duniani kutokana na Mionzi inayoakisi kwenye eneo husika la ardhi kulingana na wakati husika, kama vile ambavyo ilivyokua Jua la asubuhi kua ni lenye kutuathiri kwa kutuongezea Vitamin D kwa kupitia kwenye Ngozi yetu linapotugusa inavyotuathiri mionzi ya Xray, Ultra sound n.k pale inapokua tunaitumia kwa wmara nyingi zaidi.

Na hivyo Sayari hua ni zenye kuchangia katika kutuathiri sisi Ibn Adam Duniani Kimaumbile na kitabia kulingana na nguvu na athari ya Sayari husika katika wakati tuliozaliwa na kuingia Duniani na pia katika nyakati za Masiku na Masaa tuishio ndani ya Maisha yetu ya kila siku hapa Duniani.

Hivyo tunapoiangalia Sayari ya Qamar hua ni yenye kutuathiri kwa upande wa Mabadiliko ya Hisia za kimahusiano, Uwezo wa kuhifadhi Siri, Mahusiano baina Wanawaume na Wanawake, n.k.

Na hivyo kutokana na kua na maumbile hayo basi ni vizuri kuzitumia ndani ya wakati wake athari hizo kwani hua ni zenye kuongeza athari katika mambo yanayohusiana nayo kwa mfano kwa upande wa Sayari ya Qamar basi hua ni Mujarrab sana kufanya amali zenye kuhusiana na Afya, Kununua Nyumba, Kufunga Safari, Kutafuta vitu vilivyopotea, kupanda mazao shambani, kutafuta Wafanyakazi, Kuomba misaada kutoka kwa Wazee wa kike n.k

Kwa upande wa Sayari ya Mirikh basi hua ni yenye kua na athari za Kutia ari na nguvu ya kufanya Mambo mbali mbali, kua na hisia za mapenzi, kua na hisia za kutaka kuhifadhi, kushindana n.k.

Na ndani ya Wakati wake ni vizuri kufanya amali zenye kuhitaji kua na Nguvu,Ushujaa,Mafanikio ya Kutumia nguvu, Michozo ya kutumia nguvu, Kufungua Kesi au kuwakilisha Malalamiko,Kufukuza kazi Watu wasikua waadilifu, kuomba misaada kutoka kwa watu ambao ni Wanaume kwa Mwanamke.

Kwa upande wa Sayari ya Attarid basi hua inahusiana na Elimu, Masomo, Sharia, Mawazo, Mawasiliano, na Utabibu.

Na hivyo Ndani ya wakati wake hua ni vizuri kufanya amali zenye kuhitaji Kufanikisha kuhusiana na Masomo,Mawasiliano baina ya watu tofauti, Kusomesha, Kujifunza, Maombi ya Kuomba Kazi, Kufanya biashara, Kuuza na Kununua, kuomba misaada kutoka kwa Majirani au Wafanyakazi wenzako.

Kwa upande wa Sayari ya Mushtara basi hua inahusiana na Muongezeko wa kitu, Mafanikio ya Kitu, Huruma, Safari za masafa marefu, kupata Bahati, Ufahamu Mkubwa n.k.

Na hivyo Ndani yake hua ni Vizuri kufanya Amali zenye kuhitajia Hikma na Busara ndani yake, Uchumi, Kutafuta ushindi, Kuomba misaada kutoka kwa Wazee wa Wazee, Ndugu Wa Wazee, Matabibu, washauri wa Sharia, Uchumi n.k.

Kwa upande wa Sayari ya Zuhra basi hua inahusiana na Mapenzi, Vitu na mambo Mazuri, Mapambo, Anasa, na Ubunifu.

Na hivyo ndani yake hua ni vizuri kufanya Amali za Mahusiano ya Mapenzi, Ndoa, Mafanikio ya Kijamii na Kimapenzi, Mikutano ya Kijamii, Makubaliano ya Kijamii, Matembezi, Kuomba misaada au vitu kutoka kwa Wanawake, n.k

Kwa upande wa Sayari ya Zohal basi hua ni yenye kuhusiana na Mambo ya muda mrefu na yenye kuhitaji Subra, Kazi, Vitega Uchumi, Taasisi mbali mbali ikiwemo Hospitali na Jela, nk.

Hivyo ndani ya wakati wake hua ni vizuri kufanya Amali zenye kuhitaji Kuwaadabisha watu, Kuwarekebisha watu, Kurudisha Uchawi, Kutengua Uchawi, Kumtoa Jini Sugu, Kupingana na Vikwazo, Kushinda matatizo yenye ugumu, Kutibu maradhi sugu, kuomba msaada kwa watu ambao ni wagumu kutoa misaada, kuomba misaada kwa viongozi, Kufunua Siri, n.k

Kwa upande wa Sayari ya Shams basi hua ni yenye kuhusiana na Mafanikio, Furaha, Maradhi, Malengo, Matamanio n.k

Na hivyo ndani ya Wakati wake hua ni vizuri kufanya Amali zenye kuhusiana na Mafanikio kwa ujumla, Kutafuta ufunuo wa Kiroho, Kutafuta kukubalika Kijamii, Kufanya maamuzi makubwa, Kua na nguvu na uwezo juu ya kitu, Kuanzisha Miradi mipya, Kuomba misaada kwa watu wenye Mamlaka ambao ni Wanaume kama, Baba, Mume, Mkuu wa Kazi n.k

UMUHIMU WA ATHARI ZA KISAYARI KATIKA KUANDIKA NAKSHI AU TAAWIDH

Kama ilivyokua kuna umuhimu wa kufuatiliana kujua kuhusiana na kufanya amali husika katika nyakati husika kulingana na sayari basi na pia hua kuna umuhimu wa kujua kuhusiana na Nyakati maalum za Kuandika Kombe, Nakshi na Taawidh ili kufanikisha malengo yake ipasavyo.

Hivyo wakati wa kuandika vitu hivi basi hua inabidi Mtu awe katika hali ya unadhifu wa kimwili na mavazi na hivyo ni lazima kua na Udhu, Kua katika sehemu ya Faragha na hivyo Kutozungumza na Mtu mwengine katika wakati wa Kuandika.

Na kulingana na malengo ya Utatuzi wa Tatizo husika basi kila Nakshi, Kombe na Taawidh hua zimegawika katika sehemu nne zinazotegemea athari za Maumbile ya asili ambazo ni:

Athari ya Moto: Ambayo hua ni yenye kutumika kwa ajili ya Kuwashinda Wapinzani wenye Nguvu zaid Kiukubwa au Kimamlaka, Kukimbiza Jina Mizi, Kuomba Msaada kutokana na Viumbe wa Al Ghayb, Kutekeleza Jambo unalolitaka, Kumuangamiza Adui, n.k basi hua ni vizuri Kufanya maandalizi ya uandishi huo huku ukiwa unaangalia Upande wa Mashariki na unatakiwa unapokaa uwe umekalia paja kwa mmoja huku mguu mwengine ukiwa umeukunja na goti kugusa kifua chako, na uzuri kuwe na mto unaowaka karibu yako.

Athari Ya Hewa: Ambayo hua ni yenye kutumika kwa ajili ya kumdhibiti Mtu kupitia kwenye ufahamu wake, iwe adui au rafiki, Kutafuta Ushindi, Kufanikisha malengo, Kukuza mahusiano, mawasiliano, kuongeza Kipato. Kupanda darja n.k na hii hua ni vizuri kuandika huku ukiwa umekaa Kitako na kuelekea upande wa Magharibi na huku kartasi unayoandikia ikiwa umeiweka kwenye Paja lako la kulia.

Athari ya Maji: Ambayo hua ni yenye kutumika kwa ajili ya kuwafanya Watu waachiwe kutoka kwenye Madhila au Vifungoni, kuwaokoa kutokana na matatizo mbali mbali, Kumfunga Ulimi Adui

yako, Kumzuia Ufahamu wake usifahamu kitu juu yako, Kupendwa, Kupata Nafuu kutokana na Maumivu Fulani, n.k na hii hua ni vizuri kuandika huku ukiwa umeelekea upande wa Kaskazini na uzuri kuwe na maji karibu yako au chanzo cha maji karibu yako.

Athari ya Udongo: Ambayo hua ni yenye kutumika kwa ajili ya kuwaangamiza na kuwateketeza maadui au viumbe wenye kusababisha madhara makubwa, Kuwafunga Ulimi watu ili wasikusababishie madhara kwa maneno yao, Kuzuia kitu chochote kile kinachosababisha madhara, kuwazuia watu wasizini n.k na hii hua ni vizuri kuiandika huku ukiwa umeleekea upande wa Kusini na ukiwa umekaa mkao wa Kukalia Paja lako.

Ama kuhusiana na nyakati za Kuandika basi hua pia inatakiwa kulingana na mfumo ufuatao:

Kuhusiana na Mahusiano ya Mapenzi, Mafanikio, Mali, Utajiri, Kazi, Kupata Ushindi, Kuomba msaada wa Uliwengu wa Al Ghayb, Kutatua matatizo, Kumtoa mtu kifungoni n.k basi ni vizuri kuandika katika nyakati za asubuhi.

Ama Kuhusiana na Utabibu basi iwe kabla ya Saa sita Mchana.

Kuhusiana na Kumuangamiza Adui na kutaka ushindi dhidi ya maadui au wapinzani, basi ni vizuri kuandika baina ya saa nane mchana hadi saa kumi jioni.

Ama kuhusiana na kuvunja kuvunja umoja wa Maadui, kumkamata aliefanya ubaya n.k basi ni vizuri kuandika katika wakati wa saa nane mchana hadi saa kumi na moja jioni.

Na kuhusiaana na kutafuta Usalama, Heshima na kuwatuliza na kuwapatanisha watu basi ni vizuri kuandika katika wakati wa saa 12 jioni.

MANUFAA YA ZAFARANI

Amesema Abu Hurayrah kua: '**Mimi nilimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, Hivi* Jee Pepo imeumbwa kwa kitu gani?' na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Matofali yake ni ya Fedha na Dhahabu, Hewa yake ni yenye Harufu kali ya Miski, Chembe za mchanga wake ni zake ni za Lulu na Rubi na Ardhi yake ni Zafarani, Yeyote yule atakaeingia ndani yake atapata raha bila ya kua ni mwenye kuvunjika Moyo na Umilele usiokua na Kifo, Nguo zao hazitopauka rangi wala kuchakaa na miili yao itakua na ujana wa Milele '**(Imam At Tirmidhi)

Naam mbali ya kua Zafarani ndio itakayokua ardhi ya Peponi lakini pia Zafarani ndio Taji la Ufalme wa mimea kwani Zafarani ni Mmea wa Dhahabu. Ambao sifa yake ya kua ni Dhahabu haitokani na kua na rangi ya Dhahabu tu lakini pia hutokana na manufaa yake, kwani Zafarani ina Manufaa ya kiwiliwili na kiroho pia kwa Ibn Adam.

Ambapo anasema Alama Ibn Sinna kua Kunywa au Kuila Zafarani hua kwenye kupelekea Kunawirisha Uso, Kunatia Uchangamfu wa Mwili na akili, ni Dawa yenye kusafisha na kuviongeza nguvu za ufanyaji kazi Viungo vya ndani ya Mwili ikiwemo Ini, Figo, Mapafu n.k huongeza kinga ya Mwili na ni kinga yenye kupingana na Maradhi ya Saratani za aina tofauti, na kuunawirisha na kuutia nguvu Moyo, huogeza nuru ya Macho pia na kuunawirisha ufanyaji kazi wa viungo vya hisia ikiwemo Ubongo na kuogeza nguvu za ufahamu na kumbukumbu.

Zafarani ni yenye uwezo wa kuondoa Maumivu na Uvimbe wa viungo vya Mwili, kuponesha matatizo ya Koo na Ngozi kuanzia kwenye Chunusi Mapele hadi kwenye Mba, na pia ni yenye kuongeza Uwezo wa Hamu na Nguvu za Ufanyaji mapenzi kwa Wanaume na Wanawake na pia huongeza uzalishwaji wa Mayai ya Uzazi.

Zafarani hua ni yenye kuzuia upunguaji wa Nywele na kupigana vita dhidi ya Mba na kunawirisha Ngozi ya kichwa na kufunua tundu za ngozi na kuifanya kua ni yenye kupumua ipasavyo na kutoa uchafu usiostahiki kubakia ndani ya Ngozi ya mwili na hupunguza hamu ya kula kwa wenye tatizo la kupenda kula ovyo.

Kwa hivyo haishangazi kuona kua Zafarani ndio Wino ambao unaopendekezwa kutumiwa katika matibabu ya maradhi mbali mbali kwa kupitia katika njia ya kuandika Aya za Qur’an au Majina ya *Allah Subhanah wa Ta’ala, Dua n.k*

MANUFAA YA UBANI MAKKAH.

Faida za Ubani Makkah kwa Figo
Husaidia wagonjwa wa kushindwa kwa figo, kuvimbiwa na upungufu kwani husaidia kuongeza asilimia ya ukolezi katika usagaji chakula wa protini.
Kwa matumizi ya nyuzi katika chakula cha mchana, huinua mchakato wa kuondoa dalili zilizofanyika katika kesi ya kushindwa kwa figo kupitia njia ya uke.
Wote unahitaji kufanya ni kuongeza sawa na gramu 50 kwa siku ya Ubani Makkah iliyoyeyushwa katika vyakula ili kuondokana na magonjwa ya muda mrefu ya figo kwa kiasi kikubwa.
Hii inathibitishwa na uchambuzi wa matibabu na vipimo kwa sababu inafanya kazi juu ya upungufu wa mkojo katika damu na kukwangua kwa makohozi.

Faida za Ubani Makkah kwa Kupunguza Uzito
Shukrani kwa upatikanaji wa vitu vinavyosaidia kuchoma mafuta na mafuta kutoka kwa mwili, kurekebisha uwiano wa sukari ya damu na kuongeza asilimia ya kuungua ya enzymes hatari katika mwili, Ubani Makkah inachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza uzito.
Pia husaidia kujaza tumbo na kulifanya lijisikie limejaa nyuzinyuzi zilizopo ndani yake.
Hivyo husaidia kupunguza uzito kwa kiasi kikubwa huku ukiweka vitamini na madini yote mwilini na kutoa sumu ya unene tu.

Faida za Ubani Makkah kwa Wagonjwa wa Sukari
Kutumia kinywaji cha Ubani Makkah cha Kiarabu kila siku husaidia kupunguza kiwango cha sukari kwenye damu.
Pia hupunguza asilimia ya ufyonzaji wa mwili wa sukari iliyohifadhiwa kwenye chakula, katika vinasaba, sukari bandia, mafuta n.k., ambayo huongeza kiwango cha vimeng'enya vya usagaji wa mafuta na sukari kwenye damu, na ikiwa inaendelea, ahueni kamili. kutoka kwa kisukari itafanyika, Mungu akipenda

Faida za Ubani Makkah kwa Kidole Tumbo.
Ubani Makkah inapunguza shughuli za jeni, ambazo kwa upande hucheza dhidi ya kuvimba kwa koloni na mikazo ya misuli kwenye tumbo ambayo husababisha maumivu ya papo hapo kwenye eneo la matumbo.
Pia husaidia kuzuia saratani ya utumbo mpana kwa kula gum ya Kiarabu kwenye milo yetu.
Pia na maumivu na tumbo katika tumbo na utumbo na kutokuwa na uwezo wa kutoa gesi kutoka kwa mwili kwa kawaida ili kuondoa uvimbe wa misuli na tumbo.
Ongeza gundi kidogo ya Kiarabu na maji ya moto na mbegu za cumin kidogo.

Faida za Ubani Makkah kwa ngozi

Ubani Makkah hutumiwa katika creams nyingi za huduma za ngozi, ambapo hupunguza ngozi na kurekebisha kiwango cha uondoaji wa mafuta kwenye uso na mwili.
Hivyo basi kuondoa matatizo mengi ya uso kama vile chachu na chunusi zenye kuudhi pamoja na kinga ya ngozi kutokana na kuchomwa na jua kali.
Pia hutumiwa kwa ajili ya matibabu ya magonjwa ya uke, kuwasha nje na ngozi katika sehemu za siri.
Pia inaimarisha uso na kupunguza mikunjo, na inaweza kutumika kama mask ya kujitengenezea nyumbani kwa kuongeza uumbaji kidogo na Ubani Makkah, kumwaga maji na kuipaka kwenye ngozi nayo, kisha kuiosha baada ya kukauka kwenye uso.

Faida za Ubani Makkah kwa watoto
Ubani Makkah ina maudhui ya juu ya kalsiamu, ambayo husaidia kujenga mifupa ya watoto kwa takriban kiasi sawa na maziwa ya mama.
Aidha, inasaidia kuimarisha kinga katika miili yao na kuwaepusha na ugonjwa wa pumu au kikohozi kikali, pia hufanya miili ya watoto kuwa hai zaidi na kusaidia kurahisisha akili zao.
Kwa hivyo Ubani Makkah inaweza kuongezwa kwa watoto wakati wa kuwatengenezea peremende badala ya kutumia jeli au Nasha itafanya chakula na peremende kuwa ngumu na kushikana kama jeli na kuwapa ulinzi kamili.

Faida za Gundi ya Nywele ya Kiarabu
Kama tulivyosema, Ubani Makkah ni matajiri katika nyuzi na protini, kwa hiyo ina viungo kuu vya kulinda nywele kutokana na kuanguka, dandruff au udhaifu kwenye mizizi.
Pia huchangia katika matibabu ya mbweha ambao huonekana kwenye kichwa na husababisha kula kwa mizizi na upara katika maeneo fulani, hivyo Ubani Makkah huunda dutu na safu ya kujitenga na magonjwa haya.
Hii ni kwa sababu ya sifa na fomula inayopatikana ndani yake kwani inadhibiti kiwango cha maneno ya greasi katika nywele ikiwa ni kutoka kwa nywele zenye greasi au kuzipa unyevu ambao hurekebisha na kutibu shida nyingi za nywele bila kusababisha uharibifu au uharibifu wa nywele.
Ubani Makkah hutumika katika uundaji wa aina ghali zaidi za mafuta ya matibabu ya nywele na shampoos kwa hivyo changanya Ubani Makkah na asali kidogo au maji tu na osha nywele nayo na uziache kwa karibu masaa mawili na kisha kuoga mara kwa mara na utambue tofauti.

Faida za Ubani Makkah kwa Ini
Ubani Makkah hulinda dhidi ya magonjwa ya kawaida ya ini kama vile nyuzinyuzi za ini au viwango vya kuongezeka kwa vimeng'enya vya ini ambavyo huharibu ini na kuwatia sumu.
Hii ni kutokana na udhibiti wa dutu ya Ubani Makkah katika kiwango cha sukari ya damu na kudhibiti asilimia ya suala la njano kwenye ini.
Mbali na kuamsha na kurejesha seli nyekundu za damu kwa kuimarisha ini na tishu kwa ufanisi kwa kuongeza Ubani Makkah katika vyakula au kuchukua kikombe kimoja kila siku baada ya kufutwa kwa maji.

Faida za Ubani Makkah kwa binadamu
Ina faida nyingi, yaani kuongeza ufanisi wa ubongo na mfumo wa neva.
Hulinda mfumo wa uzazi dhidi ya dalili za kuvimba na kuwashwa na inalinda mfumo wa mkojo kutoka kwa kuziba njia ya mkojo kutoka kwa mkusanyiko wa mawe.
Husaidia kudumisha afya ya mfumo wa utumbo na kuulinda na dalili za kuharisha au kuvimbiwa ili kurekebisha uwiano wake mwilini.

Faida za Ubani Makkah kwa mifupa
Kama tulivyosema hapo awali, Ubani Makkah ina kalsiamu nyingi, ambayo husaidia kuimarisha mifupa na kuilinda kutokana na hatari za kuvunjika kwa mfupa.
Pia husaidia kuponya nyufa za mifupa zinazosababishwa katika sehemu yoyote ya mwili wa binadamu ili iweze kupona haraka.

Ubani Makkah inachukuliwa dozi mbili katika kesi ya fractures katika mwili au inachukuliwa kwa kiasi cha wastani ili kuimarisha muundo wa mfupa, hasa kwa watoto au wazee ambao huathirika zaidi na fkufanya ufa kwa mifupa

Faida za matibabu za Ubani Makkah
Huongeza kinga ya mwili kwa wagonjwa wa saratani au Ukimwi kupitia uzalishaji mkubwa wa seli za ute mwilini, hivyo huingiza dawa nyingi za kitabibu na matibabu kusaidia kuondoa magonjwa haya.
Inasaidia kutengeneza bakteria wazuri, ambao husaidia kuondoa magonjwa mengi ya matumbo na figo.

Jinsi ya kula Ubani Makkah
Kwa sababu ya ugumu wa Ubani Makkah, inapendelea kutumika kama poda ili iwe rahisi kuyeyuka.
Kusaga kwa upole na grinder au chombo maalum cha kusaga.
Kiwango kilichopendekezwa cha kila siku cha Ubani Makkah ni gramu 50 kwa siku, ambayo ni kuhusu vijiko 4.
Tunatayarisha kinywaji cha Ubani Makkah kwa kuweka kijiko au 2 ya Ubani Makkah katika glasi ya maji ya uvuguvugu, koroga vizuri na kuacha kuyeyuka kabisa kwa angalau saa moja hadi saa mbili.
Pendelea kunywa kinywaji hiki mara mbili kwa siku asubuhi na jioni.
Kuzingatia ladha ya ladha yake, inawezekana kuiweka pamoja na vinywaji vingine vya moto au baridi

AINA ZA NAKSHI NA TAAWIDH

Tawidh maana yake hua kitu ambacho ndani yake kina Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yaani aya za Qur'an na Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na yanayokubalika kulingana na sharia za Kiislam ndani yake kwa ajili ya kufanikisha kitu au jambo fulani.

Uandishi wa Nakshi au Taawidh hua ni aina ya Ilm ambayo ni yenye malengo ya kuainisha uwezo wa nguvu za siri za Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, Aya Za Qur'an au maneno husika kulingana na athari inayohitajika katika kutoa matokeo stahiki kulingana na nia husika katika wakati wa utayarishaji wake.

Na hivyo hua haitakiwi kuandika Nakshi kwa ajili ya kusababisha madhara, wala kutumia maneno au michoro inayowakilisha ya shirk ndani yake, kwani Nakshi na Tawith zenye malengo hayo na maneno na michoro hio hua hazikubaliki kisharia na hii ni kulingana vithibisho vifuatavyo ambavyo ndani yake vinaainisha aina ya Nakshi zinazokubalika na zisizokubalika.

Anasema Imam At Tirmidhii kua: **'Amesema Amr Ibn Shuyab kua amesema Baba yake kua amesema Babu yake (yaani Amr Ibn Al As *Radhi Allahu Anhu*) *kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitufundisha sisi katika wakati tunapokua na khofu kama usingizini kua tuseme: *'Audhu bikalimati Allahi Tamat min Ghadhabihi wa Sharrihiwa min hamazat al Shayatina wa Aan Yahdhurun'* ambapo Abd Allah Ibn Amr alikua wakiwafundisha Watoto wake waliokua na umri wa kuweza kufahamu, na alikua akiwaandikia na kuwafungia wale Watoto wake ambao walikua hawafaham'***(Sunat At Tirmidhii Kitab Ad Dawat Toleo la 5 Hadith nambari 3528)*

Ambapo hadithi kama hii tena imenukuliwa na Imam Abu Daud ambae yeye alisema kua aliekua akifanya hivi alikua ni Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu.*

Na Hadithi hi pia imenukuliwa na Imam Ahmad Ibn Hanbal, katika Musnad yake ,Imam Al Bukhari, Imam Ibn Abi Shaybah katika Musannaf, Imam Al Hakim katika Mustadrak 1/548,Imam AlBayhaqi katika Kitab Al Adab,Imam Al Baghawi katika Masabih Sunnah, Imam An Nasai katika Amal Al Yawm

wa Laylah, Imam Al Mundhiri katika Mukhtasar Sunan Abu Daud, Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi katika Mafatih Al Ghayb Tafsir ya aya ya 97 ya Surat Al Muuminun,Imam An Nawawi katika Al Adhkar, Imam Adh Dhahabi katika Al Tibb An Nabawi, Imam Ibn Al Qayyim katika Zad Al Maad, Qadhi Al Shawqani katika Tafsir ya aya ya 97 ya *Surat Al Muuminun.*

Ambapo Imam Al Bukhari amesema pia kua: '**Ahmad Ibn Khalid kua amesema Ismail kua amesema Amr Ibn Shuayb kua amesema Baba yake kua : Walid Ibn Walid alikua akishtuka kutoka usingizini na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia asome maneno yafuatayo: *Audhu bi Kalimatillah al taamat mi ghadhabihi wa sharri Ibadihi wa mi hamazat Al Sshayatina wa an Yahdhurun'* pale atakapolala a alipofanya hivi basi akawa hashtuki tena na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akiwafundisha Watoto wake maneno haya kwa wale waliokua na ufahamu na wasiokua na ufahamu alikua akiwafunga nayo**.*(Khalq Af al al Ibad)*

Ambapo amesema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqalani kua: '**Ama kuhusiana na Tamaim ambazo ni zenye kua na aina ya Dhikr ndani yake basi hakuna kutokukubalika juu yake kwani ndani yake hua mnatafutwa baraka na ulinzi kupitia katika Majina ya *Allah Subhaanh wa Ta'ala* na Dhikr Allah'**(Fath Al Barri 6/164)

Imam Adh Dhahabi kua: '**Ama kuhusiana na Taawidh kua haipendwi ni kutokana na pale mtu atakapokua anaamini kua Taawidh yenyewe ndio yenye uwezo wa kuleta athari inayotakiwa kwa kunufaisha au kwa kudhuru, au iwe imejumuisha maneno ambayo hayafahamiki'**

Ambapo Imam Said Ibn Al Muassayib aliulizwa kuhusiana na wenye Kuvaa Tawidh nae akasema kua**: 'Taawidh hua haina ubaya pale itakapokua imeshonewa kwangozi'**

Na Imam Ata Ibn Ab Rabah aliulizwa kuhusiana na Tawidh ambapo nae akasema: **'Haina Tatizo kuandika Aya ya Quran na kisha ukaifunga ndani ya kitu'** na akasema kuhusiana nayo pale inapokua anayo mwanammke aliekua katika siku zake ambapo nae akasema: **'Hamna tatizo bali itambidi aivue pale inapokua kwenye kifuko cha ngozi ama inapokua kwenye kifuko cha fedha basi kama akitaka anaweza kuivua na kama anataka anaweza kubakia nayo'**

Na Imam Ibn Abd Al Barr akasema kua: **'Hakuna kosa katika kuandika Ruqya zenye Majina ya Allah na kisha kuifunga kwenye shingo ya Mtu anaeumwa kwa ajili ya kutafuta athari ya uponeshaji inayopatikana ndani yake pale inapokua hakuna ndani yake nia ya kujizuia na hasad au kijicho kabla ya kuathirika nayo, lakini kam aikiwa athari tayari zimeshafika basi inakubalika kusoma Ruqya na kujinga nayo kulingana na Mtizamo wa Imam Malik***(Al Tahmid 17/161)'*

Ama kuhusiana na Waqf au Nakshi ambazo hua ni michoro yenye vyumba vililivyopangana kwa idadi fulani kulingana na malengo na makusudio kwa mfano 3 kwa 3 , 4 kwa 4, 5 kwa 5 nk ambapo ndani yake vyumba hivyo hua vinabeba nambari, Aya za Qur'an au herufi za Kiarabu ambazo zimewekwa kimpangilio kiasi ya kua ukizijumlisha kwa uzito wake kinambari kutoka kila upande basi hua unapata jawabu la aina moja basi anasema Al Muhaqqiq Imam Ibn Hajar Al Haythami Al Shafii kua: **'Hakuna kosa katika kutumia Ilm ya Awqaf pale inapokua hakuna kusababisha madhara ndani yake, yaani inapotumika kwa ajili ya kunufaisha, lakini kama ikiwa zitatumiwa kwa ajili ya usababisha madhara basi hua haikubaliki kutumika'** *(Fatawa Al Hadithiya)*

Na tunapozungumzia kuhusiana na Tawidh au Waqf zenye kujumuisha mpangilio wa vyumba vyumba ambavyo hua ni vyenye kujazwa kwa kutumia mfumo maalum kwa kila nambari, herufi au maneno ya Aya kujazwa kwenye chumba chake maalum kulingana idadi ya vyumba na kulingana na Utatuzi wa

tatizo husika, kulingana na uzito wa Athari husika, kwa mfano Nakshi ya Vumba 9 yaani vyumba 3 kwa vitatu ambao hua uko chini ya Athari ya Sayari ya Zuhal.

Ambapo ili kuuandaa Wakfu huu basi inabidi kupata idadi kamili kwa kila upande utakaohesabu kutafuta Jumla ya nakshi ya Vyumba 9 yenye jumla ya idadi ya 15 hua inabidi kuijaza katika mfumo ufuatao:

	=15	*=15*	*=15*	
=15	**8**	**1**	**6**	*=15*
=15	**3**	**5**	**7**	*=15*
=15	**4**	**9**	**2**	*=15*
	=15	*=15*	*=15*	

Yaani kwa mfano kama tukichukulia Waqf wa Bismillahi ambao kinambari hua na uzito wa nambari 786 basi ili kutengeeza Waqf wa vyumba 9 basi tunaichukua idadi hio ya 786 kisha tunatoa 12 yaani (786-12=774) na kisha jawabu inayopatikana yaani 774 tunaigawa kwa 3, yaani (774/3 = 258) na kisha tunaichukua jawabu hio iliyobakia ambayo ni 258 tunaiweka kwenye chumba nambari moja kisha tunaongeza idadi ya moja na hivyo itakua 259 ambayo tutaiweka kwenye chumba nambari 2 na kisha tunaongeza namba moja na hivyo itakua 260 na kuiweka kwenye chumba namba 3 na kisha tunaongeza moja na hivyo itakua 261 na kuiweka kwenye chumba namba 4 na kisha tunaongeza moja tena na kuiweka kwenye chumba husika hadi vyumba vijae kulingana na idadi yake kama inavyoonesha kwenye picha inayofuatia:

	=786	*=786*	*=786*	
=786	**265**	*(1)* **258**	**263**	*=786*
=786	*(3)* **260**	**262**	**264**	*=786*
=786	**261**	**266**	*(2)* **259**	*=786*
	=786	*=786*	*=786*	

Na kwenye Naqsh ya vyumba 16 basi ambayo ni vyumba vinne kwa vinne ambao hua uko chini ya Athari ya Sayari ya Mushtara basi hujazwa kwa mpangilio ufuatao.

8	11	14	1
13	2	7	12
3	16	9	6
10	5	4	15

Tuchukulie mfano wa Naqhi ya Surat Al Waqiah 102965-6 ambao ni wenye kuongeza Baraka katika Riziki ambao ni kama ufuatao:

25742	25744	25747	25733
25746	25734	25740	25745
25735	25749	25742	25739
25743	25738	25736	25748

Na kwenye Naqsh ya vyumba 25 basi ambayo ni vyumba vitano kwa vitano ambao hua uko chini ya Athari ya Sayari ya Mirikh basi hujazwa kwa mpangilio ufuatao.

1	26	19	13	7
14	8	2	22	20
23	16	15	9	3
10	4	24	17	11
18	12	6	5	25

Na kwenye Naqsh ya vyumba 36 basi ambayo ni vyumba sita kwa sita ambao hua uko chini ya Athari ya Sayari ya Shams basi hujazwa kwa mpangilio ufuatao.

1	35	3	34	32	6
30	8	28	27	11	7
13	23	22	21	14	18
24	17	16	15	20	19
12	26	9	10	29	25
31	2	33	4	5	36

Na kwenye Naqsh ya vyumba 49 basi ambayo ni vyumba saba kwa saba ambao hua uko chini ya Athari ya Sayari ya Zuhra basi hujazwa kwa mpangilio ufuatao.

22	47	16	41	10	35	4
5	23	48	17	42	11	29
30	6	24	49	18	36	12
13	31	7	25	43	19	37
38	14	32	1	26	44	20
21	39	8	33	2	27	45
46	15	40	9	34	3	28

Na kwenye Naqsh ya vyumba 64 basi ambayo ni vyumba vinane kwa vinane ambao hua uko chini ya Athari ya Sayari ya Attarid basi hujazwa kwa mpangilio ufuatao.

8	58	59	5	4	62	63	1
49	15	14	52	53	11	10	56
41	23	22	44	45	19	18	48
32	34	35	29	28	38	39	25
40	26	27	37	36	30	31	33
17	47	46	20	21	43	42	24
9	55	54	12	13	51	50	16
64	2	3	61	60	60	7	57

Na kwenye Naqsh ya vyumba 81 basi ambayo ni vyumba tisa kwa tisa ambao hua uko chini ya Athari ya Sayari ya Qamar basi hujazwa kwa mpangilio ufuatao:

37	78	29	70	21	62	13	54	5
6	38	79	30	71	22	63	14	46
47	7	39	80	31	72	23	55	15
16	48	8	40	81	32	64	24	56
57	17	49	9	41	73	33	65	25

26	58	18	50	1	42	74	34	66
62	27	59	10	51	2	43	75	35
36	68	19	60	11	52	3	44	76
77	28	69	20	61	12	53	4	45

Na kwenye Naqsh ya vyumba 100 basi ambayo ni vyumba kumi kwa kumi basi hujazwa kwa mpangilio ufuatao:

1	98	97	96	85	84	15	14	13	2
95	19	20	80	79	78	77	25	26	6
94	27	28	72	71	70	69	33	34	7
92	66	65	37	38	39	40	60	59	9
83	58	57	45	46	47	48	52	51	18
12	50	49	53	54	55	56	44	43	89
11	42	41	61	62	63	64	36	35	90
10	67	68	32	31	30	29	73	74	91
8	75	76	24	23	22	21	81	82	93
99	3	4	5	16	17	86	87	88	100

BUKHURI ZA SIKU KULINGANA NA AMALI HUSIKA

FUKIZO KULINGANA NA SIKU NA SAYARI NA AMALI HUSIKA			
SIKU	**SAYARI**	**FUKIZO LAKE**	**AMALI YAKE**
JUMAPILI	Shams	Sandalusi, Udi(Thuringite), Misk(Musk), Daarchini (Cinnamon)	Ufunguzi na Uanzilishi wa Jambo.
JUMATATU	Qamar	Ubani Makkah; Kafoor (Camphor), Shahed (Honey), Udi	Tiba ya Maradhi Tofauti
JUMANNE	Mirikh	Qist; Haltiti; Udi (Thuringite), UBANI (Frankincense)	Kupata Nguvu Kudhibiti na Kutenganisha
JUMATANO	Attarid	Kachiri; Kafur(Camphor), SandalWood,Karafuu Nyekundu.	Kustawisha kitu au Jambo
ALKHAMIS	Mushtara	Udi, Sandal Wood Nyekundu, Miski(Musk), Kafoor (Camphor),	Kupata Pesa Mali Au Utajiri
IJUMAA	Zuhra	Ubani Mashtaka,Sandal Wood Nyeupe, Kafur, (Amber	Mapenzi Kupenda au Kupendwa.
JUMAMOSI	Zohar	Miatun Saila; Udi, Mustard, Miski, Mdalasini (Cinnamon)	Kuadhibu Au Kuangamiza Uadui

MAMLAKA YA UTAWALA WA SAYARI KATIKA SAA ZA KILA SIKU ZA WIKI.

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Katika masaa 12 ya Siku ya Ijumaa mna saa ndani yake ambapo hakuna Mja atakaemuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* isipokua atampa kitu akitakacho, hivyo itafuteni katika saa ya mwisho baada ya Al Asr.*(Imam An Nasai)*

Na akasema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam aliomba* Dua katika *Masjid Fat-h* katika Siku ya Jumatatu na Jumanne na Jumatano na Dua Yake ilikubaliwa baina ya Wakati wa *Salat Dhuhr* na *Al Asr* ya siku ya Jumatano, na hivyo na mimi ikawa kila nikiwa na shida basi hua ni mwenye kusubiri katika wakati huo katia siku ya Jumatano kwa ajili ya kuomba Dua, na kila wakati nilipokua nikiomba Dua katika wakati huo basi Dua zangu zilikua zikikubaliwa'***(*Imam Bukhari*)

UTAWALA WA SAYARI KATIKA SAA ZA KILA SIKU ZA WIKI							
SAA	ZOHAR JUMAMOSI	SHAMS JUMAPILI	QAMAR JUMATATU	MIRIKH JUMANNE	ATTARID JUMATANO	MUSHTARA ALKHAMIS	ZUHRA IJUMAA
1 ASUBUHI	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA
2 ASUBUHI	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID
3 ASUBUHI	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR
4 ASUBUHI	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR
5 ASUBUHI	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA
6 ASUBUHI	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH
7 MCHANA	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAL	SHAMS
8 MCHANA	ZOHAL	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA
9 MCHANA	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID
10 JIONI	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR
11 JION	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR
12 JIONI	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA
UTAWALA WA SAYARI KATIKA SAA ZA USIKU WA KUAMKIA SIKU HUSIKA ZA WIKI							
	JUMAMOSI	JUMAPILI	JUMATATU	JUMANNE	JUMATANO	ALKHAMIS	IJUMAA
1 USIKU	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH
2 USIKU	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAL	SHAMS
3 USIKU	ZOHAL	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA
4 USIKU	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID
5 USIKU	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR
6 USIKU	ZOHAL	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA
7 USIKU	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID
8 USIKU	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR
9 USIKU	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR
10 USIKU	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA
11 AL FAJRI	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAR	SHAMS	QAMAR	MIRIKH
12 ALFAJRI	QAMAR	MIRIKH	ATTARID	MUSHTARA	ZUHRA	ZOHAL	SHAMS

Muhimu: Saa za kila siku hua zinabadilika kulingana na namna linavyochomoza Jua katika eneo ulilokuwepo, kama vile zinavyobadilika nyakati za Sala, au kama zinavyobadilika nyakati za Iftari inapoingia Sala ya Magharibi. Hivyo kwa baadhi ya siku inapokua Mchana mkubwa na Usiku Mdogo basi saa ya kwanza hua inaingia saa 12 na dakika kadhaa badala ya saa moja asubuhi, na saa ya 12 Jioni hua inaingia saa 1 kasorobo Jioni. Na katika siku ambazo Mchana unakua mdogo na Usiku Mkubwa basi saa kwanza hua inaingia Saa moja Kasorobo na Saa ya 12 Jioni hua inaingia saa 12 na robo. Kwa hivyo ilikufanikisha Amali husika katika wakati husika basi hapa kuna umuhimu kuangalia Jua linachomoza na linatua saa ngapi katika sehemu uliyokuwepo, kisha ndio utaweza kukisia mda wa sayari husika.

Na pia masaa ya wakati wa Mchana hua yanatofautiana na masaa ya wakati wa Usiku kama tulivyoona kwenye jadweli lililotangulia kua Saa Ya Kwanza ya Jumamosi Asubuhi hua ni Zohar lakini Saa ya Kwanza ya Siku hio hio Usiku hua ni Attarid ambayo hua inawakilisha siku ya Jumatano na hii ni kwa sababu kimfumo basi ili kupata saa ya Usiku wa kuamkia siku husika basi inabidi hua unarudi nyuma na kuruka siku mbili yaani Asubuhi ya siku ya Jumamosi hua ni Jumamosi lakini Usiku wa siku ya Jumamosi hupatika kwa kuziruka au kuzikiuka siku mbili zilizo nyuma ya siku ya Jumamosi yaani *Ijumaa na Alkhamis* na hivyo hua tunaanza kuhesabu na siku ya Jumatano, kama inavyoonesha kwenye Jadweli inayofuatia:

SIKU YA WIKI	USIKU WAKE HUWAKILISHWA NA SIKU YA
JUMAPILI	ALKHAMIS
JUMATATU	IJUMAA
JUMANNE	JUMAMOSI
JUMATANO	JUMAPILI
ALKHAMIS	JUMATATU
IJUMAA	JUMANNE
JUMAMOSI	JUMATANO

SAA ZA SHAMS KATIKA SIKU ZA WIKI NA AMALI ZAKE

Saa ya Shams katika Mchana wa siku ya Jumapili Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatano Kuamkia Alkhamis:

Jina tukufu La *Allah Subhanah wa Ta'ala ni Ya Hayyu Ya Qayyum* idadi yake ni 174 mara 7 au 21.
Kwa ajili aya Amali za kutafuta mafanikio ya kupata Darja, Cheo, Heshima, nk.
Dhikr za kunawirisha nguvu na uwezo wa Mtu kimuonekano na kimaumbile.
Amali za kuanzisha Uanzilishi wa Kitu au Ujenzi wa Kitu, Upandaji mazao Shambani.
Kwa ajili ya kutibu maradhi ya Moyo na Mapafu.

Saa ya Shams katika mchana wa siku ya Jumatatu Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Alkhamis Kuamkia Ijumaa:
Jina tukufu La *Allah Subhanah wa Ta'ala ni Ya Rahmani ya Rahim* idadi yake ni 554 mara 7 au 21.
Kwa ajili ya Amali za kutafuta kupata mafanikio ya kihisia kama Kusikia, Kuona Kupendwa n.k
Dhikr za kutafuta kupata mafanikio kwa Mke/Mume na mahusiano ya ndoa.
Amali za kujilinda dhidi ya Hasad, Kijicho, Wivu, Uadui n,k
Kwa ajili ya kutibu Maradhi ya Tumbo, Hedhi au Nifasi.

Saa ya Shams katika Mchana wa siku ya Jumanne Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Ijumaa kuamkia Jumamosi:
Jina tukufu La *Allah Subhanah wa Ta'ala ni Ya Maliku ya Quddus* idadi yake ni 234 mara 7 au 21.
Kwa ajili ya Amali za kutafuta Mafanikio ya Kivita na dhidi ya Maadui.
Kwa ajili ya Kushinda Vita au Makabiliao ya aina yeyote.
Kwa ajili ya kutibu Maradi ya sehemu za Siri.

Saa ya Shams katika Mchana wa siku ya Jumatano Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na usiku wa Jumamosi Kuamkia Jumapili:
Jina tukufu La *Allah Subhanah wa Ta'ala ni Ya Aliyyu ya Adhimun* idadi yake 1130 mara 7 au 21.
Kwa ajili ya mafanikio ya Ufunguzi wa Kibiashara na Mafanikio ya kuongeza Wanunuzi.
Kwa ajili ya kutibu Maradhi ya Ufahamu na Akili.

Saa ya Shams katika Mchana wa siku ya Alkhamis Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na usiku wa Jumapili kuamkia Jumatatu:
Jina tukufu La *Allah Subhanah wa Ta'ala ni Ya Mutakkabir ya Mutaali* idadi yake ni 773 mara 7 au 21.
Dhikr kwa ajili ya Amali za Kupata mafanikio ya Kuheshimika katika Jamii kwa Uwezo na Mali kua kama Mfalme wa Jamii.

Saa ya Shams katika Mchana wa siku ya Ijumaa Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku Jumatatu kuamkia Jumanne:
Jina tukufu La *Allah Subhanah wa Ta'ala ni Ya Kafii ya Ghaniyu* kwa idadi ya 1171 mara 7 au 21.
Dhikr ya Amali ya kukubalika na kuvutia katika Jamii
Kwa ajili ya Kutibu Maradhi ya Moyo na Mfumo wa Damu.

Saa ya Shams katika mchana wa siku ya Jumamosi Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumanne kuamkia Jumatano:
Jina tukufu La *Allah Subhanah wa Ta'ala ni Ya Fatahu ya Razzaq* kwa idadi ya 797 mara 7 au 21.
Kwa ajili ya kupata mafanikio katika Mamlaka, Utawala na uwezo katika sehemu husika.
Kwa ajili ya kupata mafanikio katika ujenzi na kazini
Kwa ajili kupata Mafanikio katika Kupanda mazao na Kuvuna.
Kwa ajili ya kutibu Maradhi ya Mfumo wa Mishipa ya Damu.

SAA ZA QAMAR KATIKA SIKU ZA WIKI NA AMALI ZAKE

Saa ya Qamar katika Mchana wa siku ya Jumapili Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatano Kuamkia Alkhamis:
Kwa ajili ya Amali za Kutafuta kukubalika katika Jamii.
Kwa ajili ya kukubalika kwa mwenza wako kifamilia au kwa mshirika wako kikazi na kimajukumu.
Kwa ajili ya amali za kujikinga na Hasad, Kijicho na Wivu.

Saa ya Qamar katika mchana wa siku ya Jumatatu Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Alkhamis Kuamkia Ijumaa:
Kwa ajili ya Amali za Kutafuta kukubalika na kupata umaarufu katika Jamii na kua na Ilm ya Kiroho

Saa ya Qamar katika Mchana wa siku ya Jumanne Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Ijumaa Kuamkia Jumamosi:

Kwa ajili ya Amali za Kutafuta Ushindi wa Kivita au Makabiliano dhidi ya Maadui au Wapinzani.

Saa ya Qamar katika Mchana wa siku ya Jumatano Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na usiku wa Siku Jumamosi Kuamkia Jumapili:
Kwa ajili ya Amali za Kujua kuhusiana na Waliofanya Jambo ovu husika, iwe wezi, wachawi, waliofanya husda, n.k na vizuri siku hii iwe ni ya tarehe ya mwezi 19 au usiku wa kuamkia 19 wa Kiislam.
Kwa ajili ya kwasiliana na Ulimwengu wa Al Ghayb
Kwa ajili ya amali za kuongeza ukubwa biashara na wingi wa mafanikio katika Jambo.

Saa ya Qamar katika Mchana wa siku ya Alkhamis Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na usiku wa Jumapili kuamkia Jumatatu:
Kwa ajili ya Amali za Kurahisisha kupata Kizazi au Nguvu za kurutubisha kizazi.
Kwa ajili ya Ujenzi na mambo ya Nyumbani.
Kwa ajili ya amali za Kilimo mashambani.
Kwa ajili ya kupata Umaarufu.

Saa ya Qamar katika Mchana wa siku ya Ijumaa Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatatu kuamkia Jumanne:
Kwa ajili ya Amali za Kutafuta kitu kilichopotea au kilichotoweka au kumrudisha mtu alietoroka.
Kwa ajili ya uwezo wa kutoweka mbele ya Macho za Watu na kuibukia katika sehemu nyengine.
Kwa ajili ya amali za Kuikunja Ardhi kwa kusafiri kutoka sehemu moja kueleka sehemu yengine hapo kwa hapo.

Saa ya Qamar katika Mchana wa siku ya Jumamosi Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na siku ya Jumanne kuamkia Jumatano:
Kwa ajili ya Amali za Kutibu maradhi ya Ngozi, Mgongo na Meno.
Kwa ajili ya Kulima na kupandikiza Shambani.

SAA ZA MIRIKH KATIKA SIKU ZA WIKI NA AMALI ZAKE

Saa ya Mirikh katika Mchana wa siku ya Jumapili Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatano Kuamkia Siku ya Alkhamis:

Kwa ajili ya Amali za Kuongeza Nguvu za Kimapigano
Kwa ajili ya kusababisha Ushindi katika Makabiliano ya Vita, Upinzani, Michezo n.k
Kwa ajili ya Kinga dhidi ya mashambulizi ya Maadui.

Saa ya Mirikh katika mchana wa siku ya Jumatatu Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Siku ya Alkhamis Kuamkia Ijumaa:
Kwa ajili ya Amali za Kufanikisha Utabibu wa Upasuaji.
Kwa ajili ya Kinga dhidi ya mashambulizi ya Maadui.

Saa ya Mirikh katika Mchana wa siku ya Jumanne Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Ijumaa Kuamkia Jumamosi:
Kwa ajili ya Amali za Mawasiliano ya kujikinga Kivita.
Kwa ajili ya kujiongezea Ushujaa na nguvu.
Kwa ajili ya Nguvu ya ushindi katika mashindano.

Saa ya Mirikh katika Mchana wa siku ya Jumatano Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili:
Kwa ajili ya Amali za Kuongeza uwezo wa Kimaarifa na kijuzi.

Saa ya Mirikh katika Mchana wa siku ya Alkhamis Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku Jumapili kuamkia Jumatatu:
Kwa ajili ya Amali zinazohusiana na Mapigano.
Kwa ajili ya kujiongezea Ushujaa na nguvu.
Kwa ajili ya Nguvu ya ushindi katika mashindano na Heshima.

Saa ya Mirikh katika Mchana wa siku ya Ijumaa Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumaatu kuamkia Jumanne:
Kwa ajili ya Amali za Kutafuta Mwenza wa Kifamilia, Kimapenzi Kuposa, Kutafuta mwenza wa Kikazi.
Kwa ajili ya mambo tofauti mazuri yenye kuleta mafanikio.

Saa ya Mirikh katika Mchana wa siku ya Jumamosi Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku Jumanne kuamkia Jumatano:
Kwa ajili ya Amali za kujikinga na uvamizi wa aina yeyote.
Kwa ajili ya kuanzisha au kuasisi mambo yanayohusiana na utafutaji wa hazina za Ardhini, kama migodi, visima mafuta, gesi n.k
Kwa ajili ya Kuwinda na kushambulia.

SAA ZA ATTARID KATIKA SIKU ZA WIKI NA AMALI ZAKE

Saa ya Attarid katika Mchana wa siku ya Jumapili Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatano Kuamkia Alkhamis:
Kwa ajili ya Amali za Mawasiliano ya Kisiasa na Kisanii.
Kwa ajili ya yanayohusu maombi kwa wenye Mamlaka.
Kwa ajili ya Nguvu ya ufunuo wa Ufaham.

Saa ya Attarid katika mchana wa siku ya Jumatatu Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Siku ya Alkhamis Kuamkia Ijumaa:
Kwa ajili ya Amali za Kutanua Ufahamu.
Kwa ajili ya yanayohusu maombi ya Ushirikiano katika Jamii, kuandika Khutba, Kuhutubia n.k ambapo watu watakukubali na kukushangilia bila ya kufahamu unazungumzia kuhusiana na nini.
Kwa ajili ya Nguvu ya Ufaham wa Vitu vya Al Ghaib, Yaliyotokea, Kubashiri, Uchawi na Ufasiri wa Ndoto.
Na kwa wakati wa Usiku basi hua ni Mujarrab kwa Kumhamisha Mtu au kusafiri.

Saa ya Attarid katika Mchana wa siku ya Jumanne Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Ijumaa kuamkia Jumamosi:
Kwa ajili ya Amali za Mawasiliano ya Kisiasa na Kisanii
Kwa ajili ya yanayohusu matayarisho ya Mapigano ya kutumia mikono.
Kwa wakati wa usiku wake basi ni kwa ajili ya kutafuta Nguvu ya kujidhibiti na kua na subra.

Saa ya Attarid katika Mchana wa siku ya Jumatano Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili:
Kwa ajili ya Amali za Mawasiliano na uwezo wa Kuzingatia.

Kwa ajili ya yanayohusu uwezo wa Kujishughulisha kujitafutia Maisha kwa kutumia mikono
Kwa ajili ya Nguvu ya ufunuo wa Ufaham na Umahiri wa Lugha.
Na kwa wakati wa usiku wake ni kwa ajili ya kuomba uwezo mkubwa wa kua na ubunifu.

Saa ya Attarid katika Mchana wa siku ya Alkhamis Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumapili kuamkia Jumatatu:
Kwa ajili ya Amali za Mawasiliano ya Kufanikisha Mapatano ya Pesa, Kesi, Mkopo, Misaada, n.k
Kwa ajili ya yanayohusu Mahesabu na Uchumi kupata Malipo makubwa Zaidi katika Jambo.
Na kwa wakati wa Usiku ni Kwa ajili ya Nguvu ya ufunuo wa Ufaham.

Saa ya Attarid katika Mchana wa siku ya Ijumaa Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatatu kuamkia Jumanne:
Kwa ajili ya Amali za Kufanikisha Mawasiliano ya Makubaliano ya Kimapenzi, Kibiashara, Kiushirika
Kwa ajili ya yanayohusu ufafanuzi wa yasiyofahamika, au yasiyojulikana.
Kwa ajili ya Nguvu ya ufunuo juu ya Mtu aliekimbia, alieondoka,aliesafarini aliekua mbali n.k.
Kwa ajili ya Kumrudisha Mtu alieondoka au alieachana nawe au alievunja makubaliano.
Ambapo kwa upande wa wakati wa usiku wake basi hua ni kwa ajili ya Kumvuta Mtu na kumuachisha Huru Mtu aliefungwa, au aliekua matatizoni.

Saa ya Attarid katika Mchana wa siku ya Jumamosi Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumanne kuamkia Jumatano:
Kwa ajili ya Amali za Kufanikisha Mambo ya Kielimu, Masomo na kufuzu Mitihani, Kupata Nafasi ya chou n.k
Kwa ajili ya Kutibu Ugonjwa wa akili, wa kusahau na kuongeza ufahamu wa mtu.
Ambapo kwa upande wa wakati wa usiku wake basi hua ni kwa ajili ya kumuachisha Huru Mtu aliefungwa, au aliekua matatizoni.

SAA ZA MUSHTARA KATIKA SIKU ZA WIKI NA AMALI ZAKE

Saa ya Mushtara katika Mchana wa siku ya Jumapili Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatano Kuamkia Siku ya Alkhamis:

Kwa ajili ya Amali za Kujiongezea Mali, Utajiri,Cheo, Mamlaka, na kila aina ya mambo ya Kifalme.
Kwa ajili ya yanayohusu kuanzisha Mipango mipya, Miradi mipya au Jambo jipya.
Kwa ajili ya kupanda Mashambani kutakakolea mavuno makubwa sana, kwa ajili ya kila jambo la kiuchumi. Na ikiwa ni katika wakati wa Mwezi mpevu basi ndio manufaa hua maradufu.
Na kwa wakati wa Usiku ni Kwa ajili ya Nguvu ya ufunuo wa Ufaham.

Saa ya Mushtara katika mchana wa siku ya Jumatatu Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Siku ya Alkhamis Kuamkia Ijumaa:
Kwa ajili ya Amali za kuanzisha kitu kipya.
Kwa ajili ya Kutafuta mtoto baina ya Mume na Mke.
Kwa ajili ya Kuimarisha na kupamba Makazi, Kuhamia katika Nyumba mpya.
Kwa ajili ya kupata Umaarufu, kushinda Uchaguzi, n.k

Saa ya Mushtara katika Mchana wa siku ya Jumanne Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku Ijumaa kuamkia Jumamosi:
Kwa ajili ya Amali za Kuimarisha Nguvu za Kijeshi na Kivita.

Kwa ajili Amali za Kuimarisha Uzazi na Kuilinda Mimba isitoke.

Saa ya Mushtara katika Mchana wa siku ya Jumatano Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili:
Kwa ajili ya Amali za Kujiongezea Mali, na kufungua Biashara na Kuteka Masoko Kibiashara.
Kwa ajili ya kupanga Bajeti ya kitu na mahesabu.
Kwa ajili ya Kutubu na kutatua matatizo ya Akili na Ufaham.

Saa ya Mushtara katika Mchana wa siku ya Alkhamis Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumapili kuamkia Jumatatu:
Kwa ajili ya Amali za Kuanzisha Mifuko ya Kijamii na mambo yanayohusiana na hazina au benki.
Kwa ajili ya Kuvutia kimuonekano na kimali.

Saa ya Mushtara katika Mchana wa siku ya Ijumaa Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatatu kuamkia Jumanne:
Kwa ajili ya Amali za Kutafuta kilichopotea, kumpata alieondoka n.k
Kwa ajili ya kua na Muonekano mzuri wa kuvutia kihisia.
Kwa ajili ya Kupendwa na Wanawake.

Saa ya Mushtara katika Mchana wa siku ya Jumamosi Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumannae kuamkia Jumatano:
Kwa ajili ya Amali za Kushinda Kesi Mahakamani, Mashindano au migogoro.
Kwa ajili ya yanayohusiana na Mashamba na ardhi.
Kwa ajili ya Kujenga Nyumba.
Kwa ajili ya kupanda na kuvuna.

SAA ZA ZUHRA KATIKA SIKU ZA WIKI NA AMALI ZAKE

Saa ya Zuhra katika Mchana wa siku ya Jumapili Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatano Kuamkia Alkhamis:

Kwa ajili ya Amali za Kujenga Mahusiano katika Jamii.
Kwa ajili ya yanayohusu kukubalika na wanafamilia,wazee n.k
Kwa ajili ya Kuikunja Ardhi kwa usafiri kutoka katika sehemu moja kulekea nyengine kwa kasi kubwa sana.

Saa ya Zuhra katika mchana wa siku ya Jumatatu Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Siku ya Alkhamis Kuamkia Ijumaa:

Kwa ajili ya yanayohusu kukubalika na wanafamilia, wazee n.k
Kwa ajili ya Kuikunja Ardhi kwa kusafiri kutoka katika sehemu moja kulekea nyengine kwa kasi kubwa sana.
Na wakati wa Usiku kwa ajili ya Kujua siri ya yaliyotokea au yaliyoonekana kwenye ndoto na ubashiri.

Saa ya Zuhra katika Mchana wa siku ya Jumanne Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Ijumaa kuamkia Jumamosi:
Kwa ajili ya Amali za Kumrudisha Mtu alierushwa, aliekimbia au alieachana na watu wake.
Kwa ajili ya Kumvuta Mtu Kimapenzi.

Saa ya Zuhra katika Mchana wa siku ya Jumatano Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili:
Kwa ajili ya Amali za Kupatanisha waliogombana, Waliotengana, Walioachana n.k
Na kwa wakati wa Usiku kwa ajili ya kuwarudisha na kuwagundua waliofanya madhara, iwe wezi, Wachawi, Mahasidi, Maadui n.k

Saa ya Zuhra katika Mchana wa siku ya Alkhamis Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumapili kuamkia Jumatatu:
Kwa ajili ya Amali za Kukubalika kimashirikiano katika Kazi, Biashara, Miradi mbalimbali n.k
Kwa ajili ya Kumvuta Mtu na kukubalia Kimapenzi.
Kwa ajili ya kurudisha kile kilichotoka kibiashara au kikazi au kifamilia.
Ama katika wakati wa Usiku wake hua ni kwa ajili ya Kufanikisha mambo ya Kidini na Kiroho.

Saa ya Zuhra katika Mchana wa siku ya Ijumaa Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatatu kuamkia Jumanne:
Kwa ajili ya Amali za Kukubalika kimahusiano.
Kwa ajili ya Kumvuta Mtu na kukubalia Kimapenzi.
Ama katika wakati wa Usiku wake hua nik wa ajili ya Kumgudua Mwizi au adui yako.

Saa ya Zuhra katika Mchana wa siku ya Jumamosi Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumanne kuamkia Jumatano:
Hakuna athari yeyote.

SAA ZA ZOHAL KATIKA SIKU ZA WIKI NA AMALI ZAKE

Saa ya Zohal katika Mchana wa siku ya Jumapili Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatano Kuamkia Alkhamis:
Kwa ajili ya Amali za Kujiongezea uwezo wa Kujiamini katika Mambo tofauti.
Kwa ajili ya Kujikinga dhidi ya madhara ya Moto.
Haifai kufanya Amali za Tiba ndani yake.

Saa ya Zohal katika mchana wa siku ya Jumatatu Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Alkhamis Kuamkia Ijumaa:
Kwa ajili ya Amali za Kujiongezea uwezo wa Kushika Mimba na kupata Watoto.
Kwa ajili ya Kujikinga dhidi ya kupukutisha Mimba.
Kwa ajili ya kukubaliana makubaliano ya mikataba ya nyumba na ujenzi.

Saa ya Zohal katika Mchana wa siku ya Jumanne Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Ijumaa kuamkia Jumamosi:
Kwa ajili ya Amali za Kufanikisha Matibabu ya Upasuaji.
Kwa ajili ya Kujikinga dhidi ya Madhara ya Sumu, Mauaji na uvamizi.

Saa ya Zohal katika Mchana siku ya Jumatano Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili:
Kwa ajili ya Amali za kutibu mambo yanayohusiana na Akili na ufahamu.

Saa ya Zohal katika Mchana wa siku ya Alkhamis Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumapili kuamkia Jumatatu:
Kwa ajili ya Amali za Kujiongezea uwezo wa Ufahamu na Kiakili.
Kwa ajili ya Makubaliano kuhusiana na mikataba ya Majengo na uwekezaji wa ardhini.

Kwa Ajili ya kujiepusha na kuwakimbia wanaotaka kukusababishia Madhara.

Saa ya Zohal katika Mchana wa siku ya Ijumaa Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumatatu kuamkia Jumanne:
Haifai kufanya Amali yoyote ndani yake.

Saa ya Zohal katika Mchana wa siku ya Jumamosi Ambayo Usiku wake Hua ni sawa na Usiku wa Jumanne kuamka Jumatano:
Kwa ajili ya Kujikinga dhidi ya madhara ya Maadui.
Kwa ajili ya kujiongezea nguvu ya kimwili, kiuwezo na Kimamlaka.

Nyakati za Zohal na Mirikh hua hazifai kwa ajili ya Amali zinazohusiana na Watoto au mambo ya Mali na Uchumi.

SALA YA HAJA JUU YAKUFANIKISHA KILA JAMBO.

Ukitaka kusali Sala ya Haja ya kufanikisha kila Haja yako basi Utaamka katika Usiku wa kuamkia siku ya Ijumaa, kisha utatia udhu na kutia nia ya kusali Salat Al Hajjat ya rakaa 4 kisha utasali kwa mfumo ufuataoo:

Katika rakaa ya kwanza uatsoma Surat Al Fatiha mara moja na kisha utasoma aya 44 ya Surat Ghafir mara 100 ambayo ni:

(وَأُفَوِّضُ أَمْرِي إِلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ)

Rakaa ya 2 utasoma Surat A l Fatiha na aya 13 ya Surat As Safaat mara 100 ambayo ni:

(نَصْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ)

Rakaa ya 3 utasoma Surat Al Fatiha na aya 53 ya Surat Al Shuaraa mara 100 ambayo ni:

(أَلا إِلَى اللَّهِ تَصِيرُ الأُمُورُ)

Rakaa ya 4 utasoma Surat Al Fatiha na aya 1 ya Surat Fatih mara 100 ambayo ni:

(إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا)

Kisha baada ya salam utafanya istighfar mara 100 kwa kusema maneno yafuatayo:

(غفرانك ربنا واليك المصير)

Na kisha baada hapo utasjudu na utafanya istighfar mara 100 kwa kusema maneno yafuatayo

(استغفر الله وأتوب إليه)

Na kisha baada ya hapo utakua umemaliza Sala yako ya Hajja ya kila kitu, na kisha utamsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mara 7 na kisha utasoma Dua unayoitaka na kisha kisha utamsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam mara* 7 tena.

DUA YA AL HAYYU AL QAYYUM.

Mwenye kuisoma Dua hii mara elfu katika mchana au usiku na akashikamana na hayo na akaomba dua ifuatayo, atapata kila kheri, siri na baraka.

(ياحي ياقيوم يامحي أحي قلبي ورزقي وديني ودنياي اللهم انى اسالك ياحي قبل كل حي ياحيي بعد كل حي ياحي محي كل حي ياحي مميت كل حي ياحي يارازق كل حي ياحي لايشبهه حي أسالك بحياتك قبل كل حي وبحياتك التى تحي بها كل حي وبحياتك التى تمت بها كل حي ياحي ياقيوم ياذا الجلال والإكرام فرج كربي ونفس همي وغمي واجل صدأ قلبي واغن فاقتى يامن لا يخفاه حالى ولا تعجز مسألتى لا اله الا انت ياحي ياقيوم عجل لى مطالبي وبلوغ مأربي فقد دعوتك باسمك الذي نجا به من نجا وهلك به من هلك ياحي ياقيوم إحدى عشرة مرة فاستجبنا له ونجيناه من الغم الى المؤمنين وصل بجلالك على محمد وعلى اله وصحبه وسلم

MAJINA MATUKUFU YA ALLAH SUBHANAH WA TA'ALA NA NYAKATI ZAKE

﴿قُلِ ٱدْعُواْ ٱللَّهَ أَوِ ٱدْعُواْ ٱلرَّحْمَـٰنَ أَيّاً مَّا تَدْعُواْ فَلَهُ ٱلأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ وَلاَ تَجْهَرْ بِصَلاَتِكَ وَلاَ تُخَافِتْ بِهَا وَٱبْتَغِ بَيْنَ ذٰلِكَ سَبِيلاً﴾

Quli odAAoo Allaha awi odAAoo alrrahmana ayyan ma tadAAoo falahu al-asmao alhusna wala tajhar bisalatika wala tukhafit biha waibtaghi bayna dhalika sabeelan *(Surat Al Isra 17:110)*

Tafsir: ***Sema Muombe Allah au Muombe Mwingi wa Rehma, kwani vyovyote vile utakavyomuomba basi Majina mazuri Zaidi ni yenye kumilikiwa nae. Na usinyanyue sauti yako juu sana katika kuomba kwako na ipunguze na tumia baina ya njia hizo.***

Ambapo Majina hayo yanayojumuisha sifa zake Tukufu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni:

الله ، الرحمن ، الرحيم ، الملك ، القدوس ، السلام ، المؤمن ، المهيمن ، العزيز ، الجبار ، المتكبر ، الخالق ، البارئ ، المصور، الغفار ، القهار ، الوهاب ، الرزاق ، الفتاح ، العليم ، القابض ، الباسط ، الخافض ، الرافع ، المعز، المذل ، السميع ، البصير، الحكم ، العدل، اللطيف ، الخبير ، الحليم ، العظيم ، الغفور، الشكور ، العلي ، الكبير ، الحفيظ، المقيت ، الحسيب ، الجليل ، الكريم ، الرقيب، المجيب ، الواسع ، الحكيم، الودود ، المجيد ، الباعث ، الشهيد ، الحق ، الوكيل ، القوي ،

المتين، الولي ، الحميد ، المحصي ، المبدي ، المعيد ، المحيي ، المميت ، الحي ، القيوم، الواجد ، الماجد ، الواحد ، الأحد، الصمد ، القادر ، المقتدر ، المقدم ، المؤخر، الأول ، الآخر ، الظاهر، الباطن، الوالي ، المتعالي ، البر ، التواب ، المنتقم ، العفو، الرؤوف، مالك الملك ، ذو الجلال والإكرام ، المقسط ، الجامع ، الغني، المغني، المانع ، الضار النافع ، النور ، الهادي ، البديع ، الباقي ، الوارث ، الرشيد، الصبور.

Huwa Allahu Ldhii La Ilaha Illa Huwa Rahmani Rahim. Al Maliki Al Quddusu As Salamu Al Mu'minu Al Muhayminu Al Azizu Al Jabbaru Al Mutakabbiru Al Khaliku Al Bariu Al Musawwiru Al Ghaffaru Al Qahharu Al Wahhabu Ar Razzaku Al Fattahu Al Alimu Al Qabidhu Al Basitu Al Hafidhu Ar Rafiu Al Muizzu Al Mudhillu As Samiu Al Basiru Al Hakimu Al Adlu Al Latifu Al Khabiru Al Halimu Al Azimu Al Ghafuru Al Shakuru Al Aliyyu Al Kabiru Al Muqitu Al Hasibu Al Jalilu Al Karimu Ar Raqibu Al Mujibu Al Wasiu Al Hakimu Al Wadudu Al Majidu Al Baithu Al Shahid Al Khaqqu Al Wakkilu Al Qawiyyu Al Matinu Al Waliyyu Al Hamidu Al Muhsi Al Mubdiu Al Muidhu Al Muhyi Al Mumitu Al Hayyu Al Qayyumu Al Wajidu Al Majidu Al Wahidu Al Ahadu As Samadu Al Qadiru Al Muqtadiru Al Mukaddimu Al Muakhhiru Al Awwalu Al Akhiru Adh Dhahiru Al Batinu Al Wali Al Mutaali Al Barriu At Tawwabu Al Muntaqimu Al Afuwwu Ar Raufu Maliki ul Mulki Dhul Jalali Wal Ikramu Al Muqsitu Al Jamiu Al Ghaniyyu Al Mughni Al Maniu Ad Dharr An Nafiu An Nuru Al Hadi Al Badiu Al Baqi Al Warithu Ar Rashidu As Sabur.

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **‘Allah ana majina 99, 100 kasoro Moja na atakaeyahifadhi yote basi kwenye Moyo wake basi ataingia Peponi’***(Imam Bukhari)*

Lakini pia wanasema Wanazuoni kua: ‘**Yeyote yule atakaeyasoma Majina haya yote mara tu baada ya Sala ya Alfajir bila ya kunyanyuka katika sehemu uliyo Sali na bila ya kusungumza na mtu yeyote basi hatokutwa na dhara la aina yeyote wala hatofikwa na Mauti ya Ghafla ndani ya siku hio**.’

Mtu atakae yasoma mara 3 baada ya Salat Fajr kila siku basi atakua ni mwenye Ilm kubwa sana ni mwenye Ukaribu sana na *Allah Subhanah wa Ta’ala,* atakua anapendwa na *Allah Subhanah wa Ta’ala* na atakua sala kutokana na Adhabu ya Kaburi na Adhabu ya Moto wa *Jahannam na Allah Subhaanh wa Ta’ala* atamuingiza Peponi.

Mtu atakaeyasoma mara 7 baada ya *Salat Al Fajir* Kila siku basi atakua ni mwenye kutekelezewa mahitajio yake yote na *Allah Subhanah wa Ta’ala.*

Mtu atakaeyasoma mara 41 katika Usiku wa manane huku akiwa na nia ya kuomba Mema, kuondolewa Matatizo nakutekelezewa haja zake basi atafanikiwa maombi yake hayo.

Hivyo Tunapoangalia kuhusiana na *Asmau Al Husna* au Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* basi tunaona kua kama ilivyokua Qur’an kua ndani yake mna Shifau yaani Dawa au matibabu kwa walimwengu kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta’ala* katika Qur’an:

﴿وَنُنَزِّلُ مِنَ ٱلْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَآءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ وَلاَ يَزِيدُ ٱلظَّالِمِينَ إَلاَّ خَسَاراً﴾

Wanunazzilu mina alqur-ani ma huwa shifaon warahmatun lilmu/mineena wala yazeedu aldhdhalimiina illa khasaran *(Surat Al Isra 17:82)*

Tafsir: ***Na tumeiteremsha hii Qur'an ndani yake mkiwa na Tiba na Rehma kwa Walioamini, lakini kwa Madhalimu haiwanufaishi na chochote isipokua Hasara.***

Naam aya imetumia neno *Shifaun* ambalo ni lenye kutokana na neno *Shafa*. Na kwa kilugha basi neno *Shafa* hua ni lenye kumaanisha Kuponya, Kutibu, Kurudisha Afya, Kuridhisha, Kurudisha katika hali yake ya Asili au ya Kimaumbile ndio maana wenye Lugha yao hua wanasema *Shaf'ahu aAn Al Masalati* kumaanisha kua Amemuondolea Mashaka na kumridhisha Nafsi yake juu ya Jambo.

Ambapo anasema *Sultan al Mutakallimin Mujaddid ud Din* Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Ibn Al Husayn Al Taymi Al Bakri Al Tabaristan Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kuhusiana na ayah hii kua: '**Quran ni Tiba ya Kitabia, Kijamii, Kiroho na Kiafya pia. Na bila ya shaka baadhi ya Aya zake zimebainika kua ni Tibba ya Maradhi tofauti ya Kimwili'**

Basi na Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni Tiba pia ya matatizo mbalimbali kwani ni yenye uwezo mkubwa sana wa Kutuathiri sisi viumbe Kiafya, Kihisia, Kiufahamu, Kiakili na kimazingira ya Ulimwengu kwa ujumla, na hii nikwa sababu Majina haya hua ni yenye kumuwakilisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Nyoyo zetu na katika Maisha yetu kwa ujumla.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Hadith Al Qudsi kua: 'Hakika mimi siwezi kutosha kwenye Dunia, lakini nnaweza kutosha kwenye Moyo wa Mja wangu anaeniamini.'**

Na kama alivyosema mwenye *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua:

﴿ٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ ٱللَّهِ أَلاَ بِذِكْرِ ٱللَّهِ تَطْمَئِنُّ ٱلْقُلُوبُ﴾

Alladheena amanoo watatma-innu quloobuhum bidhikri Allahi ala bidhikri Allahi tatma-innu alquloobu*(Surat ArRad 13:28)*

Tafsir: ***Wale ambao ni walioamini na wakazituliza Nyoyo zao kutoka na kumkumbuka Allah Subhanah wa Ta'ala, Kwani kwa hakika kutokana na kumkumbuka Allah Subhanah wa Ta'ala basi Nyoyo hupata Utulivu.***

Hivyo katika Majina ya *Asmau ul Husna* basi ndani yake mna Tiba ya utatuzi wa matatizo mbali mbali ikiwemo ya Mwili ambapo nimuhimu kuyatumia katika nyakati zake na idadi yake kama inavyooneshwa kwenye jadweli ifuatayo:

MAJINA YA ISMU AL ADHIUMU KULINGANA NA NYAKATI NA IDADI YAKE

MAJINA MATUKUFU YA ALLAH SUBHANA WA TA'ALA KULINGANA NA NYAKATI ZAKE						
SIKU/SAA	SOMA MAJINA MATUKUFU HAYA KULINGANA NA WAKATI NA IDADI YAKE					
SHAMS	(131) ياسلام	(170) ياقدوس	(90) ياملك	(258) يا رحيم	(298) يا رحمن	(66) يا الله
	(812) ياخبير	(351) يارافع	(104) ياعدل	(117) يامعز	(213) ياباری	(731) ياخالق
	(550) يامقيت	(73) ياجليل	(998) ياحفيظ	(110) ياعلى	(1286) ياغفور	(88) ياحليم
	(744) يامقتدر	(47) ياوالى	(18) ياحى	(148) يامحصى	(573) ياباعث	(78) ياحكيم
	(256) يانور	(161) يامانع	(1060) ياغنى	(156) ياعفو	(37) ياأول	(305) ياقادر
	(68) ياحكم	(298) ياصبور	(514) يارشيد	(113) ياباقى	(20) ياهادى	(1098) ياذالجلال والاكرام
QAMAR	(256) يانور	(62) ياباطن	(20) ياودود	(78) ياحكيم	(302) يابصير	(336) يامصور
MIRIKH	(46) ياولى	(116) ياقوى	(770) يامذل	(306) ياقهار	(206) ياجبار	(94) ياعزيز
	(1001) ياضار	(630) يامنتقم	(13) يا احد	(801) ياآخر	(19) ياواحد	(490) يامميت
ATTARID	(1020) ياعظيم	(489) يافتاح	(212) يامالك الملك		(286) ياروف	(124) يامعيد
MUSHTARA	(232) ياكبير	(180) ياسميع	(903) ياقابض	(150) ياعليم	(662) يامتكبر	(145) يامهيمن
	(56) يامبدئ	(68) ياحميد	(66) ياوكيل	(319) ياشهيد	(78) ياحكيم	(55) يامجيب
	(114) ياجامع	(86) يابديع	(209) يامقسط	(409) ياتواب	(134) ياصمد	(156) ياقيوم
	(707) ياوارث					
ZUHRA	(129) يالطيف	(201) ياناقع	(72) ياباسط	(308) يارزاق	(1281) ياغفار	(136) يامؤمن
	(108) ياحق	(57) يامجيد	(312) يارقيب	(270) ياكريم	(80) ياحسيب	(526) ياشكور
	(48) ياماجد	(202) يابر	(14) ياواجد	(68) يامحيى	(66) ياوكيل	(500) يامتين
	(1100) يامغنى		(1481) ياخافض		(256) يانور	
ZOHAL	(57) يامجيد	(1106) ياظاهر	(184) يامقدم	(78) ياحكيم	(551) يامتعالى	(137) ياواسع
	(108) ياحق	(312) يارقيب	(270) ياكريم	(80) ياحسيب	(526) ياشكور	(846) يامؤخر
	(48) ياماجد	(202) يابر	(14) ياواجد	(68) يامحيى	(66) ياوكيل	(500) يامتين
	(201) ياناقع		(1100) يامغنى		(256) يانور	

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Na miongoni mwa Majina na Utatuzi wa maradhi hayo ni pamoja na:

Ya Samiu (uzito wa idadi yake 180) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Sikio.
Ya Jabbar (uzito wa idadi yake 206) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Uti wa Mgongo, Mifupa na Mishipa na Tezi ya Shingo(Goiter)
Ya Badiu (uzito wa idadi yake 86) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Nywele.
Ya Razzaq (uzito wa idadi yake 308) kwa Ajili ya kutibu Maradhi Mishipa ya Moyo,Mapafu,Tumbo.
Ya Raufu (uzito wa idadi yake 286) kwa Ajili ya kutibu Maradhi Kidole Tumbo,Magoti.
Ya Rafiu (uzito waidadi yake 351) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Miguu.
Ya Rashidu (uzito wa idadi yake 514) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Mafuta ya Mwili.
Ya Badiu (uzito wa idadi yake 86) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Nywele.
Ya Nur (uzito wa idadi yake 256) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Moyo.
Ya Nafiu (uzito wa idadi yake 201) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Tezi Dume na Ini.
Ya Latiif (uzito wa idadi yake 129) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Fuko la Uzazi.
Ya Kafii (uzito wa idadi yake 111) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Mishipa ya Damu ya Macho.
Ya Jallal (uzito wa idadi yake 73) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Saratani.
Ya Hafidhu (uzito wa idadi yake 989) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Msongo wa Mawazo.
Ya Hadi (uzito wa idadi yake 20) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Mkojo.
Ya Hayyu ya Qayyum (uzito wa idadi yake 174) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Figo.
Ya Bariu (uzito wa idadi yake 202) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Sukari.
Ya Ahad (uzito wa idadi yake 13) kwa Ajili ya kutibu Maradhi ya Kutafunwa na Nyoka unasoma mara 100.

MAJINA MATUKUFU YA ALLAH SUBHANAH WA TA'ALA,AMALI NA IDADI YAKE

Ya Allah (66) يا الله

Jina Tukufu la Allah ndio Jina linalojumuisha majine mengine yote Mtukufu na Sifa zote Tukufu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake ndani yake, na hivyo hakuna anaestahiki kuitwa kwa jina la Allah isipokua yeye, nani yeye pekee nde mwenye kustahiki kuabudiwa na kutukuzwa kwani ndie mmuumbaji na msimamizi wa Ulimwengu na kila kilichomo ndani yake.

Jina hili la Allah hua ni vizuri zaidi kulitumia katika wakati wa Shams, ambapo Mawalii hua ni wenye kulitamka jina hili mara 1000 katika siku ya Ijumaa.

Kutaka kukubalika na kutekelezeka kwa shida yako basi lisome mara 66. Na ukilisoma mara 200 katika siku ya Ijumaa huku ukiwa na Udhu basi utafanikisha haja yako.

Ya Rahmân (298) يا رحمن

Jina Tukufu la Al Rahman ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwingi wa Rehma na ni mwingi wa Kusamehe na kuwapenda na kuwapa hifadhi Viumbe wake wote.

Jina la Ya Rahman ni vizuri zaidi kulisoma katika wakati wa Shams.

Jina hili hua linatumika kwa kutibu Usahaulivu, na kama ukimsomea mtu aliekua Katili basi atakua mpole.

Na ukulisoma katika wakati wa Zuhra mara 298 huku ukiwa umewasha ubani basi utakua ni mwenye kupendwa na kila kiumbe atakaesikia harufu ya ubani huo.

Soma mara 100 kila baada ya Sala kwa ajili ya kua Wepesi wa Moyo nakua na ufahamu makini na mzuri.

Ya Rahim (258) يا رحيم
Jina Tukufu la Ya Rahim ni lenye Kumaanisha kua Allah Subhanah wa Ta'ala ni Mwingi wa Huruma na ni mwenye kuwalipa wale wenye kufanya mema kutokana na kufuata maamrisho yake.

Jina Ya Rahim ni vizuri kulisoma katika wakati wa Shams, na kama likisomewa kwa ajili ya Mwenye kufanya Maasi basi uasi wake Mtu huyo utatoweka, na ukilisoma kwenye Sijda mara 258 utafanikisha kutatua matatizo yako yote. Ukilindika kwa Zafarani na kisha ukamwagia maji yake kwenye shamba lako basi utapa mazao bora zaidi.

Soma jina hili mara 100 katika kila baada ya Sala kwa ajili ya kujiokoa na Matatizo na mitihani.

Soma mara 100 baada ya Salat Alfajr kwa ajili ya kupata Mapenzi na ukaribu kwa mtu umtake.

Ya Malik (90) ياملك
Jina Tukufu la Ya Malik ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwenye Mamlaka juu ya kila kitu.

Jina hili Ya Malik ni vizuri kulisoma katika wakati wa Shams na hua ni lenye kumpa Mamlaka mtu alisomae kulingana na Umiliki wa Kitu anachokitaka, na kulingana na uhuru juu ya kitu anachotaka kua huru nacho, na kuheshimika.

Kwa ajili ya Mali na utajiri basi soma mara 3 baada ya Sala ya Dhuhr Dua Ifuatayo*: Allahuma Antal Maliku Al Haqq al ladhii la ilaha illa anta, ya Allahu Ya Salam Ya Shafii ya Shafiyah Al Qluub*

Ya Quddus (170) ياقدوس
Jina Tukufu la Ya Quddus ni lenye Kumaanisha kua Allah Subhanah wa Ta'ala ni Mwenye Utukufu wa Ukamilifu juu ya Kila kitu.

Jina hili la Ya Quddus ni vizuri kulisoma katika wakati wa Shams pia na hua ni lenye kuficha Siri za kila anaependa kulisoma kiasi ya kua hakuna atakaekua na uwezo wa kufichua siri zake Isipokua *Allah Subanah wa Ta'ala* na pia hua ni lenye kumsababishia hali ya kupendwa na watu mtu anadumu nalo katika kulisoma.

Kwa mwenye matatizo ya wasiwasi na mashakil ya mawazo yanayozonga moyo na maumivu basi na atumie Jina hili. Ambalo humtanulia mtuhusika kifua na moyo kua huru kutokana na kila kitu.

Ya Salam (131) ياسلام
Jina Tukufu la Ya Salam ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwenye kusimami Usalama na Amani wa kila Kitu.

Hivyo ni vizuri kulisoma katika wakati wa Shams pia na hivyo hua ni lenye kukuhakikishia Usalama wako pale unapokua katika matatizo na kukuhakikishia usalama katika hatari za aina mbalimbali. Na kutibu maradhi mbali mbali pale unaposoma huku ukiwa umemkamata Kichwa Mgonjwa, na ukidumu nalo basi utakua na ilm kubwa sana ya mambo mbali mbali.

Ya Mu'min (136) يامؤمن

Jina Tukufu la Ya Mu'min ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwenye kuaminika pale unapomtegemea.

Jina la Ya Mu'min hua ni vizuri kulisoma katika wakati wa Zuhra na hivyo hua lenye kukuongezea Nuru ndani ya Moyo wako na kukusababishia kupata ushindi dhidi ya Maadui zako. Na kukuweka mbali na maadui wa Kijini na Watu.

Kua mbali na matamanio ya Nafsi basi soma jina hili mara 36.

Ya Muhaymin (145) يامهيمن

Jina Tukufu la Ya Muhaymin ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye Kuokoa kutokana na Matatizo mbalimbali kwani mwenye kudhibiti kila kitu.

Jina hili ni vizuri kulisoma katika wakati wa Mushtara na hua ni lenye uwezo wa kumpa ushindi yule alisomae dhidi ya maadui zake.

Likisomwa katika siku za Ukame basi hua ni lenye kusababisha Mvua kunyesha. Ulilisoma kila baada ya Sala basi utakua na Malaika maalum anaekulinda kutokana na madhara mbali mbali. Na hivyo pia hukufanya kua Mcha Mungu.

Ukiliandika Jina hili kwenye kitambaa cha Hariri kwa kutumia Zafarani na kisha ukikifukiza kwa Ambari, Misk na Sukari na kisha ukaweka chini ya mto wake kulala basi utaona yale mambo ambayo yatakayotokea baadae kwenye maishayako.

Ukitaka Mfanikio juu ya kila kitu kimaisha basi soma jina hili mara 5000 kwa mda wa siku 7 mfululizo.

Ukitaka utulivu wa Nafsi na Moyo basi tia udhu kisha elekea kibla na usome jina hili mara 115 na utapata utulivu mkubwa sana.

Ya Azîz (94) ياعزيز

Jina Tukufu la Ya Aziz ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwenye Utukufu Wa Hali ya juu n ani mwenye uwezo juu ya kila kitu.

Jina hili hua ni vizri kulisoma katika wakati wa Mirikh kwa ajili ya Kupata ushindi dhidi ya Maadui na kupata utukufu mbele ya Watu.

Ukilisoma mara 13 kila siku basi hukuongezea Kipato, ukilisoma mara 94 kila siku hukuongezea Ilmu. Na ukilisoma mara nyingi zaidi kila siku basi hukufungulia Moyo wako na kua na mawasiliano na viumbe wa ulimwengu wa Al Ghayb.

Ya Jabbar (206) ياجبار

Jina Tukufu la Ya Jabbar ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwenye uwezo mkubwa wa kinguvu dhidi ya kila kitu.

Jina hili ni vizuri kulisoma katika wakati wa Mirikh kwa ajili ya kufanikisha Kupata Ushindi dhidi ya maaduai na waliokudhulumu. Ukilisoma mara 21 tu kila siku basi utakua salama na maadui zako, na ukilisoma mara 21 asubuhi na jioni basi hutokutana na madhara yeyote ndani ya maisha yako. Na ukilisoma kwa mara nyingi zaid kwa mda wote basi maadui zako watatoweka.

Ya Mutakabbir (662) يامتكبر
Jina Tukufu la Ya Mutakkabir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye Uwezo wa kumiliki na kudhibiti kila kitu.

Jina hili ni vizuri kulisoma katika wakati wa Mushtara kama unataka kupata Mamlaka juu ya jambo husika.

Na kama ukiwa unataka kujaaliwa mtoto wa kiume basi unalisoma mara 662 katika usiku kabla ya kuingiliana na Mkeo. Ukilisoma mara 14 kabla ya kulala basi hutokua na ndoto za kutisha wala za kijinga, ukimsomea mtu anaejifanya Jabari basi ataadhirika mbele yako.

Ukimsomea Mtu ambae hataki kukusikiliza mara 3125 basi atakubaliana na wewe katika kila jambo lako na atakua mtiifu kwako kwa kila kitu.

Ukilisoma kabla ya kuanza kitu au jambo lako basi jambo hilo litakua na mafanikio.

Ya Khaliq (731) ياخالق
Jina Tukufu la Ya Khaliq ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuumba Kila kitu bila ya kutokana na kitu chochote, kwani kwake yeye kuumba kwake hua ni katika kusema tu: 'Kua' na hivyo hivyo kitu husika hua ni chenye kua tangu mwanzo wake hadi mwisho wake.

Jina hili ni vizuri kulifanyia kazi katika wakati wa Shams ambapo hua ni lenye kukupa Darja katika siku ya Malipo.

Na ukilisoma mara nyingi zaidi kila siku basi unaweza ukawapita watu usiotaka wakuone bila ya wao kukuona, na pia hukusafishia Moyo wako.

Ukilisoma kabla ya kulala basi utakua chini ya ulinzi wa Malaika hadi asubuhi.

Ya Bâriu (213) ياباري
Jina Tukufu la Ya Bariu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuumba vitu ambavyo vyenye kuendana na kufaana katika kuwepo kwake.

Jina hili ukilisoma katika wakati wa Shams hua ni lenye kukurahisishia mambo yako kutokana na kila kitu kua ni chenye kukunufaisha na kuendana zaidi na mahitajio yako. Ukimsomea mtoto wako mara 202 basi Mtoto huyo hua ni mwenye kuandamana na mafanikio katika kila hatu ya Maisha yake.

Kwa mwenye kutaka mtoto basi n afunge kwa mda wa siku 7 na katika kila siku anapofungua Funga yake basi na aseme Ya Khaliq, Ya Bariu Ya Musawwir mara 7.

Ya Musawwir (336) يامصور
Jina Tukufu la Ya Musawwir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuvipa maumbo mazuri vitu tofautia alivyoviumba.

Aambapo Jina hili hua ni vizuri kulitumia katika wakati wa Qamar kwa ajili ya kutafutia Mtoto kwa watu wasiokua na uwezo wa kupata Watoto.

Kwa ajili ya kupata Mtoto wa Kiume basi Mwanamke anatakiwa afunge mara 7 kuanzia ndani ya wiki ya mwanzoni ya Mwezi wa Kiarabu na kisha aandike Al Mussawwir kwa Zafarani huku akilitamka mara 12 na kisha ayatumie Maji hayo kwa ajii ya kufungulia Funga yake.

Na ukilisoma mara 12 kwa ajili ya kupata hifadhi kutoka kwa Maadui zako basi utawashinda maadui hao.

Kwa anaetaka kuingia kwenye ndoto ya mtu mwengine ili aonekane ndani ya usingizi wa mtu huyo basi na atie udhu kisha amfikirie Mtu huyo huku akiwa ni mwenye kulitamka jina hili mara 336.

Ya Ghaffar (1281) ياغفار
Jina Tukufu la Ya Ghafar ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni Mwenye Kusamehe Madhambi ya Waja wake na ni mwenye sifa ya kuwazuia kufanya Madhambi waja wake pale wanapokua ni wenye kudumu na Jina hili.

Jina hili ni vizuri kulitumia katika wakati wa Zuhra na hivyo Mtu mwenye kudumu nalo hua ni mwenye Kupata Ulinzi na kusamehewa kutokan na Wenye Mamlaka dhidi yake.

Ukilisoma mara 1281 katika kila siku ya Ijumaa basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakujaalia kua ni mwenye kufutiwa dhambi zako zote.

Ukitaka kupunguza hasira zako basi soma kwa wingi jina hili.

Al Ghaffuur (1286) الغفور
Ukilisoma Mara 70 kwa siku 3 mfululizo huku ukiwa unapulizia Mchanga uliouweka mkononi mwako na kisha ukaumwaga mchanga huo kwenye Pango au Kisima basi Siri zako zote hua ni zenye kuhifadhika.

Ya Qahhâr (306) ياقهار
Jina Tukufu la Ya Qahhar ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye Kua na ushindi dhidi ya kila kitu.

Hivyo uzuri Jina hili kulisoma katika wakati wa Mirikh kwa ajili ya kumzidi Mpinzani au Dhalim na ingawa ni jina linaloweza kuangamiza lakini halitakiwi kusomwa kwa ajili ya kuangamiza.

Ukilisoma mara 306 katika siku tatu za mwisho wa mwezi wa Kiarabu na kisha ukasoma Dua ifuatyo:

يا قاهر ياذو البطش الشديد انت الذي لا يوتق انتقامة

Yaaqaahiru Yaa Dh'al Batshish Shadeedi Antal Ladh'ee Laa Yootaqu Intiqaamuhu.

Tafsir: **Ewe Mwenye kua na ushindi juu ya kila kitu, wewe ni mwenye kudhibiti kikamilifu kila kitu, Wewe yule usiepatana pale unapoamua kutekeleza kisasi.**

Basi Maadui zako wataangamia.

Au soma ya Qahhar mara 100 kila baada ya Sala ya Alfajir kwa ajili ya kuwazidi nguvu maadui zako.

Ya Wahhab (14) ياوهاب

Jina Tukufu la Ya Wahhab ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Mwenye kuwapenda Waja wake na ni mwenye kuwamwagia kila ya aina ya Rehma katika Maisha yao.

Jina hili ukidumu nalo kwa kulisoma katika Sijda yako ya Mwisho ya kila sala yako mara 14 basi kamwe hutokua na matatizo yeyote, kwani utashushiwa rehma nyingi sana na *Allah Subhaanh wa Ta'ala* na kukutatulia matatizo yako yote.

Na ukilisoma mara 21 katika wakati wa Usiku wa manane huku ukiwa umenyanyua mikono yako juu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakuondolea matatizo yako.

Au nenda uani yaani kwenye sehemu isiyokua na paa katika wakati wa usiku na kisha sujudu mara 3 ambapo katika kila sijda utasoma jina hili mara 300. Na kisha omba maombi yako.

Kama una matatizo ya kiuchumi na kipato basi soma Ya Wahhab mara 100 baada ya Salat ya Rakaa mbili ya Usiku wa manane kwa mda wa siku 3 hadi 7.

Ya Razzaq (308) يارزاق

Jina Tukufu la Ya Razzaq ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuwapa Riziki waja wake wote wanaomuamini na wasiomuamini, wanaompenda na wasiompenda, anaowapenda na asiowapenda.

Jina hili ukilisoma katikawakati wa Zuhra basi hukufunglia milango ya Riziki yote kua wazi kwa ajili yako.

Ukilisoma kila baada ya Sala mara 11 basi utafunguliwa Milango mingi yenye kukuletea riziki ya kutosha sana kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ukilisoma mara 11 baada ya Salat Al fajr basi hukuongezea kipato na kukunawirishia makazi yako.

Au soma jina hili mara 10 huku ukiwa umeelekea kibla na kisha geukia kushoto kwako sema tena mara 10 kisha nyuma yako mara 10 na kulia kwako mara 10, ili kuongezewa na Baraka katika kipato.

Ya Fatah (489) يافتاح

Jina Tukufu la Ya Fattah ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kufungua Milango ya kheri na kufunga Milango ya Shari kwa Waja wake kutokana na uadilifu wake.

Jina hili ni zuri kulifanyia kazi katika wakati wa Attarid kwani hua ni lenye kukufungulia Milango ya kheri juu ya kila ukitakacho.

Ukilisoma mara 70 baada ya *Salat Al Fajr* huku ukiwa umeweka mkono wako kwenye kifua chako basi utaondokewa na mashakil yote ndani yake na kuongezewa kipato katika riziki yako.

Na ukilisoma mara 21 kila baada ya Sala basi Moyo wako utakua Msafi na usiokua na mazonge ya Kidunia.

Ya Alîm (150) ياعليم

Jina Tukufu la Ya Alimu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni Mwenye kujua juu ya kila kitu.

Jina hili linaposomwa kweye wakati wa Mushtara basi hua ni lenye uwezo wa kuwatawanya na kuwavunja nguvu Maadui wa anaelisoma, na hivyo hua ni lenye kuupa Moyo utulivu.

Ukilisoma mara 6 kila baada ya Sala basi hukufungulia Milango ya Siri zisizojulikana, na kukuongezea Ilm na Ufahamu na Hikma.

Au katika usikuwa siku ya Ijumaa basi sujudu kisha ndani yake soma jina hili mara 100.

Kama ukiwa na shida kubwa na hujua njia ya kuitatua basi toka nje kwenye sehemu isiokua na paa juu yake Sali Rakaa mbili za Sunna na baada ya hapo soma jina hili mara 1000.

Ya Qâbıidh (903) ياقابض
Jina Tukufu la Ya Qabiidh ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kukamata na kudhibiti kwa kubana.

Mwenye kulisoma Jina hili katika wakati wa Mushtara humtatulia matatizo yake na kumfanikishia malengo yake, na ukidumu nalo basi hukuletea watu wengi wenye manufaa nawe.

Ukilisoma mara 12 kila siku basi Utawadhibiti Maadui zako, na ukilisoma mara 903 basi utawashinda maadui zako

Ya Basit (72) ياباسط
Jina Tukufu la Ya Basit ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kukabidhi kwa wingi kwa yule amtakae.

Jina hili ukilisoma katika wakati wa Zuhra hufanikisha kukabidhiwa kwa uhuru wa yule aliedhibitiwa na kutokua na uhuru, na pia utakua na heshima na kupendwa.

Soma mara 72 kila siku baada ya Sala za Fardhi kisha jipulizie mikono yako usoni na kamwe hutokua ni mwenye kuadhirishwa na utakua ni mwenye kuridhika na kukinai.

Ya Hafidh (1481) ياخافض
Jina Tukufu la Ya Hafidh ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuhifadhi na kutoa Ulinzi.

Jina hili ukilisoma katika wakati wa Zuhra mara 989 basi hua ni lenye kukupa Ushindi na kukuhifadhi dhidi ya maadui zako nakukhifadhi na kila shari.

Ukimsomea mgonjwa mara 40 kwa mada wa siku 26 basi mgonjwa atapoa.

Kama mtu amekudhulumu na unataka hifadhi ya Allah Subhanah wa Taala kutokana nae basi hesabu idadi ya jina lake mtu huyo kiuzito na jumlisha na 1481 kisha soma jina la Hafidh kwa idadi hio huku ukiwa na nia ya kuhifadhiwa kutokana nae.

Au fungeni kwa siku 3 na kisha katika siku ya 4 someni jina hili mara 70000 na mtakua huru kutokana nae dhalimu husika.

Ya Rafi (351) يارافع

Jina Tukufu la Ya Rafiu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kunyanyua Darja ya yule amtakae.

Jina hili ukilisoma katika wakati wa Shams basi linakupandisha Darja na na heshima kwa wasiokuheshimu na wanaokudharau, na kukuzidishia kupendwa na watu ikiwemo ndani ya familia.

Na Ukilisoma mara 351 kila baada ya Salat Al Dhuhr basi litakupandisha Darja na ukilisoma mara 9 baada ya kila Sala basi utahifadhi kutokana na wanaotaka kukudhulumu.

Na ukilisoma katika kila usiku wa Jumapili na Alkhamis mara 100 basi utapanda darja, utaheshimika na kua na mali.

Ya Mu'izz (117) يامعز
Jina Tukufu la Ya Muiz ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Mwenye Kua na Utukufu na mwenye kutukuza.

Jina hili ukilisoma katika wakati wa Shams hukufungulia milango ya Furaha. Ukilisoma mara 124 basi utakua ni mwenye kukikumbuka kile ulichokisahau baada ya kukihifadhi na ukidimu alo basi litakuokoa na adhabu katika siku ya Malipo.

Ukilisoma mara 140 baada ya Sala ya Magharibi ya siku ya Jumapili na Alkhamis basi utaheshimika na kutokua na khofu dhidi ya mtu yeyote.

Ya Mudhil (770) يامذل
Jina Tukufu la Ya Mudhilu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuwadhalilisha Maadui zake pale anapotaka kutokana na hikma zake.

Ukilisoma Jina hili katika wakati wa Mirikh basi hukufanikishia kukuondoshea na kuwadhalilisha Maadui zako na ukilisoma mara 770 basi hukuondolea madeni yako.

Ili kujikwamua kutokana na madhara ya maadui zako na madhara yake basi soma Ya Mudhil mara 75 wakati ukiwa kwenye sijda na kisha muombe *Allah Subhanah wa Ta'ala* akuepushe na madhara ya maadui zako hao.

Ya Samî u(180) ياسميع
Jina Tukufu la Ya Samiu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kusikia kila kitu hadi kilichoo ndani ya Nyoyo za Viumbe wake.

Ukilitumia Jina hili akatika wakati wa Mushtara basi utakua na uwezo wa kufanikisha kila kitu unachokihitaji.

Kwa kutibu maumivu ya Sikio basi andika kwa Zafarani na Miski neno Samiu na kisha kosha kwa Mafuta ya Rose na kisha tia tone kwenye Masikio.

Ukiwa na tatizo basi soma ya Samiu mara 500 baada ya Salat Dhuhr kisha omba dua yako.

Ya Basîr (302) يابصير
Jina Tukufu la Ya Bassiru ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuona kila itu kinachoonekana na kisichoonekana kwa Viumbe wake.

Ukilisoma katika wakati wa Shams basi hua inanufaisha sana, na ukisoma katika wakatu wa Qamar basi hua ni zuri kwa ajili ya kuzidisha mapenzi katika Nyoyo.

Kutibu matatizo ya kutoona katika wakati wa usiku na maradhi ya macho basi soma mara 5 kila siku.

Kutapata mafanikio na ushindi katika jambo lako basi soma Ya Allahu ya Basiru mara 100 kabla ya Sala ya Ijumaa.

Kupata nguvu na nuru ya imni ndaniya moyo na utulivu basi sema mara 100 ya Allah Ya Basiru baada ya Sala ya Ijumaa

Ya Hakim (78) ياحكم

Jina Tukufu la Ya Hakim ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwingi wa Hikma na mwenye kutoa hukumu kwa Uadilifu katika kila kitu.

Hili ni vizuri kulisoma katika wakati wa Shams pia kwa ajili ya kutafuta Hukumu au malipo juu ya lile ulilodhulumiwa.

Ukitaka kujua nguvu za Al Ghayb kama zinakuunga mkono au zinapigana nawe basi lisome jina hili mara 78 kila baada ya sala ya Tahajjud, na pia ili kupata mafanikio juu ya kitu basi lisome Jinahili mara 78 Kila siku.

Ukitaka kupata mazao mazuri shambani basi andika Jina hili kwa Zafarani mara 78 na kisha maji yake yarushie rushie kwenye mimea ya Shambani mwako.

Kutaka kujua siri za mambo yaliyojificha katika kitu Fulani basi amka usiku wa kuamkia siku ya Alkhamis kisha soma jina hili mara 100 na utapata ufumbuzi wake.

Ya Adl (105) ياعدل

Jina Tukufu la Ya Adl ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Uadilifu katika kila kitu.

Ni vizuri kulisoma katika wakati wa Shams kwa ajili ya kukuzisha Bahati.

Na ukilisoma kila siku basi mambo yako yote hua yaliyonyooka kwani unarahisishiwa yote na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kufunguliwa milango ya siri juu ya kila kitu.

Kumfanda mtu kua muadilifu na msikivu na mtiifu kwako basi anadikaneno Adl kwenye mkate kisha mpe ale.

Ya Latîf (129) يالطيف

Jina Tukufu la Ya Latif ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua na Upole katika kila kitu chake.

Ni vizuri kulisoma katika wakati wa Zuhra kwa ajili kufanikisha Kila jambo unalolitamani lenye Kheri ndani yake.

Na ukilisoma mara 129 katika kila Siku ya Jumatatu basi matatizo yako yote huondoka na utakua si mtu mwenye kuishi katika Maisha yenye Mitihani.

Soma jina hili mara 133 kwa kujiongezea kipato, au baada ya sala ya rakaa mbili ya hajat basi lisome mara 11 na utakwamuka kutoka kwenye mitihani ya kipato na kiuchumi.

Ya Khabîr (812) ياخبير

Jina Tukufu la Ya Khabir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye Habari juu ya kila kitu kilichokua wazi na kilichofikichikana.

Hili ni Jina ambalo linatumika kwaajili ya kupata Habari juu ya kitu, na hua linatumika katika wakati wa Shams, na kama ikiwa ni kwa ajili ya mtu basi kama ni mwanamme hua ni katika wakati wa Shams na kama ni mwanamke basi hua ni katika wakati wa Qamar.

Ili kutaka kujua yale yanayoendelea ambayo huyajui basi soma jina hili mara 812 kabla ya kulala na utaona kila kitu usingizini. Na kama ukilisoma mara 11 ndani ya Rakaa ya Mwisho ya Sala kwa mda wa Wiki moja basi utakua ni mwenye kua na habari juu jambo lenye manufaa nawe na namna ya kulifanikisha jambo husika.

Ukitaka kuachana na mambo maovu yasiyoachika basi soma jina hili mara kwa mara.

Al Khaliis (721) الخالص

Ukilisoma mara 721 basi utakua ni mwenye kujua kuhusiana na bashirio jema la Kaburini baada ya kufariki kwako.

Ukishikamana nalo kila siku kulisoma basi Utaishi Maisha yenye Ikhlasi hadi mwishoni mwa uhai wako.

Ya Halîm (88) ياحليم

Jina Tukufu la Ya Halim ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala ni* mwenye sifa Tukufu ya kua na upole na Utaratibu katika kutekeleza mambo yake pale asipotaka kutumia nguvu.

Jina hili likisomwa katika wakati wa Shams hua ni lenye kumsababishia Maiti Muumini kusitishiwa Adhabu ya Kaburi.

Na likisomwa katika wakati wa Asubuhi ya siku basi hua ni lenye kuwasababishia wenye kutaka kusababisha matatizo na dhulma kutokua na nguvu wala uwezo wowote wa kufanya wayatakayo. Kwani Nabii Musa alilitumia Jina hili pale alipoiingia kwenye ukumbi wa Fir'awn.

Kufanikisha kazi zako za mikono na kuzijaza baraka basi andika Jina hili kwa Zafarani na kisha likoshe kwa maji safi kisha tumia maji hayo kwa ajili ya kusafishia zana zako unazotumia katika kazi zako.

Kwa ajili ya kumrudisha mtu umpendae kwenye mapenzi baada ya kutoendelea kutapena kua nawe basi chukua chakula kita kisha kisomee jina hili na kish amtu husika ale na mapenzi yatarudi upya.

Ukiyasomea maji jina hili na kisha ukaymwaga kwenye mti basi mti huo hautoathiriwa na wadudu waharibifu.

Ya Adhim (1020) ياعظيم

Jina Tukufu la Ya Adhim ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua na Sifa Bora na tukufu kuliko zote.

Likisomwa jina hili katika wakati wa Attarid basi humjaalia msomaji kua ni mwenye kuogopewa na maadui zake na kuonekana kua ni mwenye darja ya upekee.

Ukilisoma mara 100 asubuhi basi utakau salam akutkana na maadui zako na utapanda darja na kupendwa zaidi.

Ya Ghafûr (1286) ياغفور
Jina Tukufu la Ya Ghafur ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kusamehe Kila kitu.

Ukilisoma katika wakati wa Shams basi hua ni sababu ya kusamehewa kila kitu na *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Ukitaka kuhifadhi Siri zako dhidi ya Maadui zako na watu wengineo basi somea Ya Ghafur mara 70 kwenye gao la mchanga au kokoto kwa siku 3 na kisha litumbukize kisimani au kwenye pango au shimo kubwa.

Kuondoa na kufuta Mawazo juu ya kitu au Mtu aliekugana akilini au Moyoni basi soma Jina hili mara 1286.

Ya Shakur (526) ياشكور
Jina Tukufu la Ya Shakur ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kuonesha shukrani kwa waja wake nakuwaridhia kutokana na utiifu wao juu yake.

Ukilisoma Jina hili katika wakati wa Shams na Attarid basi hukufanikishia mambo yako mbele ya wenye Mamlaka juu yako.

Kutiba maradhi ya macho pia yasomee maji Jina hili mara 526 na kisha nawia uso maji hayo.

Ukiyasomea maji jina hili kwa mara 41 na kisha ukanawa uso basi utapunguza uzito wa matatizo uliomo ndani ya moyo wako na ndani ya maisha yako.

Ya Aliyyu (110) ياعلى
Jina Tukufu la Ya Aliyyu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Cheo na Darja ya Juu Kabisa.

Ukilisoma katika wakati wa Shams basi bila ya shaka utapanda Darja. Kwani ni wenye Mamlaka ndio Uradi wao. Na ukilisoma katika wakati wa Zuhra basi utakua na ugomvi na Wanawake.

Ukiliandika Jina hili kwenye Karatasi na kukaa nalo kwa mda wa masaa 24 basi hukuongezea mafanikio katika Maisha yako.

Ukilisoma mara 41 basi utapungukiwa na uzito wa matatizo yako na utakua na usalama.

Ya Fardan 284 الفرد
Kuwafanya Watu wasahau kuhusiana nawe kutokana na kuwasitisha kukuzungumzia wewe na kuwafunga midomo basi soma jina hili mara 284 Kila siku.

Ya Kabir (232) ياكبير

Jina Tukufu la Ya Kabir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuana Ukubwa mkubwa sana kuliko kitu chochote.

Na ukilisoma katika wakati wa Mushtara basi yeyote yule anaoneka kua ni mwenye uwezo wa kinguvu dhidi yako hua ni mwenye kua chini zaidi yako na hivyo kama una matakwa yako basi hukubalika mbele ya wenye Mamlaka.

Na ukikisomea chakula au kinywaji mara 232 au 1250 na kisha kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mara 11 na ukampa mtu akala au kunywa basi mtu huyo atakua anakupenda zaidi.

Jina hili linatumika pia kwa jili ya kutibu sehemu ya mwili iliyoungua moto.

Ya Hafidh (998) ياحفيظ

Jina Tukufu la Ya Hafidh ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuhifadhi na kukipa usalama kila kiti kutokana na matatizo.

Likisomwa katika wakati wa Shams kwa Mgonjwa basi Mgonjwa atapata hifadhi ya afya yake. Ukilisoma kila mara basi utakua na Ujasiri mkubwa sana na kukuondolea kila aina ya matatizo.

Kujikinga na Matatzo basi som ajina hili mara 16 kila siku.

Ya Muqît (550) يامقيت

Jina Tukufu la Ya Muqiit ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kunawirisha kila kitu.

Likisomwa katika wakati wa Shams basi hua ni lenye kunawirisha Riziki ya msomaji na kila kitu chake hunawirika.

Ukidumu nalo kulisoma Jina hili kila siku basi hu ana hali ya kutoonekana na wale usiotaka wakuone hata kama ikiwa wanakuangalia wakati unapita mbele yao.

Mwenye tabia ya kutkanana kutumia maneno mabaya basi chukua maji kisha yasomee jina hili mara 100 na kisha mpe anywe na atabadilika.

Na kwa ajili ya kutekelezeka shida yako basi yasomee maji jina hili mara 7 kisha yanywe.

Ya Hasîb (80) ياحسيب

Jina Tukufu la Ya Hasib ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kuweka hesabu na kulipa juu ya kila kitu.

Likisomwa katika wakati wa Zuhra basi utapatikana uwezo wa msomaji kua ni mwenye kuwaathiri wengi sana katika mambo yake na atakua na umaarufu.

Ukilisoma mara 80 kila siku kuanzia siku ya Alkhamis kwa mda wa Wiki 7 basi hukutekelezea mambo yako yote magumu kwa kuyarahisisha.

Na ukilisoma mara 80 katika alfajiri ya siku ambayo unatakiwa kuhojiwa au kuchunguzwa basi utatoka salama kwenye mahojiano hayo.

Ya Jalil (73) ياجليل

Jina Tukufu la Ya Jalil ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Ukubwa wa Mkubwa sana.

Ukisoma katika wakati wa Shams basi utakua na uwezo wa kuwavunja moyo maadui zako. Na pia hukupatia heshima katika jamii.

Ya Karim (270) ياكريم.
Jina Tukufu la Ya Karim ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Ukarimu katika kila kitu usiokua na mwisho.

Ukilisoma katika wakati wa Zuhra kwa wafanya biashara basi litakuongezea faida katika mambo yako. Kwa Wanawake pia, ama kwa Wanaume basi ni katika wakati wa Mushtara. Na ukidumu nalo katika wakati wa Zuhra basi hutokua na Matatizo yeyote.

Ukilisoma kabla ya kulala basi Malaika hukushukia na kukuombea Maghfira usiku kucha hadi utakapoamka.

Ukilisoma mara 9 kila siku baada ya Sala basi utakua na darja na heshima katika Jamii.

Ya Raqîb (312) يارقيب
Jina Tukufu la Ya Raqib ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuona na kuangalia na kudhibiti kila kitu.

Likisomwa katika wakati wa Zuhra basi huleta na kumpa furaha katika familia ya yule anaesoma.

Ukichukua mafuta ya aina yeyote unayoweza kupaka mwilina kisha ukayasomea Jina hili basi yatakua na uwezo wa kutibu maradhi ya Ngozi.

Na kama kuna kitu kimepotea basi ukisoma Jina hili kwa idadi yake basi kitu hicho kitaonekana.

Soma jina hili kila sikua mara 7 kwa ajili ya kupata ulinzi wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwako, kwa familia yako na mali zako.

Ya Mujîb (55) يامجيب
Jina Tukufu la Ya Mujib ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kujibu pale anapooombwa na Waja wake wanaomuamini.

Unapodumu nalo Jina hili katika wakati wa Mushtara basi utafanikisha malengo yako juu ya kila kitu, na penda kulitumia jina hili katika kila dua ili kusisitiza kujibwa Dua yako.

Ukilisoma mara 55 baada ya Salat Al Hajjat hua ni lenye kusitisha masengenyo na mazulio kutoka kwa maadui zako kwa kuwaziba maadui hao midomo yao.

Ya Wâsi '(137) ياواسع
Jina Tukufu la Ya Wasi' ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye Usamehevu, Rehma zenye kunika kila kitu.

Ukilitumia katika wakati wa Zuhra hukuondolewa Huzuni na Matatizo.

Kwa Mtu alietafunwa na Nge msomee Jina hili mara 11 hukua ukimsugulia katika sehemu aliyotafunwa.

Ya Hakîm (78) ياحكيم
Jina Tukufu la Ya Hakim ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye wingi wa Hikma.

Mwenye kulisoma Jina hili katika wakati wa Shams basi hua ni mwenye kuongezewa Hikma na Ilm kubwa sana, akisomewa Mgonjwa basi hua ni mwenye kupona, likisomwa katika wakati wa Zohal na Qamar basi hua ni lenye kukupa mamlaka ya kuwadhibiti Wanawake na kwa upande wa kuwadhbiti Wanaume basi ni katika wakati wa Mushtara.

Jina hili hua linatumika pia kwa ajili ya kukabiliana na matatizo na kupata ufumbuzi wa matatizo hayo.

Ya Wadud (20) ياودود
Jina Tukufu la Ya Wadud ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Mwenye Mapenzi makubwa sana kwa Waja wake wampendao.

Ukilisoma katika wakati wa Qamar basi utakua na uwezo wa kuwaathiri Wanawake, na katika wakati wa Shams basi utakua unawaathiri Wanaume.

Kuondoa tofauti na chuki baina ya watu basi kisomee chakula au kinywaji jina hili mara 20 na kisha waachie wahusika wale.

Ya Majid (57) يامجيد
Jina Tukufu la Ya Majid ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kua na Heshima itokanayo na Ushindi.

Ukilisoma mara kwa mara basi Maombi yako hua ni yenye kukubalika.

Kupatanisha na kuongeza mapenzi baina ya watu basi andika jina hili kwa Zafarani na kisha likoshe kwa maji na kisha maji hayo wape wahusika wanywe.

Au kisomee chakula kwa jina hili mara 1000 na kisha wape.

Ya Bâ'ith (573) ياباعث
Jina Tukufu la Ya Baith ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kuana Uwezowa Kufufua waliokufa katika siku ya Malipo.

Ukilisoma katika wakati wa Shams basi hukufufulia kila kitu chako kilichokufa kiuchumi na kukupatia mafanikio juu yake.

Ukilisoma mara 573 kabla ya kulala basi hukuogezea ufahamu; na ukilisoma mara 100 kabla ya kulala na kisha ukajipangusia kifuani basi moyo wako huimarika Kiimani na Kielimu na ukimsomea mtu asiekua na utulivu wa kihisia na kiakili basi mtu huyo hutulia.

Lisome jina hili mara 7070 kwa ajili ya kujisafisha jina lako baada ya kupakwa matope na kusingiziwa mambo maovu.

Ya Şhahid (319) ياشهيد
Jina Tukufu la Ya Shahid ni lenye Kumaanisha *kua Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kushuhudia juu ya kila kitu.

Ni vizuri kulitumia katika wakati wa Mushtara kwa ajili ya Kumdhibiti Adui yako.

Msomee mtu mkaidi mara 21 huku ukiwa ni mwenye kumuwekea mkono wako kwenye paji lake la uso.

Kama kuna mtu au kitu kimepota basi chukua karatasi kisha andika jina hili kwenye pembe nne za Kartasi hio na kisha katikati andika Jina la Mtu au kitu husika na kisha lala uamke usiku wa manane na kisha chukua kartasi hio na kusoma Jina hili mara 319, basi kitu hicho au mtu huyo ataonekana.

Ya Haqqi (108) ياحق
Jina Tukufu la Ya Haqqi ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Mwenye kusimamia haki.

Ukilisoma katika wakati wa Shams hua ni lenye kukusimamia Haki zako na hazitopotea. Na katika wakati wa Zuhra hukuongezea Mapenzi.

Ya Wakil (66) ياوكيل
Jina Tukufu la Ya Wakil ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kusimamia kila Mtu anaedhulumiwa na ni mwenye kuaminika.

Kwa Mwanamke Ukilisoma katika wakati wa Zuhra basi hukufanikishia mahusiano yako, na kwa Mwanamme ukilisoma katika wakati wa Mushtara hukufanikishia mahusiano yako. Na katika wakati wa Shams hukusimamia mambo yako, kwani jina hili ni kwa ajili ya maombi yote.

Ya Qawîyy (117) ياقوى
Jina Tukufu la Ya Qawwiy ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua na Nguvu na uwezo juu ya kila kitu.

Ukilisoma katika wakati wa Mirikh basi litakupatia Ushindi katika kila kitu. Jina hili ndio lililotumiwa katika Utekwaji wa Mji wa Istanbul kutoka kwenye mikono ya Warumi na Utawala wa Ottoman Empire.

Ukilisomea kwenye punje 1000 za chakula mara 117 an kisha ukawarushia ndege punje hizo na wakala basi hatari zote zinazokukabili zitatoweka.

Ukitana kua na Taqwa na Imani ya hali ya juu basi lisome jina hili mara 116.

Ya Matinu (500) يامتين
Jina Tukufu la Ya Matinu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kutokua na mpinzani katika kila kitu.

Hili ni vizuri kulisoma katika wakati wa Zuhra ili kufanikisha mambo yako. Na ukilisoma katika wakati wa kabla ya kuingiliana na Mke wako au Mume wako basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakujaalieni Kizazi cha Wacha Mungu.

Soma jina hili kwa ajili ya kuyateketeza matatizo yako, na ukilosma mara 500kwa ajili ya kumuangamiza Adui na uadui wake na kujiondolea matatizo ndaniya Nafsi yako.

Ya Walii (46) ياولى

Jina Tukufu la Ya Walii ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni msaidizi wa wale Marafiki zake wanaompenda nae akawapenda.

Kwa wenye matatizo na Wake zao ni vizuri kulisoma hili katika wakati wa Mirikh na Mke atakua ni mwenye kutulia na kua na usikivu kwa Mume.

Ukitaka kupata muongozo kwenye Ndoto kuhusiana na jambo usilolijua basi Tia Udhu kisha Sali rakaa 2 na kisha soma Jina hili mara 46 huku ukiwa unalifikiria jambo hilo kish alala na utapata ufafanuzi.

Msomee mtu mwenye tabia chafu na atakua ni mwenye kubadilika

Kupata ufumbuzi wa Jambo au ukutatua tatizo basi soma jina hili mara 46 katika usiku wa Ijumaa.

Ya Hamid (68) ياحميد

Jina Tukufu la Ya Hamid ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kustahiki Kushukuriwa.

Likisomwa katika wakati wa Mushtara basi hua ndio njia ya kumbadilisha mtu kutokana na tabia mbovu, humuongezea Mtu Maisha, Humfanya kua mcha Mungu na kumtatulia matatizo yake yote.

Andika jina hili kwa zafarani kwenye kikombe kisha kunywa maji yake kwa ajili ya kua na wepesi wa kauli.

Ya Muhsî (148) يامحصى

Jina Tukufu la Ya Muhsi ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya ni mwenye kujua hesabu juu ya kila kitu.

Likisomwa katika wakati wa Shams basi huboresha Ufahamu na akili na huondoa usahaulivu.

Ukilisoma mara kwa mara basi Maadui zako watajisalimisha kwako.

Tamka jina hili mara 100 kila siku kwa ajili ya kupata afueni katika siku ya malipo.

Ukilisoma mara 148 kila siku basi utakua na ufahamu mkubwa sana.

Ya Mubdî (56) يامبدئ

Jina Tukufu la Ya Mubdi ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni Mwenye kuanzisha kila kitu Ulimwenguni.

Ukilisoma katika wakati wa Mushtara basi utakua ni mwenye kuoneshwa majibu ya yale unayoyauliza ndani ya ndoto. Na ukilisoma kwa mwanamke mja mzito anaepukutisha Mimba basi litazuia kadhia hio.

Ya Mu'îd (124) يامعيد

Jina Tukufu la Ya Muid ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kuhuisha baada ya Kufisha.

Ukilisoma katika wakati wa Attarid, basi kilichopotea kitaoonekana na kilichokimbia kitarudi.

Ukimsomea mtu mwenye kutaka kuingia hatarinibasi atasalimika kutokana nalo.

Unapokua huna maamuzi basi tumia jina hili na kisha utakua ni mwenyekua na maamzui juu ya nini cha kufanya katika hali husika.

Mwanamke mja mzito akilisoma jina hili huku akiwa ni mwenye kujipapasa tumbo lake kwa mkono wake wa kulia.

Ya Muhyî (68) يامحيى

Jina Tukufu la Ya Muhyi ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Mwenye kuvipa Uhai viumbe.

Katika wakati wa Zuhra kwa aliefungwa kwa kuonewa na akisoma basi atatoka kizuizini.

Ukiwa na matatizo basi lirudie Jina hili mara 7 kila siku na yatatatuka.

Lisome mara 68 kwa ajili ya kutibu maradhi sugu.

Ya Mumît (490) يامميت

Jina Tukufu la Ya Mumit ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya Kufisha Viumbe katika wakati wake unapowadia.

Litakaposomwa katika wakati wa Mirikh basi wenye kufanya maovu dhidi ya msomaji watatoweka.

Na inapotokea kua Waislam wanadhulumiwa na kuvunjiwa haki zao na mtu ambae ni Kafiri basi likisomwa jina hili mara 1570 kwa mda wa siku 40 mfululizo basi Kafiri atakumbwa na balaa na atafariki.

Au kila unapolala basi soma jina hili huku ukijipangusia mwilini mwako kuanzia kifuani kwa ajili ya kua na Moyo safi na kuwaangamiza maaduia zako.

Ya Hayy (18) ياحى

Jina Tukufu la Ya Hayy ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua na Uhai wa Milele.

Iikisomwa katika wakati wa Shams basi mgonjwa anaesomewa atapona.

Ya Hayyu ya Qayyum yakisomwa Pamoja mara 174 kila siku kwa mtu aliefungwa kwa kusingiziwa basi anaesoma ataachiwa, na ukidumu nalo basi utakua kwenye njia iliyonyooka.

Ya Qayyûm (156) ياقيوم

Jina Tukufu la Ya Qayyum ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni msimamizi wa kila kitu.

Likisomwa katika wakati wa Mushtara basi anaesoma atadhihirishiwa ya Ulimwengu wa dhahir na wa Ghayb.

Ukilisoma kila siku baada ya sala ya asubuhi mara 156 kwa ajili ya kupata ukaribu kwa mtu umtakae au watu uwatakao basi utafanikiwa.

Ya Wujud (14) ياواجد,
Jina Tukufu la Ya Wujud ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kujitosheleza anafanya kile anachotaka katika wakati autakao bila ya kuhitajji chochote.

Likisomwa katika wakati wa Zuhra basi hunawirisha Nyoyo.

Ya Majid (48) ياماجد
Jina Tukufu la Ya Majid ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Ushindi na Utukufu.

Likitumiwa katika wakati wa Zuhra basi msomaji atapata Furaha ya kudumu.

Kutibu Kifafa basi Funga katika siku za mwezi 13,14, na 15 na kisha lisome jina hili mara 1000 kila baada kuftari.

Ukilisoma kila siku mara 465 asubuhi na jioni basi utakua ni mwenye kukubalika na kufahamika kutokana na unayoyasema katika jamii.

Ya Wahid (19) ياواحد
Jina Tukufu la Ya Wahid ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa asiehitaji Mwenzake.

Likisomwa katika wakati wa Mirikh basi Mtu aliemuacha mwenzake atarudi.

Jina hili linatumika pia kwa ajili kuleta umoja na mapenzi katika familia ukilisoma mara kwa mara.

Na ukilisoma mara 1000 wakati ukiwa peke yako basi utaondokewa na khofu.

Ya Ahad (13) يا احد
Jina Tukufu la Ya Ahad ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua na Umoja wa Pekee.

Likisomwa katika wakati wa Mirikh basi Nafsi ya Mtu husika itakua haina kitu ndani yake isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Likisomwa mara 100 kwa Mtu alaietafunwa na Nyoka mara 100, hua ni Tiba tosha. Atakaelisoma mara 1000 akiwa peke yake basi hua ni mwenye kuzungukwa na Malaika watakaomuombea Dua. Na kua na ukaribu na watu na kupendwa basi linatakiwa kusomwa kila wakati.

Ya Qabidhu (904) (يا قابض)
Jina Tukufu la Ya Qabidh ni lenye kumaanisha kua Allah Subhanah wa Ta'ala ni mwenye Hikma yenye kusababisha Kuzuia Kitu kwa namna atakavyo na kwa wakati atakao.

Likisomwa mara 904 kwa kila siku ndani ya siku 4 kwa nia ya kutaka mtu aliekukosea arudi kwa kukuomba msamaha basi mtu huyo atarudi kwako na kuomba msamaha.

Ukilisoma mara 904 basi utakua salama utokana na maadui zako.

Ya Samad (134) ياصمد
Jina Tukufu la Ya Samad ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Kila kitu kinamhitaji yeye na yeye hahitaji chochote.

Likisomwa katika wakati wa Mushtara basi mahitaji hutekelezeka.

Kutibu maradhi ya Tumbo soma jina hili huku ukipapasa sehemu inayouma.

Soma jina hili mara 115 wakati ukiwa kwenye Sijda kwa ajili ya kuwaangamiza maadui zako.

Ukilisoma mara 1000 basi utakua na ilm juu ya yale yasiyoonekana.

Ya Qadir (305) ياقادر
Jina Tukufu la Ya Qadir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kau na uwezo wa kufanya na kukadiria chochote.

Likisomwa katika wakati wa Shams basi hufanikisha kila kitu.

Kuwazidi nguvu Maadui zako basi lisome jina hili katika Jumatano ya Mwisho ya Mwezi wa Kiarabu mara 305.

Ukilisoma jina hili katika wakati w akutia udhu kwa kukisomea kila kiugo chako basi hakuna atakaeweza kukudhuru.

Ukiwa na matatizo basi lisome mara 41 kwa ajili ya kuepuka matatizo na madhara na mara 305 kwa ajili ya kujibiwa hisia zisizopokelewa.

Ya Muqtadir (744) يامقتدر
Jina Tukufu la Ya Muqtadir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kua na Mamlaka na uwezo wa kufanya kama atakavyo.

Likisomwa katika wakati wa Shams basi humpatia mtu Heshima na darja. Likisomwa mara 15 baada ya kuamka kabla ya kuzunguzma na mtu yeyote basi hutekelezeka shida zao zote.

Kama akisomewa Mtu aliefariki kwa idadi kubwa zaidi basi Mtu huyo hua ni mwenye kupandishwa darja na *Allah Subhaanh wa Ta'ala* na kuondolewa adhabu ya Kaburi.

Ya Muqaddim (184) يامقدم
Jina Tukufu la Ya Muqadim ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kusimamia na kusanzisha Kile akitakacho.

Likisomwa katika wakati wa Zohal, basi hufanikisha Mamlaka na cheo mbele ya watu.

Likisomewa kwenye gilasi ya maji au kinywaji kwa ajili ya kupatanisha Watu na kisha wakapewa kinywaji hicho basi watakua ni wenye kupendana.

Na kama likisomwa kwenye sehemu yenye Vita basi sehemu ya ardhi husika hua salama kutokana maafa mabaya ya vita.

Likisomewa kwenye Gilasi ya Kinywaji na kisha kinywaji hicho akapewa mtu na kanywa basi utaanza kuonekana mvutano wa maridhiano na mapenzi baina ya msomaji na aliekunywa kinywaji hicho.

Unaweza kulisoma hili kwa ajili ya kurudisha mambo au vitu kua kama vilivyokua katika hali yake hapo kabla.

Ya Mu'akhir (846) ياموءخر
Jina Tukufu la Ya Muakhir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kau ni mwenye kuchelewesha kila akitakacho na kutanguliza akitakacho.

Likisomwa katika wakati wa Zohal hufanikisha mambo yote.

Likisomewa kwenye Gilasi ya Kinywaji na kisha kinywaji hicho akapewa mtu na kanywa basi utaanza kuonekana mvutano wa maridhiano na mapenzi baina ya msomaji na aliekunywa kinywaji hicho.

Ukilisoma jina hili mara 846 kisha ukatubu kwa makosa yako basi toba yako hua ni yenye kukubaliwa.

Ukilisoma mara 144 kila siku baada ya Salat Al Fajr basi kwa mda wa siku 7 kwa ajili ya kumzuia dhalim kuingia madarakani basi utafanikiwa.

Ya Awwal (37) يااول
Jina Tukufu la Ya Awwal ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kua ndie wa Mwanzo wa kila kitu.

Likisomwa katika wakati wa Shams hufanikisha kila kinachohitajika. Na ukidumu nalo hukusababishia Ukarimu wa watu juu yako.

Ukilisoma mara 40 katika siku ya Al Khamis usiku basi shida zako hutatulika

Ya Akhir (801) ياآخر
Jina Tukufu la Ya Akhir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa kua yeye ndie wa Mwisho.

Likisomwa katika wakati wa Mirikh basi huhilikisha maadui wote, na kukutia ari baada ya kuvunjika Moyo.

Ukilisoma mara 1000 katika siku ya Ijumaa basi riziki huongezeka na dhambi zako hufutika.

Ya Dhahir (1106) ياظاهر
Jina Tukufu la Ya Dhahir ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa ya kuoneka Dhahiri kutokaaana na Dalili zake.

Likisomwa katika wakati wa Zohal kwa ajili ya mwenye hasira basi humuondolea mtu hasira zote na kisasi.

Ya Bâtınu (62) ياباطن
Jina Tukufu la Ya Batin ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kutofahamika akilini kutokana na kufichikana kwake na kutoonekana.

Kama likisomwa kwenye wakati wa Qamar basi hua ni lenye kufungua Nyoyo, na kuhifadhi siri za anaedumu nalo.

Ukilisoma mara 22 kwa ajili ya kutaka kujua kuhusiana na ukweli wa mambo basi utakudhihirikia ukweli huo.

Kama una tatizo kubwa linalohitaji kutatuliwa basi Sali Salat Al Hajjat basi litatatulika kwa kusema *Huwwa Al Awwalu wa Al Akhiru wa Al Dhahiru wa al Batinu wahuwa aAla Kulli Shay-in Qadir* mara 100.

Ya Waliy (47) ياوالى
Jina Tukufu la Ya Waaliy ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kusimamia kila kitu katika viumbe wake pamoja na matokeo ya kila kitu ndani yake.

Likisomwa katika wakati wa Shams basi uadui utaondoka na kutapatikana urafiki baada ya uhasama.

Ya Muta'âlî (551) يامتعالى
Jina Tukufu la Ya Mutaali ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye heshima ya juu kabisa katika mamlaka juu ya kila kitu.

Likisomwa katika wakati wa Zuhra basi kutapatikana Ushindi mkubwa sana ndani ya muda mfupi.

Kwa ajili ya kurudishiwa hadhi yako basi soma mara 540 na pia kwa ajili ya kupata mafanikio katika mahojiano ya kuomba kazi au mahkamani.

Kwa mwanammke mwenye maumivu katika wakati wa hedhi basi akisoma jina hili litamsaidia sana kupunguza maumivu.

Ya Bariu (202) يابر
Jina Tukufu la Ya Bariu ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kuanzisha mema na kuwakabidhi Waja wake.

Likisoma katika muda wa Zuhra basi adui atashusha mikono chini na kujisalimisha.

Ukimsomea Mtoto mara 202 basi Mtoto huyo hua ni mwenye kua na Bahati, na ukilisoma wewe mwenyewe basi hukuondolea Mitihani na kukuongezea mapezi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*

Ukilisoma kwa Mwanamke asieshika mimba basi hua ni mwenye kushika Mimba.

Likisomewa kwa Maiti basi maiti hio haitooza.

Kwa mwenye Matatizo basi kama akilisoma matatizo yataisha, ukilisoma mara 7 basi tabia mbaya zitaondoka za mtu. Na akisomewa Mtoto mchanga mara 7 basi mtoto huyo atakua salama kutokana na majanga.

Ya Tawwwab (409) ياتواب
Jina Tukufu la Ya Tawwab ni lenye Kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye sifa Tukufu ya kua ni mwenye kupokea Toba na kusamehe na kuwahimiza waja wake waombe msamaha kwake.

Likisomwa kwenye wakati wa Mushtara basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* humsamehe aliesoma.

Ukitaka kua salama kutokana na madhara ya maadui unayokabiliana nayo basi soma mara 13.

Ya Muntaqim (630) يامنتقم
